

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 28 Juni, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. KAPT. MST.
GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI,
MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE):**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka ya Spika linalomhusu Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge na Shauri la Kusema Uwongo Bungeni linalomhusu Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Mwanne Mcemba.

Na. 452

Mradi wa *MIVARF*

MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. MGENI JADI KADIKA) aliuliza:-

Mradi wa *MIVARF* ni wa Muungano na Makao Makuu yapo Arusha ambapo kazi yake kuu ni kujenga masoko, miundombinu ya barabara, kuongeza thamani na kupeleka maendeleo vijiji:-

Je, ni kwa kiasi gani mradi huu umechangia kuleta maendelezo Zanzibar?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *MIVARF* ni programu inayohusika na miundombinu ya masoko, uongezaji thamani ya mazao na huduma za kifedha vijiji. Miundombinu ya masoko ni pamoja na majengo, barabara, maghala na vituo vya kuongeza mazao thamani. Katika utekelezaji wa programu hii Zanzibar imenufaika kukarabatiwa barabara zenye urefu wa kilometra 144; Unguja kilometra 68; na Pemba kilometra 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara zilizokarabatiwa zimechangia katika kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kushamiri kwa usafiri wa abiria yaani daladala kati ya Kibwegele, Makunduchi, Bwejuu, Vikunguni, Uwandani, Mwachealale na maeneo mengine. Gharama za ukarabati wa barabara hizo ilikuwa ni shilingi bilioni tisa na milioni mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unatarajia kuchangia tena shilingi bilioni nne na milioni mia sita katika kujenga masoko matatu ya ghorofa na yenye vyumba vyatubaki kwa ajili ya kuhifadhia mazao. Kinyasini Unguja, Tibirizi na Konde - Pemba, pamoja na ujenzi wa kituo cha mafunzo juu ya uhifadhi na utunzaji wa mazao baada ya mavuno Pujini – Pemba. Mradi unatarajiwa kujenga masoko 16 Tanzania nzima hivyo, Zanzibar imenufaika kwa asilimia 20 ya idadi hiyo ya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unashughulikia pia na kuhamasisha na kuimarisha shughuli za vyama vyatubaki na kukopa yaani *SACCOSS* ambapo kwa kipindi cha mwaka 2013 mpaka mwaka 2016 *SACCOSS* kwa upande wa Zanzibar zimevezeshwa kukuza mtaji kutoka shilingi bilioni 3.5 zilizokuwepo hadi kufikia shilingi bilioni 10.5. Mikopo nayo imepanda kutoka shilingi bilioni 3.9 mwaka 2013 hadi kufikia shilingi bilioni 15 mwaka 2016. Aidha, idadi ya wanachama hai imepanda kutoka 8,000 mwaka 2013 hadi kufikia 28,000 mwaka 2016.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, swali la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, mradi huu umeleta mabadiliko makubwa sana hapa nchini hususan Tabora; na kwa kuwa fedha zinazotolewa ni kwa awamu na kidogo kidogo. Je, Serikali iko tayari sasa kupeleka fedha hizo vijijini ambako tayari wananchi wana uelewa wa kutumia masoko hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anthony Mavunde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki hasa ya mradi huu ni kwenda kusaidia katika miundombinu ya masoko na barabara hasa katika maeneo ya vijijini. Lengo kubwa hapa ni kusaidia katika kuongeza thamani ya kile ambacho kinafanywa na wakulima. Kwa hiyo, nimwondolee hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba upelekaji wa fedha katika miradi hii unategemeana pia na vigezo ambavyo vimewekwa kwa kila Halmashauri kuweza kuvifikia. Kwa hiyo, tumeendelea kufanya hivyo na tayari mradi huu kama nilivyosema hapo awali umekwishatoa fedha nyingi sana kwa ajili ya huduma hizi.

Mheshimiwa Nailbu Spika, katika maeneo mengine, wale ambao wamekidhi vigezo, fedha hizi zimekuwa zinatoka kwa wakati kwa ajili ya kwenda kusaidia huduma hizi zipatikane kiurahisi. Nimwondoe hofu kwamba fedha hizi zinafika na zinakwenda kwa wakati katika kusaidia malengo yaliyokusudiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ussi Pondeza. Samahani Mheshimiwa, nyuma yako yuko nani? Mheshimiwa Machano samahani, nilikuona kama Mheshimiwa Pondeza.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa *MIVARF* ulikuwa na nia nzuri sana kuwasaidia wananchi wa Tanzania. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kwa upande wa Zanzibar tumeepata fedha na miradi, lakini katika utekelezaji wake inaonekana miradi hii haikuzingatia sana *value for money* na barabara ambazo zimejengwa kupitia mradi huu sasa hivi zimeharibika na hazipitiki ndani ya mwaka mmoja. Pia Wizara ya Kilimo ambayo imesimamia bado

hawajazikabidhi kwa Wizara ya Ujenzi Zanzibar. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda kuzitembelea barabara hizi na kuzifanyia ukarabati?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa upande wa soko la Kinyasini nalo pia limejengwa chini ya viwango. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu suala hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza ameniomba kama nina uwezo wa kwenda kuzitembelea. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi binafsi pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria tulikwishafika katika eneo hilo. Tulitembelea na tulitoa maoni ya Kamati ambayo tulishaagiza Watendaji pale Zanzibar waweze kuyafanya kazi na hasa katika hili eneo ambalo amelisema la miundombinu, kwa sababu katika baadhi ya zile barabara ambazo tulizitembelea tayari *MIVARF* kwa maana ya programu na Halmashauri ya Wilaya pale waliingia makubaliano kwamba Manispaa inazichukua kwa ajili ya kuzi-*upgrade* na kuendelea kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tayari tulishafika katika eneo hilo, tumeziona na kuna hayo makubaliano ambayo yanaendelea. Pia nami nikipata fursa zaidi nitakwenda kuzitembea na kuhakikisha kwamba yale ambayo tumekubaliana yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii la pili la soko la Kinyasini, nilisema katika majibu yangu ya msingi ya kwamba mradi huu pia unatarajia kuchangia kiasi cha shilingi bilioni nne na milioni mia sita, ambazo ukiacha shughuli nyingine zitasaidia katika ujenzi wa ghorofa yenye vyumba vyaa baridi katika eneo la Kinyasini – Unguja, Tibirizi na Konde pia Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia katika mradi

huu, kazi kubwa sana imefanyika Zanzibar na ukiangalia kuanzia katika sehemu ya Kaskazini Unguja, maeneo ya Donge, Vijibweni, Pwani, Donge Mnylimbi, kote huko shughuli zimefanyika kupitia mradi huu. Vilevile katika maeneo ya Mjini Magharibi kule Mwakaje, Mwera, Fuoni, Kibondeni nako pia kazi hizi zimefanyika. Kwa hiyo, nimwondoe hofu kwamba hata hayo mengine yote aliyoasema tutakuja kuyapitia na kuona namna gani mradi huu unaendelea kutekeleza. Huu ni mradi ambao una manufaa makubwa sana Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rehani, swali fupi.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naitwa Mheshimiwa Mpakate. Napenda kuuliza swali la nyongeza. Katika maeneo yanayozalisha korosho, mfumo wa stakabadhi ghalani umesaидia sana wakulima kuongeza kipato, lakini moja ya changamoto inayokumbana nayo ni matatizo ya maghala katika vijiji vyetu katika maeneo yote ambayo yanalinwa korosho. Mradi wa *MIVARF* ungeweza kusaidia kujenga maghala kila Kata angalau ghala moja moja ili kuwapunguzia wakulima gharama ya kusafirishia korosho. Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa kujenga angalau ghala moja kila kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili kuwapunguzia wakulima wa Tunduru gharama ya kusafirisha korosho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mradi huu jambo kubwa ambalo linaangaliwa ni miundombinu ya masoko, barabara, lakini vile vile na huduma za kifedha kijijini. Katika eneo la miundombinu ya masoko jambo ambalo linaangaliwa pia ni suala la ujenzi wa maghala. Sasa katika programu hii yako maeneo ambayo tayari maghala yamejengwa lakini siwezi kutoa ahadi ya Serikali hapa kwamba tutajenga katika kila Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikoa ile ambayo inazalisha zao la korosho, kwa mfano, Ruvuma na Mtwara tayari maghala haya yapo, lakini kutoa ahadi ya kwamba tutajenga kila Kata Mheshimiwa Mbunge hii inategemeana pia na bajeti na programu jinsi tulivyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia katika ile mikoa ambayo tuliona umuhimu huo na ndiyo maana katika Mikoa ya Ruvuma na Mtwara tayari maghala haya yamekwishajengwa. Kwa hiyo, tunaamini kabisa labda baadaye fedha ya ziada ikipatikana hiyo inaweza ikawa sehemu ya *consideration*, lakini kwa sasa kama Serikali na kupitia programu hiyo hayo ndiyo maeneo hasa ambayo tumeanzia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa, Waheshimiwa Wabunge waielewe programu hii ya *MIVARF*, programu hii ni shirikishi, Mheshimiwa Mbunge anaomba ni kwa nini programu hii isiwe inajenga maghala tu. Tunachokifanya sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, tunatafuta fedha na tunatengeneza *plan* ya nini kitafanyika kwenye fedha hiyo. Jukumu la kuamua aina ya mradi utakaoteklezwa kwenye Halmashauri husika ni jukumu la Halmashauri yenywewe na sio jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachokifanya sisi, tunapeleka aina za miradi, Halmashauri kupitia vikao halali vyta kikanuni inaamua aina ya miradi katika Halmashari yao. Kwa hiyo, tunachotaka kusema hapa kama fedha hii itapatikana tena kwa sababu ni mradi ambao unaenda kwa *phases*, kama fedha itapatikana tena, Halmashauri zikishapelekewa miradi hii basi waamue aina ya miradi kwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuzingatia hali halisi ya mazingira waliyonayo na shughuli wanazozifanya na Ofisi ya Waziri Mkuu tutakubaliana nao lakini sio wajibu wetu kuwaamulia wao nini kikafanyike kwenye mradi katika Halmashauri yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, katika maeneo ambayo miradi imefanyika wametupa ushirikiano wa kutosha. Nawapongeza sana na kama kuna tatizo lolote tunaomba tuendelee kuwasiliana ili miradi hii itekelezwe kwa viwango vinavyotakiwa huku ikisimamiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, sasa aulize swali lake.

Na. 453

Kuwabambikiza Kesi Wananchi

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Kutokana na wananchi wa vijiji kuwa na uelewa mdogo wa masuala ya sheria na haki zao, Watendaji wa Vijiji na wa Kata wakishirikiana na Mahakama za Mwanzo na Mabaraza ya Ardhi huwaonea na kuwadhlumu kwa kuwabambikizia kesi na kuwanyang'anya ardhi:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za kukomesha tabia hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo malalamiko dhidi ya baadhi ya Watendaji wa Kata na Vijiji ambao wamekuwa wakilalamikiwa na viongozi na wananchi kuwabambikizia kesi na kushirikiana na Mahakama za Mwanzo na Mabaraza ya Ardhi kuwaonea na kuwadhulumu ardhi wananchi hao kwa kuwanyang'anya ardhi yao. Serikali inakemea vikali tabia ya baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu na ambao wanakiuka maadili ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha tabia hii, Serikali inaelekeza kwa viongozi na watendaji mambo yafuatayo ya kuzingatia:-

(i) Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahakikishe wanasmamia uzingatiaji wa maadili ya watendaji walio chini yao.

(ii) Watendaji wote katika ngazi zote za mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, miiko na maadili katika utekelezaji wa majukumu yao.

(iii) Serikali haitasita kumchukulia hatua Mtendaji ye yeyote atakayekiuka sheria, kanuni, taratibu na maadili ya kazi yake, ikiwemo kujihusisha na tabia ya ubambikizaji kesi wananchi na kuwanyang'anya ardhi;

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha inasimamia kikamilifu maadili ya watumishi wa umma ili kuongeza nidhamu katika utumishi wa umma na haitasita kuchukua hatua mara moja dhidi ya Mtendaji ye yeyote wa Kata au Kijiji atakayethibitika kutumia vibaya madaraka yake ikiwemo kubambikia kesi wananchi kwa lengo la kuwanyang'anya ardhi. Nitoe wito kwa viongozi na wananchi wote nchini kuhakikisha wanafichua utendaji na watumishi wa umma wenye tabia kama hii ili waweze uchukuliwa hatua stahiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kafumu, swali la nyongeza.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna dhuluma sana mionganini mwa wananchi wetu, ni lini sasa Serikali itachukua hatua kwa sababu kuna matukio mengi sana ambayo siwezi kuyaorodhesha hapa, yako kule kwenye Jimbo la Igunga ambapo wananchi wengi sana wamedhulumiwa. Ni lini sasa Serikali itachukua hatua hizo badala ya kutoa onyo tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kwenye Kijiji cha Lugubu, kijiji kiliamua kutenga eneo moja kuwa eneo la hifadhi, lakini kwa bahati mbaya baadhi ya watendaji waliwaruhusu wananchi wawili waingie kwenye hilo eneo na kukazuka mgogoro mkubwa sana wa ardhi ambaao Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Mwanzo wameshindwa kuurekebisha huo mgogoro. Je, ni lini sasa Serikali itatusaidia jambo hili ili tuweze kutenga eneo katika Kijiji hicho cha Lugubu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba lini tutaanza kuchukua hatua naomba nikuhakikishie kwanza naomba ikiwezekana atupe orodha sasa hivi, kama kuna watu wa aina hiyo basi tuanze kuelekeza mara moja jinsi gani watu ambaao wanakwamisha haki za watu ambaao wanadhulumu kwa makusudi na wao wamepewa dhamana tuweze kuwachukulia hatua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nimsihi kama ana orodha sasa hivi naomba aikabidhi kwangu tuweze kuifanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine katika Kijiji cha Lugugu ambalo amezungumza kwamba kuna eneo la kijiji limetengwa lakini kuna watu wawili wamekabidhiwa eneo hilo, eneo ni mali ya kijiji, kwa kweli inatia huzuni. Katika hili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutalifanya kazi. Naomba nimwelekeze Mkuu wetu wa Wilaya ya Igunga aweze kufanya uchunguzi wa haraka katika eneo hilo kipi kinachojili ili mradi mwisho wa siku haki ya wananchi iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hilo halitavumilika hata mara moja na kwa vile nimekubaliana na Wabunge wa Mkoa wa Tabora kwamba nitakwenda Mkoa wa Tabora lakini nitakuwa na *interest* ya kufika eneo hilo kwenda kujua ni ubadhirifu gani unaofanyika amba unanyima haki za watu, lengo kubwa tuhakikishe wananchi wanapata huduma inayotakiwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkundi swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa kukosa fedha za kuendeshea shughuli za Mabaraza ya Ardhi ya Kata ni kichocheo kikubwa sana cha rushwa kinachopelekea wananchi wengi kunyimwa haki zao za msingi. Sasa Serikali haionti sababu na umuhimu sasa itoe ruzuku kwa Mabaraza haya ili yaweze kuendesha shughuli zake na kuondoa uwezekano wa kuchukua rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa kesi kubwa nyingi sana kuja kuziangalia hata maamuzi mengine yanakuwa yanababishwa na baadhi ya wale amba wako katika Mabaraza ya Kata. Wakati mwingine inaonekana kwamba mtu aliyenacho ndiyo huyo ambaye

haki inamwendea, hili ndiyo maana Serikali ilikuwa inafanya tathimini kwa kina sana kuangalia nini kifanyike katika suala zima katika uendeshaji wa Baraza la Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge tunalichukua lakini kuna mchakato mpana tunaufanya kuona jinsi gani tutaboresha haya Mabaraza ya Kata yaweze kufanya kazi vizuri zaidi kulinganisha na hivi sasa kwa sababu haki nydingi za watu zinapotea kwa sababu haki haisimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wazo hili tunalichukua, lakini tunajumuisha mionganoni mwa mambo ya kufanya *restructuring* tuifanyeje, lengo kubwa la Mabaraza hayo yaweze kufanya vizuri, kwa hiyo, ni wazo zuri tunalichukua kama Serikali kulifanya kazi kwa mpango.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama alivyojibu mjibu swali, kwa kuwa hawa Wazee wa Mahakama wanalipwa nafikiri Sh.5,000/= au Sh.7000/=. Je, huo mchakato wanaoufanya wanajiandaa kuongeza kiwango cha hawa Wazee kwa sababu ni kazi ya hiyari? Isije kuwa wanashindwa kwenda Mahakamani ndiyo maana haki inachelewa kupatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapa Mheshimiwa Bulembo kwamba tunachokifanya ni kufanya tathmini ya kina jinsi gani tutafanya kuhakikisha wananchi wanapata haki. Siwezi kusema kwamba kiwango hiki kitaongezeka kwa sababu kuna mambo mengi ndani yake yanaendelea hapa, isipokuwa kwamba tuamini Serikali inafanya kazi na mwisho wa siku ni kwamba mionganoni mwa kuondoa kero nydingi za wananchi

ni kushughulikia Mabaraza ya Kata, ili kulinda haki za watu kwa kuyashughulikia na kuyaunda vizuri Mabaraza ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inafanya kazi hii hatima yake itakapofika, basi tutapata mwelekeo maalum wa Serikali wa jinsi gani jambo hili tunaenda kuli-*handle* vizuri kwa maslahi mapana ya wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali fupi.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, sababu mojawapo ya utendaji mbovu wa Mabaraza ya Ardhi ni kwa sababu hawana weledi na mafunzo ya kutosha; na kwa kuwa pia Halmashauri ndiyo yenye jukumu la kuwapa mafunzo Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Halmashauri hizi hazina pesa, Serikali inaonaje kupiga marufuku Mabaraza ya Ardhi ambayo hayajapata mafunzo ya kutosha kufanya kazi yake mpaka hapo yanapokuwa yamepata mafunzo ya kutosha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupiga marufuku kwamba Mabaraza yasifanye kazi jambo hilo naomba niseme kwamba hatuwezi kupiga marufuku hapa, isipokuwa tunachotaka kufanya ni kwamba niwasihii hasa Wakurugenzi wa Halmashauri zetu zote 185 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pale inapobainika kwamba kuna Mabaraza ya Kata ambayo uelewa wao ni mdogo katika utaratibu tunaokwenda nao katika kuyaboresha kipindi hiki cha mpito, lazima wahakikishe wanatumia ile *staffing* yao iliyokuwa katika Halmashauri kuona watafanyaje kuhusu *capacity building* kwa watu hawa, lengo kubwa waweze kutoa haki stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hoja ya msingi, kwa hiyo, hatuwezi kusitisha hivi sasa, lakini tutaendelea kuwasihii Wakurugenzi wetu wa Halmashauri zetu wafanye *capacity*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

building kwa kushirikiana na Wanasheria tuliokuwa nao, lengo kubwa likiwa, Mabaraza haya yaweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini.

Na. 454

Mradi wa Maji katika Kijiji cha Ngomalousambo

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Tangu mradi wa maji katika Kijiji cha Ngomalousambo ukamilike haujawahi kutoa maji hata kidogo:-

Je, ni sababu zipi zilizofanya mradi huo usitoe maji kama ilivyokusudiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Kijiji cha Ngomalousambo chenye jumla ya wakazi 1,672 ulianza kujengwa mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2015 kwa gharama ya shilingi 268.9. Mradi huo unategemea jenereta ya dizeli inayopampu maji kutoka kwenye kisima kwenda kwenye tenki. Mradi huu umeshindwa kutoa huduma kwa wananchi kutokana na kuibowi betri ya pampu iliyofungwa katika mradi huo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imekamilisha ununuzi wa betri mpya na kuifunga wananchi wa Ngomalousambo wameanza kupata maji kuanzia tarehe 22 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ina mpango wa kuchimba kisima kingine katika mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kuwezesha mradi huo ufanye kazi kwa ufanisi kutokana na kisima kilichopo sasa kupoteza uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wizi wa betri uliojitokeza hapo awali, Serikali inatoa wito kwa wananchi wa Kijiji cha Ngomalusambo kulinda mradi huo kwa manufaa ya wananchi wote. Napenda kusisitiza kuwa, Serikali haitasita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kwa uharibifu wowote wa miradi ya maendeleo kwa maslahi ya watu binafsi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Moshi Kakoso, swalii la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Niulize sasa maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa msimamizi wa mradi huu aliyejenga mradi wa maji wa Kijiji cha Ngomalusambo alijenga chini ya kiwango, ikiwa ni pamoja na kufunga pampu ya kusukuma maji ambayo haina uwezo na haikuwa stahili iliyokuwa imelengwa. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Mkandarasi na Msimamizi aliyejenga mradi huu chini ya kiwango na kuipotezea Serikali kiasi kikubwa cha fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, miradi mingi ya maji imekuwa na tatizo ya usimamizi mbovu kiasi kwamba miradi inayoelekezwa haitengenezwi vizuri. Mfano pale Kijiji cha Majalila kulikuwa na mradi mkubwa wa maji ambao Serikali imetoka fedha nyingi lakini ilipangia kujengewa vituo vya maji 28 vikajengwa 12. Je, msimamizi wa mradi huu wanachukua hatua gani ili aweze kuwajibishwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa Ngomalusambo kwamba imefungwa mashine ambayo

iko chini ya kiwango siwezi kulizungumza hapa sasa, lakini kwa taarifa nilizozipata ni kwamba ule mradi ulianza lakini *charging capacity*yake kile kisima imekuwa kidogo, kwamba pampu inafungwa lakini ikisukuma maji sasa hivi wanasukuma takribani masaa 18 wanavyotumia *diesel* maana yake gharama inakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni taarifa ambazo nilizipata kwa wataalam wangu. Hata hivyo, *concern* aliyozungumza Mheshimiwa Mbunge naomba tufanyie kazi, kwenda kufanya uchunguzi je, ni kweli kisima kimepoteza uwezo au pampu iliyofungwa haina uwezo. Maana yake mpango uliopo sasa hivi katika Halmashauri ya Mpanda ni kwenda kuchimba kingine kuhamisha ile mitambo iendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Mbunge anasema pampu iliyofungwa haina uwezo basi hili maana yake ni jambo kubwa sana lazima tukalifanyie kazi na ikiwezekana tuunde Tume maalum kwenda kuchunguza kwamba kipi kinachojili katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika katika mradi wa Majalila na Mbunge anakumbuka siku ile tulivyofika pale tulikuta ule mradi upo *idle* pale katika Wilaya Tanganyika haufanyi kazi. Nikatoa maelekezo na nimepata taarifa mradi ule umeshaanza kufanya kazi, lakini inaonekana kwamba kuna changa la macho, badala ya vituo vyatya maji 24 vimefungwa 12 maana yake hapo kuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matatizo hayo yote, kama hali ipo hivyo, Ofisi ya TAMISEMI hatuwezi kuridhika na hali hiyo. Naomba nimhakikishie tutaunda Tume maalum kutoka ofisini kwangu kwenda kufanya uchunguzi wa miradi hiyo miwili, lakini siyo hiyo miradi miwili na ile miradi mingine minne inayoendelea, kuweza kubaini kwamba ni tatizo gani linaendelea lengo kubwa tuweze kulinda fedha za Serikali na kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Mheshimiwa

Mbunge kimesikika, tunaenda kukifanyia kazi kama tulivyofanya kazi Mkao wa Geita na maeneo mengine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga swalii nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Miradi ya *World Bank*, miradi ya maji mikubwa ya *World Bank Kijiji* cha Rungu, Wilaya ya Mbozi lakini pia kuna mradi mwininge Kijiji cha Ihanda tangu imezinduliwa na Mwenge miradi hii haijawahi kutoa maji. Sasa naomba niulize kwa nini miradi inazinduliwa na mwenge lakini haitoi maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja siyo miradi ya kuzinduliwa na Mwenge haitoi maji, nafikiri hoja ya msingi ni kwa nini mradi umezinduliwa lakini hautoi maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasihii Wabunge sisi ni Wajumbe wa Kamati za Fedha, Wajumbe wa Baraza la Madiwani. Tusikubali hata siku moja, mradi ambao tunasimamia katika Kamati ya Fedha watu wanakuja kufanya kanyaboya, mradi unazinduliwa hautoi maji na wewe Mbunge upo, niseme kwamba jambo hili ni la kwetu sote. Mheshimiwa Haonga naomba niseme kwamba hili la kwetu sote hatuwezi tukakubali katika jambo hili, kama mradi huo hautoi maji na kwa vile tumekubaliana kwamba baada ya Bunge hili tunakwenda kupiga kazi ngumu Mkao wa Songwe, tupitie huo mradi twende tukabaini kitu gani kinachoendelea hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku tulinde fedha hizi ambazo wananchi wana shida kubwa ya maji hatuwezi kukubali, sio mbio za mwenge peke yake isipokuwa kiongozi yoyote au mradi wowote unaozinduliwa ni lazima ufanye kazi kama unavyokusudiwa. Kwa hiyo, naomba

nimsihi nikifika pale, hata kama ratiba yangu haijawekwa huko naomba aniambie kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ule mradi uko hapa, lazima tufike hapo *sitetwende* kuangalia nini kinaendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri bora umesema unakwenda Songwe yote maana na Mheshimiwa Frank Mwakajoka naona anasimama tena. Mheshimiwa Lubeleje swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Katika Wilaya ya Mpwapwa, Vijiji vya Bumila, Mima na Iyoma vilichimbwa visima vya maji na maji yalipatikana, sasa ni miezi nane hakuna cha bomba, hakuna cha pampu. Sasa nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri vile visima vilichimbwa kwa ajili ya mapambo kuonyesha wananchi tu au ni lini wataweka pampu na mabomba wananchi wanapata tabu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tulishazungumza naye na nimeshazungumza ndani ya Bunge lako hili Tukufu, ukishachimba kisima maji yakapatikana Mkurugenzi unatakiwa utengeneze *quotation* ya kununua pampu. Ukishatuletea *quotations* sihiyo tunaiweka kama ni *certificate* tunakupa hela ili uende ukununue pampu na pampu hizi zifungwe wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama tulivyoongea nje kwamba amwambie Mkurugenzi wake wa Halmashauri atengeneze *quotation* na kama hana huo utaaliam basi tuwasiliane ili Wizara ya Maji na Umwagiliaji, tutume mtaalam wetu akamsaidie Mkurugenzi wake wananchi wapate maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swali la nyongeza.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo Ngomalusambo Wilayani Mpanda la mradi wa maji kukamilika lakini hautoi maji halina tofauti na mradi wa maji uliopo Wilayani Tunduru Kijiji cha Nandembo. Mradi ule ultumia mamilioni mengi ya shilingi lakini mpaka hivi tunavyozungumza wananchi wale hawapati maji. Napenda kujua ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha sasa huduma hiyo inapatikana ipasavyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna sababu inawezekana mradi mwingine kwa mfano juzi juzi nilikuwa na ndugu yangu Kibajaji hapa katika Kijiji chake cha Manzase mradi umekamilika lakini tatizo kubwa lilikuwa ni suala zima la *power*, kwamba nishati ya aina gani iweze kutumika, kwa hiyo *case by case* hii miradi haitoi maji kwa sababu maalum. Inawezekana sehemu nyingine pampu hazijakamilika, hazijanunuliwa au mradi haufanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *case* ya Mheshimiwa Mbunge, sifahamu mradi huo ukoje. Jambo ninalotaka kulifanya tukitoka hapa naomba anipe takwimu halisi ni kitu gani kinachoendelea pale tutoe maelekezo ya stahili nini kinachotakiwa kufanyika, kwa sababu najua miradi hii inakwama katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo Mheshimiwa Sikudhani naomba anijulishe baadaye kuna kitu gani pale kinachoendelea, tutoe maagizo mahsusni katika suala zima la mradi tuweze kuwasaidia wananchi wake waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nilimwona Mheshimiwa Musukuma hapa akisimama kwa ajili ya mradi wake wa Changorongo, naamini alitaka kusimama kwa hoja

hiyo. Mheshimiwa Msukuma kwa sababu tumekubaliana hapa mionganii mwa jambo tunalotaka kwenda kulifanya baada ya Bunge kutembelea ile shule ya msingi tutafika hapo kwa ajili ya kujibu lile swali kwa ajili ya wananchi wa Geita pale ambao muda mrefu tumewapigia kazi waweeze kupata huduma inayostahili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msukuma nadhani swali lako limeshajibiwa sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri hukuwaona Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Jacqueline? Mheshimiwa Mwamoto swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri sasa naomba niulize swali moja. Kwa kuwa, miradi ya maji imekuwa ikisumbua sehemu nyingi hata Wilaya ya Kilolo imekuwa haliishi vizuri na kwa kuwa kuna watu wanaitwa Wakandarasi Washauri wamekuwa wakilipwa pesa kwa ajili ya kushauri miradi yetu ili iende vizuri pale inapokuwa imeharibika wanachukuliwa hatua gani hawa Wakandarasi Washauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba huyu Mkandarasi Mshauri au *Consultant* kwenye usajili wake akipata kazi yoyote ya Serikali kuna kitu kinaitwa *Design Liability Insurance*. *Insurance* hiyo inalinda *performance* ya kazi yake na kama hakufanya vizuri kuititia kwenye ile *insurance* au kuititia kwenye ile *bond* basi anatakiwa arudishe hela kama mradi haukufanyika vizuri. Kwa hiyo, kama haujafanyika vizuri kwenye eneo lake naomba sana Mheshimiwa Mbunge awasiliane na TAMISEMI au na Wizara ya Maji ili tuweze kumwajibisha huyo Mhandisi Mshauri. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, swali fupi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji la Mpanda Vijijini linalingana kabisa na tatizo la mradi wa maji wa *World Bank* katika kata ya Mkako, Wilayani Mbinga lakini pia katika Kata ya Litola, Wilayani Namtumbo na Kata ya Luwiko, Wilayani Songea Mjini, naomba kujua kwamba miradi hii imeonesha tayari imekamilika kwa mujibu wa taarifa, lakini haitoi maji hata kidogo, kiasi ambacho inaleta tafrani kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasanaomba nijue kwamba je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi katika Mkoa wangu wa Ruvuma kwenye maeneo haya niliyoyataja ili kuona hali halisi ya miradi hiyo na kuweza kuikamilisha ili wananchi, wanawake wote wa Mkoa wa Ruvuma kwenye maeneo hayo wapate maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kumjibu kwa haraka tu kwamba mimi nipo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba...

NAIBU SPIKA: Nilifikiri umeshamaliza, maana lilikuwa ndilo ombi lake.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Naomba nitoe maelekezo mahsuswi kwamba karibu maeneo mengi miradi hii ina matatizo. Naomba niwaagize Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote 185 by tarehe 20 mwezi Julai tupate takwimu za miradi yote iliyokamilika ipi inatoa maji na ipi haitoi maji tuje na suluhisho la kusaidia wananchi wetu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo tunaona kwamba, tumepata takwimu hiyo, baadaye tunaona kwamba, Mbunge analalamikia mradi fulani, lakini katika orodha haupo, tutajua kwamba, mradi ule umehujumiwa makusudi na Halmashauri husika. Kwa hiyo, hatutosita kuchukua hatua stahiki kwa watu wote ambao kwa njia moja au nyingine wameshiriki kuhujumu hii miradi, mwisho wa siku wananchi wanashindwa kupata huduma hii ya maji. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, sasa aulize swali lake.

Na. 455

Matumizi ya Kuni na Nishati Mbadala

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Hitaji la kuni limekuwa kubwa kwa matumizi kama nishati ya kupikia na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira:-

Je, Serikali itawezesha vipi wananchi kupata nishati mbadala kwa matumizi ya kupikia majumbani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y.
WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Uendelezaji na Usambazaji wa Teknolojia za Kilimo Vijiini (*CAMARTEC*) inaendelea na ujenzi wa mitambo ya bayogesi nchini kwa ajili ya kupikia na matumizi mengine majumbani, taasisi za Serikali zikiwemo shule, hospitali na

Magereza. Hadi sasa mitambo ya bayogesi iliyojengwa inafikia 20,000. Lengo la kituo ni kujenga jumla ya mitambo 22,000 kwa nchi nzima ifikapo mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) ilianza kutekeleza mradhi wa kusambaza gesi asilia katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kupitia mradhi wa mfano (*Pilot Project*) kwa ajili ya kupikia majumbani. Hadi sasa hoteli tatu, gereza moja, nyumba 70 na viwanda 36 vinatumia gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara. Miradi ya usambazaji wa gesi asili katika mikoa hiyo utaanza mwaka 2018 na kukamilika mwaka wa 2020/2021 kwa kuwafikishia gesi wateja wapatao 50,410. Miradi hii itagharimu jumla ya dola za Marekani milioni 126.959.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2017, Serikali kupitia *TPDC* itaanza kutekeleza mpango wa kupeleka gesi majumbani katika mikoa mingine ya Tanzania Bara ili kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na huduma hii.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nipate kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina nia njema ya kupeleka nishati mbadala katika maeneo mbalimbali ya Tanzania; na kwa kuwa, Jimbo la Kavuu lina idadi kubwa ya wafugaji na kinyesi cha wanyama kinapatikana kwa wingi hasa ng'ombe, nguruwe na mbuzi. Pia, kwa kuwa, bado hatuna mtandao mzuri wa majitaka katika miji mingi ya vijijini ikiwemo Jimbo langu la Kavuu. Je, Serikali sasa haionti ni wakati muafaka kupitia taasisi za *TADETO* na *UN Habitat* katika kuanzisha miradi ya *biolatrine* ambayo inatumia kinyesi cha binadamu katika maeneo ya mashule, ili tuweze kupata gesi ya uhakika

kutokana na kwamba sasa uharibifu wa mazingira katika Jimbo la Kavuu umekuwa mkubwa especially katika kukata miti hovyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, naomba niulize si kwa Serikali na Watanzania kwa ujumla, je, matumizi ya mkaa na gesi yapi ni bora zaidi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kwamba, Serikali inaupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa tufanye utafiti wa kutosha ili tuweze kutumia *human waste* kutoka kwenye *pit latrins* na ku-convert kuwa *energy* ambayo inaweza ikasaidia matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, Serikali iko tayari kutumia hii taasisi ya *TADETO* ambayo tayari imeshafanikisha miradi miwili Dar es Salaam kwa kujenga *bioelectric* ambayo sasa hivi inatumika kwenye sekondari mbili pale Dar es Salaam ikiwemo Sekondari ya Manzese. Teknolojia hii inatumiwa zaidi na Uganda kwenye shule za sekondari na shule za misingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake pili kuhusu yapi matumizi bora, tutumie gesi au tutumie mkaa. Ni bora kutumia gesi kwa sababu kwanza gesi bei yake ni nafuu ukilinganisha na bei ya mkaa. Kwa mfano, Dar es Salaam gunia moja la mkaa la kipimo cha kawaida ni Sh.75,000/= lakini ukienda kwenye teknolojia ya nguvu gani inapatikana katika mkaa, wataalam wameshafanya vipimo wakaona kwamba, tunapata *unit* 2.645 kwenye gunia la mkaa ni *energy* ambayo inayojulikana kwa kwa jina la *Gigajoule*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, *unit* moja ya gunia la mkaa inauzwa kwa Sh. 28,000/=, lakini ukienda kwenye gesi *unit* moja inauzwa kwa shilingi 18,000. Pia,

ukitumia gesi tayari unakuwa umeshaokoa mazingira yetu, watu wa mazingira ukikata miti unaleta uharibifu wa mazingira ambao unaweza ukatuathiri kwenye mambo mengine kama kutopatikana kwa mvua inayostahili kwa masuala ya kilimo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 456

Ukosefu wa Umeme Katika Kata za Jimbo la Mufindi

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mtambula, Idunda, Itandula, Kiyowela, Idete, Maduma na Nyololo Shuleni?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y.
WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi kabambe wa usambazaji umeme vijiji awamu ya tatu umeanza kwa nchi nzima tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele-mradi vitatu vya *Densification, Grid Extension* na *Off-Grid Renewable* ambayo inalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji na vitongoji ambavyo havikufikiwa na miundombinu ya umeme. Kata za Idete, Idunda, Itandula, Kiyowela, Mtambula, Maduma pamoja na Kata nyingine za Wilaya ya Mufindi zimejumuishwa katika utekelezaji wa mradi wa *REA* awamu ya tatu wa *Grid Extension* utakaokamilika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vya kata hizo itahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 153.65; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4, yenye urefu wa kilometa 233; ufungaji wa transfoma 92, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 3,225. Gharama ya kazi hii ni shilingi bilioni 14.1. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mendrad Kigola, swali la nyongeza.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika awamu ya pili ya *REA* ambayo imekwisha kuna vijiji ambavyo havijapitiwa na katika upelekaji wa umeme ule ulienda kwenye makao makuu ya kata. Kwa mfano, pale Malangali Vijiji vya Isinikini, Kingege, Ibangi na Ikaning'ombe pale bado havijapata umeme. Je, Serikali itarudi kwenye kutekeleza ile ambayo ilikuwa ni awamu ya pili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ilisema kwamba itapeleka umeme kwenye vituo vya afya, zahanati, pamoja na shule za sekondari na shule za msingi, lakini mpaka sasa hivi shule za msingi bado hatujaona programu kwamba, Serikali inapeleka. Je, katika awamu hii ya tatu mnatuhakikishia kwamba, katika maeneo haya niliyoyataja watapewa umeme?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme utekelezaji wa miradi ya umeme unafanana sana na miradi ya maji. Katika utekelezaji wa miradi ya umeme Wilaya zote kwa sasa wanafungua Ofisi za *TANESCO*. Awamu ya pili amesema kwamba, kuna vijiji ambavyo vimeachwa, kama tayari Ofisi ya *TANESCO* iko pale, basi wale ambaao hawajapata

wapeleke maombi kwenye zile ofisi ambazo zitaendelea kufanya *extension* ikiwa ni pamoja na kuingiza umeme kwenye majumba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, Taasisi za Serikali naomba sana Mheshimiwa Mbunge kwamba, kukishakuwa na ofisi ni vema hizo taasisi za Serikali kama zina mahitaji ya umeme na ni lazima zina mahitaji ya umeme, basi ni kuwasiliana na ofisi zilizopo jirani kupeleka maombi, ili waweze kufikiriwa kupelekewa umeme kwenye hizo taasisi. Kama bajeti itakuwa haitoshelezi kwenye ofisi za Wilaya au Mkao wao basi wata-forward moja kwa moja hayo mahitaji Makao Makuu ya TANESCO ili waweze kupatiwa pesa au waweze kuingiza hizo shule na taasisi za Serikali ziweze kuingizwa katika mradi mkubwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 457

Serikali Kushindwa Kesi Mahakamani

MHE. AIDA J. KHENAN aliuliza:-

Mara kwa mara Serikali imekuwa ikishindwa kesi mbalimbali Mahakamani:-

Je, Serikali imefanya uchunguzi na kujua sababu za kushindwa kesi mara kwa mara?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge hakutaja aina ya kesi anazomaanisha katika swal lake, nianze kwa kufafanua kwamba, kuna aina mbalimbali za kesi au mashauri yanayofunguliwa Mahakamani na Serikali au dhidi ya Serikali. Mfano, mashauri ya jinai, madai, katiba, uchaguzi na kadhalika. Kwa ujumla mashauri hayo hufunguliwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, vilevile Halmashauri, Mashirika ya Umma, Taasisi, Wakala wa Serikali na Idara za Serikali zinazojitegemea zinayo mamlaka ya kuendesha na kusimamia mashauri yanayofunguliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashauri yote yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali yamekuwa yakiendeshwa kwa weledi na pale inapostahili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikiratibu uendeshaji wa mashauri hayo na takwimu zetu zinaonesha mashauri mengi Serikali inashinda. Kwa mfano, kati ya mashauri 53 ya kupinga Uchaguzi wa Ubunge yaliyofunguliwa Mahakamani baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, Serikali ilishinda mashauri 52 na kushindwa shauri moja tu na katika mashauri 199 ya kupinga Uchaguzi wa Madiwani, Serikali ilishinda kesi 195.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama takwimu zinavyoonesha si kweli kwamba, Serikali imekuwa ikishindwa kesi mara kwa mara. Hata hivyo, katika nchi yoyote inayozingatia uhuru wa Mahakama na utawala wa sheria, Serikali haiwezi kushinda kila shauri hata kama haistahili. Ni kweli kuna baadhi ya kesi ambazo Serikali inashindwa, sababu zinazosababisha Serikali kushindwa baadhi ya mashauri ni pamoja na namna ushahidi ulivyokusanywa na vyombo vyta Serikali, kutokupatikana mashahidi muhimu, mashahidi kutokutoa ushahidi uliotegemewa, baadhi ya Taasisi, Mashirika ya Umma na Idara za Serikali kutoishirikisha mapema ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, zinapofungua au kufunguliwa mashauri Mahakamani, namna ushahidi unavyochukuliwa Mahakamani, mashahidi kula njama na kutoa ushahidi unaoathiri mashauri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na

changamoto hizo, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa ikiwemo kuhakikisha kuwa, mashahidi muhimu wanapatikana, kuwaandaa ipasavyo mashahidi kabla ya kutoa ushahidi, kuijandaa vema katika kila shauri, kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi ipasavyo, kushirikiana na vyombo vya Upelelezi kama TAKUKURU na Jeshi la Polisi katika maeneo yanayosababisha ushahidi kuwa hafifu na kurekebisha kasoro hizo, kukata rufaa na kuendelea kuzishauri taasisi za Serikali kutoa taarifa mapema kwa Mwanasherri Mkuu wa Serikali katika kila shauri liliofunguliwa Mahakamani, ili kwa pamoja kuangalia namna ya kulinda maslahi ya Serikali katika shauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuptitia Bunge hili sheria zinazosimamia Mashirika na Taasisi za Serikali zimekuwa zikirekebishiwa na kuweka masharti yanayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kuingilia kati shauri lolote liliofunguliwa dhidi ya Serikali au Taasisi ya Umma kwa lengo la kulinda maslahi ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenan, swalii la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, Halmashauri nyingi nchini zinapopelekwa Mahakamani zinashindwa kesi, hali inayoonyesha ni jinsi gani Wanasheria wetu wa Halmashauri wanashindwa kuwashauri vizuri Wakuu wa Idara na kusababisha hasara kwenye Halmashauri zetu. Serikali ina utaratibu gani wa kufuatilia weledi wa Wanasheria wetu kwenye Halmashauri ili kuepusha hasara zinazotokea kwenye Halmashauri zetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; katika kesi za usuluhishi nje ya nchi napenda kufahamu, ni kesi ngapi tumeshinda kama Serikali na zippi tumeshindwa ikiwepo ya *DOWANS, IPTL* na nyinginezo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Swali la pili kama utakuwa hauna takwimu kanuni zinakuruhusu kuleta takwimu baadaye.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA): Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anauliza namna ambavyo Serikali inaweza kufuatilia weledi wa Mawakili katika Halmashauri ambao wamekuwa wakisababisha hasara kwa Halmashauri kushindwa kesi nydingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imekuwa ikiingilia katika baadhi ya mambo ambayo maslahi ya Serikali yanakuwa yako hatarini na pla katika ushauri ambao tumeuweka hapa tumeshauri taasisi hizi zikiwa zina kesi kubwa ambazo zinahitaji *intervention* ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa-*consult* mapema, ili wapate ushauri ambao unaweza kusaidia kulinda maslahi ya Serikali. Katika swali aliloliuliza sasa, nitoe tu rai kwa Wanasheria wote, hasa wale Mawakili katika Taasisi za Serikali katika kila Halmashauri kuendelea kufanya kazi hizi kwa weledi mkubwa na ufanisi, ili kulinda maslahi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuwajengea uwezo Mawakili mbalimbali na pia Halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wanasheria wao, ili pindi wanapokwenda kulinda maslahi ya Serikali, basi wafanye kazi hiyo katika weledi na ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la kesi ngapi tumeshinda za usuluhishi; Mheshimiwa Mbunge aniruhusu tu nikachukue takwimu na nikishazipata nitampatia ili na ye ye aone ni kwa kiwango gani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya kazi hii ya kulinda maslahi ya nchi yetu. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, sasa aulize swali lake.

Na. 458

Faida Itokanayo na Mabaki ya Mjusi (Dinosaria)

MHE. HAMIDU H. BOBALI aliuliza:-

Kumekuwa na Maswali yaliyokosa majibu stahiki kila mara kuhusu suala la mabaki ya mjusi (*Dinosaur*) yaliyopo Ujerumani, kila linapoulizwa au kuchangiwa hapa Bungeni:-

(a) Je, ni nini kauli ya mwisho ya Serikali kuhusu faida ambayo wananchi wa Mkoa wa Lindi na Tanzania kwa ujumla watanufaika kutokana na mabaki hayo?

(b) Je, kwa nini Serikali isishauriane na Serikali ya Ujerumani kuboresha barabara na huduma za maji katika Kijiji cha Manyangara katika Kitongoji cha Namapwiya, ambapo mabaki ya mjusi huyo yalichukuliwa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali kuhusu mijusi mikubwa (*Dinosaria*) iliyochimbiliwa katika Kilima cha Tendaguru, Mkoani Lindi, nchini Tanzania katika mwaka 1909 hadi mwaka 1913 na kupelekwa katika Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Berlin, nchini Ujerumani, yamejibowi kwa miaka mingi na wakati tofauti Bungeni ambapo Serikali imekuwa ikitoa ufanuzi uliokidhi haja katika mazingira yaliyokuwepo wakati maswali hayo yanajibowi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni

Wizara yangu imefuutilia suala hili kwa umakini mkubwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kujiridhisha kama ifuatavyo:-

(a) Wazo la kuwarudisha *dinosaria* nchini halina tija kutokana na changamoto za kiteknolojia na gharama, ikilinganishwa na faida za kuchukua hatua hiyo.

(b) Tanzania iendelee kusisitiza kupata manufaa kutokana na uwepo wa *dinosaria* wake huko Berlin, Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia majadiliano bya kina yaliyohusisha pia wataalam waliobobea katika masuala ya malikale kutoka pande zote mbili, imekubalika kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ya Ujerumani itendesha shughuli za utafiti zaidi huko Tendaguru na katika maeneo jirani, ili kuwezesha uchimbuaji wa mabaki ya *dinosaurian* wengine yanayoaminika kuwepo katika maeneo hayo.

(ii) Serikali ya Ujerumani itawezesha kuanzishwa kwa kituo cha makumbusho, ili shughuli za utalii zifanyike katika eneo hilo na kuvutia watalii kutoka nchini na nje ya nchi.

(iii) Serikali ya Ujerumani itafadhili zoezi la uimarishaji idara inayohusika na malikale katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na kuwezesha upatikanaji wa watalaaam wa kutosha wa fani husika, ili kuendeleza utalii wa malikale nchini. Hivyo, uboreshaji wa barabara na miradi ya maji anaouzungumzia Mheshimiwa Mbunge utakuwa sehemu ya mafanikio ya shughuli za utalii katika eneo linalozungumziwa.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha yoyote ambayo tunaweza tukazungumza haiondoi ukweli kwamba

dinosaurian huyu ni mali yetu sisi Watanzania, kwa hiyo, manufaa yoyote yanapaswa sisi tuanze kunufaika. Sasa kwa kuwa, Serikali imesema kwamba, Serikali ya Ujerumani imeji-*commit* katika masuala matatu aliyoyasema Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi, naomba jibu kwamba, ni lini utekelezaji wa haya utafanyika, ili tuweze kujua kwa sababu, wakati anajibu amesema kwamba, majibu yalikuwa yanatolewa wakati huo kwa wakati huo. Sasa sasa hivi nataka katika hizi *commitment* tatu ambazo Serikali ya Ujerumani wamezitoa, ni lini sasa utekelezaji utafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi sasa tunapozungumza kumekuwa na *tendency* ya watalii kuwa wanakwenda, mwaka huu tumepokea watalii zaidi ya watano ama sita wamekwenda, lakini walikuwa wanapata kikwazo kikubwa cha barabara. Sasa Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, kuna haja ya kujenga barabara hata kwa dharura ya kwenda kule, ili njia ikawa inapitika wakati tunasubiri hayo makubwa ambayo Serikali ya Ujerumani imeji-*commit*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Bobali kwa kuungana na Wabunge waliotangulia kabla yake, lakini pia na mawazo ya Wabunge wengine wote humu ndani ambao wana nia njema ya kuhakikisha kwamba, rasilimali na maliasili za nchi hii zinanufaisha Taifa hili. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu swali lake kwamba, ni lini hatua hizi zinazozungumziwa zitachukuliwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua hizi ni za majadiliano ya pande mbili. Hivi ninavyozungumza Naibu Waziri wa Mambo ya Nje alikuwa asafiri wiki hii, kutohana na changamoto nyingine za Kiserikali safari hiyo imesogezwa mbele kwa wiki moja. Atakapokwenda, matokeo ya mazungumzo hayo pengine yatakuja sasa na mpango kazi na ratiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kusema sasa hivi kwa upande mmoja bila kujua sasa kwa pamoja sisi sasa, Serikali ya Tanzania na Ujerumani, ratiba yetu ya utekelezaji wa haya ambayo yanaonekana kwamba tunakubaliana inaanza lini. Wakati huo utakapofika basi, utapata jawabu kwamba lini tunaanza na tunategemea kukamilisha lini programu tunayoizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika swali lake la pili, anataka mpango wa muda mfupi, kwamba, kwa sasa hivi hatuwezi kufanya utaratibu pale, hivyo hivyo palivyo kwa sababu tu za kihistoria watu wanajua kwamba alitoka mjusi mkubwa pale wa vipimo na viwango tunavyovizungumzia watu wanataka kwenda kuona kwa mazingira hayahaya yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili nafikiri nipate nafasi sasa ya kufika kwa uhalisia kabisa kwenye eneo hilo na kuona barabara hiyo inayozungumziwa, kwanza ni barabara ya aina gani. Barabara ya Mkoa, ni barabara ya Halmashauri au ni barabara ambayo jukumu lake linatakiwa kutekelezwa na nani Serikalini. Baada ya hatua hiyo tutaweza kujipanga vizuri zaidi kutekeleza, ili hayo mambo mazuri tunayokusudia yaweze kutekelezwa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ningependa Serikali ituambie kwa muktadha wake kabisa kwa sababu haya ambayo wameelezea kuyafanya *it is a peanut!* Ni madogo sana. Kujenga kituo cha Makumbusho, kuwafadhili watu kupata fani ya malikale ni hela ndogo sana! Mjusi huyu tangu apelekwe kule ni kiasi gani, kwa maana ya faida kutokana na utalii, umeiingizia Serikali ya Ujerumani? Kwa nini Serikali ya Tanzania tusiingie angalau mkataba tuwaambie angalau asilimia tano au 10 ya mapato watuletee kutokana na mjusi ambaye anaingiza fedha za utalii kule Ujerumani kuliko hizi *peanut package* ambazo wanatupa ambazo hazisaidii nchi yetu? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshauri tu Dada yangu kwamba, masuala yanayohitaji utafiti na takwimu ni vizuri kusubiri utafiti na takwimu utoe matokeo badala ya kutoa kauli za jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda niseme tu kwa kifupi kwamba, mijusi huyu au mijusi hawa waliotoka Tanzania kule Ujerumani na bahati nzuri wako baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa wamefika pale mahali na mmojawapo ni Mheshimiwa Dkt. Kafumu ni kwamba, mijusi hawa wawili ni sehemu tu moja ya vivutio vingine vya malikale vilivyoko katika jumba la makumbusho kule Ujerumani ambalo ni kubwa na lina vitu vingi na kiasi ambacho hata kukokotoa kwamba, mijusi wawilli wa Tanzania wanazalisha nini ndani ya jumba ambalo watu wanakuja kuangalia vitu vingi ambayo Wajerumani hawa walivitoa katika nchi za Afrika walizotawala wakati huo katika maeneo mengi na wako wengi kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo matatu ambayo yanafahamika tayari ni kwamba, viingilio katika makumbusho ya Elimu Viumbe huko Berlin ni *Euro* 3.5 hadi *Euro* nane, kwa jumba zima ambalo lina vivutio vingi ambapo wanafunzi, watafiti na wazee wanaingia bure, hilo la kwanza.

Pili, asilimia 95 ya Bajeti ya Makumbusho ya Elimu Viumbe Berlin kule, inatoka katika Serikali Kuu na Serikali ya Mji wa Berlin, maana yake ni kwamba, hiyo makumbusho haina hata uwezo wa kuweza kujidoresha yenyewe.

Tatu, Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Berlin ina kumbi nydingi za maonesho, Ukumbi wa *Dinosauria* ukiwa ni mmoja tu, kwa hiyo, ni vigumu kujua kiasi halisi cha fedha kinachopatikana kutokana na kuingia na kuona masalia ya mijusi wa Tanzania. Vilevile kwenye makumbusho hii kuna nakala ya masalia ya mijusi kutoka nchi nydingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapozungumzia suala la kuboresha eneo hili ambako mijusi wametoka, ili liweze kuwa eneo la utalii si sahihi kusema kwamba, kipato kitakachotoka pale kitakuwa *peanut*. Pia, pili, ukifundisha watu kwenye taaluma hiyo ya malikale ambayo itaendelea kufanya tafiti katika nchi nzima hii, athari yake ni kubwa. Kwa hiyo, kiufupi unaweza kusema tu kwamba, watu hawa sasa badala ya kutupa samaki wanataka kutupa boti, wanataka kutufundisha kuvua, ili tuweze kuvua wenyewe samaki tupate faida zaidi kuliko kupewa samaki wa siku moja tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kwamba kwa kweli, Naibu Waziri nadhani hili swali la Mbunge wa Tarime amelinanii. Pamoja na *dinosaur* Mikoa ya Lindi na Mtwara ina utajiri mkubwa wa utamaduni ambaao unaweza kutumika kama sehemu ya utalii na kufaidisha watu wa Kusini. Je, ni lini Serikali au Wizara itaamua kuanza kuwekeza kenyé utamaduni wa Kusini ili utumike kama utalii wa watu wa Kusini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli Kusini ni sehemu ya maeneo yaliyoko nchi nzima, Tanzania nzima ambayo yana utajiri mkubwa wa kihistoria hasa Historia ya Utamaduni wa Mtanzania katika makabila yote tuliyonayo na kwamba, eneo hilo pia, ni kivutio cha kutosha kabisa chenye sifa ya kuweza kuwa maeneo ya shughuli za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudie tu kama ambavyo nimejibu swali kama hili mara nyingi nikiwa nimesimama hapa, mbele ya Bunge lako Tukufu. Ni kwamba, Halmashauri zote, ikiwemo ile ambayo Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani waharakishe kutekeleza

Agizo la Serikali la kuorodhesha maeneo yote ambayo yako kwenye maeneo yao, Halmashauri zao, ambayo yana sifa hizo tunazozizungumzia, ili tulete Wizarani yawefe kupitiwa, yachambuliwe, ili kuweza kuwekwa katika viwango na kuweza kuona namna gani mahitaji yake yakoje, ili tuweze kuendelea katika kuvitangaza na badaye kuwafutia watalii kwa ajili ya shughuli za utalii.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 459

Kumaliza Tatizo la Wahamiaji – Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua au kumaliza kabisa tatizo la baadhi ya wakazi wanaoitwa Wahamiaji katika Vijiji vya Nyabuzume, Tiring'ati, Nyaburundi na Bigegu ambao kwa miaka minge wamekuwa wakisumbuliwa na hoja hiyo bila kupewa ufumbuzi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika nchi yetu, hususan maeneo ya mipakani, imekuwa na tatizo la wahamiaji ambao hufahamika kama walowezi walioingia na kuishi nchini kwa miaka minge. Wahamiaj hawa waliingia nchini kwa sababu mbalimbali tangu wakati wa ukoloni, ikiwemo kufanya kazi katika mashamba na migodi ya wakoloni, vita vya kikabilna uhaba wa ardhi katika nchi zao na pia kuvutiwa na hali ya amani iliyopo katika nchi

yetu. Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura Namba 357, kama ilivyorejewa mwaka 2002 walowezi hawa hawatambuliwi kama raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ni mionganoni mwa maeneo yenye tatizo hili. Hivyo, kwa kutambua changamoto za tatizo hili Serikali kuititia Idara ya Uhamiaji mwaka 2009 ilifanya sensa ya wahamiaji hao katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni pamoja na vijiji tajwa ambapo, ilibaini kijiji cha Nyabuzume kuna walowezi 160, Tiring'ati 48, Nyaburundi 530 na Bigegu 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya sensa hiyo, Serikali imekuwa ikiwapatia wahamiaji hao vibali vyta kuishi nchini baada ya kukidhi vigezo ili kuwatambua na kuhalalisha ukaazi wao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Katika nchi yetu raia wengi hawana vyeti vyta kuzaaliwa. Katika Mkoa wa Mara lipo kabilia la jamii ya Waluo kwa maana ya Wajaluo. Kwa kuwa wao ni wengi, wengi wao wanaishi Kenya na inaonekana kwamba, zipo hisia tu kila Mjaluo anayeonekana Tanzania hapa anakuwa kama mhamiaji. Ni lini sasa hawa Wajaluo ambaa ni raia wa Tanzania wanaishi mpakani na hasa kwenye vijiji nilivyovitaja, ni lini watapewa haki yao ya msingi kama raia kuliko kusumbuliwa kila siku kuonekana kama wahamiaji wakati wao ni wa karibu hapa wanaishi maeneo ya Rarya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hivi mtu akiwa mlowezi, ni lini ulowezi wake unakoma? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana babu yangu, Mheshimiwa Getere, kwa maswali mawili mazuri sana. Moja, hili alilosema la Wajaluo, si Wajaluo tu watu amba wana makabila yanayoingiliana na nchi za jirani kupata misukosuko ya aina hiyo, yapo matatizo haya Mikoa yote ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimwambie tu kuhusu lini hilo litakwisha ni kwamba, Serikali kuitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kuitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa wako katika hatua za mwisho za kufanya utambuzi na badaye kuwapatia vitambulisho wananchi wote wa Tanzania. Kwa hiyo, pale watakapokuwa wameshapata vitambulisho hapatakuwepo na mtu tena kuhisiwa hisiwa kwa ajili ya makabila kuwa yana mwingiliano katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu walowezi na lenyewe liko karibu sana na hili nililolisema. Kuna taratibu za walowezi, watu walilowea hapa kupewa uraia wao. Kwa hiyo, kwa wale amba watakidhi vigezo na wakapewa uraia watapewa vitambulisho na hilo litakuwa limekoma la kuwa walowezi na watakuwa Raia wa Tanzania. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Chacha, swal fupi tafadhali la nyongeza, muda wetu umekwenda sana.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, swal i la Bunda la Mheshimiwa Getere, halina tofauti sana katika Jimbo langu la Serengeti katika Vijiji vya Rwamchanga, Masinki, *Ring One* na maeneo mengine, ambapo kuna jamii ya Wakisii, Wanandi, amba wamekuwepo kabla ya uhuru. Je, ni lini Serikali itawafanya kuwa raia wa Tanzania? Maana tumeona maeneo mengine wakimbizi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge Waziri ameshasikia swal iako. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Naibu Spika, nimjibu babu yangu Mbunge wa Serengeti kwamba, kwa wale wote ambao wameshakaa tangu enzi ya uhuru na wako Tanzania na wangependa kuwa raia wa Tanzania, pana taratibu. Wafike kwenye Ofisi za Uhamiaji watapewa taratibu za kuhalalisha uraia wao kwa sababu, uraia hatuwapi tu kwa kutamka, lazima wapite kwenye taratibu zile ili kuweza kuweka kumbukumbu sawa kwamba, wameshakuwa raia.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Salome Wyycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Na. 460

**Wananchi wa Kata ya Muhunguala Kukosa
Huduma za Jamii**

MHE. WILFRED M. LWAKATARE (K.n.y. MHE. SALOME W. MAKAMBA) aliuliza:-

Zaidi ya Kaya 800 za wananchi wa Mitaa ya Bukondamoyo na Muhunguala katika Kata ya Muhunguala, Jimbo la Kahama Mjini wamezuiliwa kupatiwa huduma muhimu za kijamii kwa madai kwamba wanaishi kando ya Bwawa la Niyhogo, ilihali wananchi hao wanaishi umbali wa zaidi ya mita 700 kutoka katika bwawa hilo:-

Je, ni kwa nini Serikali inawanyima wananchi hao huduma za kijamii wakati wako umbali wa mita 60 zilizowekwa kisheria?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Nyihongo ndiyo chanzo pekee mbadala cha maji katika Mji wa Kahama, ambapo bwawa hilo lilisanifiwa mwaka 1948, lenye eneo la zaidi ya ekari 145. Mipaka ya bwawa hilo ilitangazwa katika Gazeti la Serikali, Namba 72, mwaka 1963.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wamevamia kwenye hifadhi ya eneo tengefu la bwawa hilo, hasa katika sehemu za kidakio cha maji na wengine wapo kwenye eneo hatarishi, linalopitisha maji baada ya bwawa kujaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Maji Kahama kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya ya Kahama na Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa ujumla umetoa ilani ya kusitisha shughuli zote za kibinadamu kufanyika ndani ya hifadhi ya bwawa na kidakio cha maji. Kutokana na hilo Serikali inaandaa mpango wa kuwaondoa wananchi hao katika maeneo hayo na kuendelea kuzuia shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa kaya zote ambazo ziko nje ya mpaka wa hifadhi ya bwawa kwa kuwapatia huduma ya maji safi na inawashauri wananchi ambao wapo ndani ya hifadhi ya bwawa hilo kuhama ili kulinda chanzo hicho kwa manufaa yao wenyewe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare, swali la nyongeza.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ningombaa niulize maswali mawili ya nyongeza mafupi. Kwa kuwa, Serikali inatambua kuwa eneo hilo ambalo limetajwa kama vyanzo vyaa maji kwamba halipashwi kupewa huduma zozote na inawataka wananchi kuhama. Serikali inasemaje kuhusu huduma nyingine ikiwamo ya kuwepo viongozi ambao wamechanguliwa kwa kura na kura zinaendelea kufanyika pale eneo hilo na viongozi waliochaguliwa wengine ni wa CCM ambao wanaongoza

eneo hili, Serikali inasemaje hiyo huduma ya kiuongozi nayo hawaitambui. Kwa hiyo, waondokeje wakati kuna uongozi uliochaguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Sheria namna ilivyo kwa hali halisi inajichanganya sana kutokana na tafsiri ya chanzo cha maji cha mita 60, lakini Serikali imewahi kujibu hapa kutokana na hali halisi kwamba kuna maeneo ambayo kijiografia leo hii ukiwaondoa watu kwa mita hizo 60 wakiwemo wananchi wa maeneo mbalimbali ya Bukoba Town ni kwamba Mji wa Bukoba Town hautakuwepo kwa sababu kila mita 60 kuna mto kuna chanzo cha maji. Serikali inasemaje katika kuleta kanuni ambazo ilisema itazileta ambazo zinaweka tafsiri pana na inayofafanua hizi mita 60 zina maana gani? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kiuongozi katika eneo tengefu, niseme watoke. Watoke na wala huduma ya kiuongozi huko haitakuwepo, wala huduma ya aina yoyote watoke, wakisubiri wataondolewa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kuhusu mita 60, namshukuru sana Mheshimiwa Lwakatare, *definition* ya mita 60 inalenga maeneo fulani fulani. Sasa hivi tumeanza kuzungumzia suala hili ukiangalia katika mito kuna mito kuna vijito na kuna *vi-stream* vingine ni vidogo sana ambavyo pengine mvua ikinyesha kinawenza kikatirisha maji kwa wiki moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi tuwe na *definition* pana, mita 60 inalenga wapi, ni kwa kila kamto hata mto kama Rufiji kwenye mito ambayo ni mikubwa ina mabonde makubwa *definition* ya mita 60 haipo na ndiyo maana kwenye bwawa la Nyihongo mipaka yake imekuwa ni mikubwa zaidi kuliko hiyo mita 60. Tunalenga pia lile eneo ambalo ni oevu ambalo ndiyo linafanya sasa lile bwawa

liweze kuishi. Kwa hiyo, hii tutaiweka vizuri ili kuondoa mkanganyiko kama uliotaka kujitokeza hapa wa vinyungu.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho Mheshimiwa Injinia Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Muhamwe, sasa aulize swali lake.

Na. 461

Mradi wa Maji katika Mji wa Kibondo

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE aliuza:-

Kwa muda mrefu sasa Mji wa Kibondo hauna maji baada ya chanzo cha maji kuharibiwa na shughuli za kibinadamu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mradi mwagine wa maji toka chanzo kingine (hasa Mto Malagarasi) ili Kata za Busunzu, Busagara, Lusohoko, Kitahana, Kumwambu, Kibondo Mjini na Miserezo zipate maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba la Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Jimbo la Muhamwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo Sekta ya Maji awamu ya pili, Serikali imepanga kuboresha huduma ya Maji safi katika Mji wa Kibondo kwa kufanya usanifu wa kina na uandaaji wa vitabu vyat zabuni ili kupata gharama ya ujenzi wa mradi mkubwa ambao utapita katika Kata saba zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwa kutumia chanzo cha Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa

makabrasha ya zabuni unaotarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2017. Vilevile taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinaendelea na anatarajiwa kupatikana mwezi Julai, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa Mji wa Kibondo. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 21017/2018. Kazi zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na upanuzi wa mtandao umbali wa kilomita saba na ukarabati wa bomba la maji urefu wa kilomita nne, ununuzi dira 850 na ufungaji wa pampu na mota.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Wilayani Kibondo wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetengea kiasi cha shilingi milioni 826.8 Halmashauri hiyo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya vijijini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Injinia Atashasta Nditiye, swali la nyongeza.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mepesi mepesi ya ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, inaonyesha jinsi ambavyo mtiririko wa *project management engineering pattern* usivyokuwepo katika majibu yake ya swali ya msingi. Haiwezekani leo Serikali inapanga kuchukua kufanya usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni halafu wakati huo huo mtaalam mshauri anaendelea na usanifu ambao unatakiwa kwisha mwezi Julai, 2017, wakati mtu wa *Environmental Impact Assessment* hajafanya kazi yake. Hilo inanipa mashaka kama kweli huu mradi upo au haupo. Sasa naomba Serikali itoe tamko kama kweli huu mradi upo na utaanza lini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, amezungumzia kiasi cha shilingi milioni 300 zilizotolewa kwa ajili ya Mji wa Kibondo kupanua miundombinu. Hata hivyo, ninayo uhakika na yeze Mheshimiwa Naibu Waziri niliwasiliana naye mwezi wa Aprili mwanzoni, kwamba kuna milioni 300 zilizotolewa kwa ajili ya Mji wa Kibondo toka mwaka jana bajeti iliopita hii tunayoimalizia, lakini ziliendelea kuchezewa chezewa pale Mkoani mpaka sasa hivi tunavyoongea pesa haijaenda Kibondo. Lakini tunaambiwa tuna milioni 300 zina...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nditiye naomba uulize swali lako la pili ambalo linaweza likawa ni la tatu sasa maana umesauliza mawili tayari.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka njue hilo milioni 300 anayozungumza kwamba itatolewa mwaka huu ni ile tuliyodhulumiwa Kibondo mwaka jana au inakuwa *carried forward* au ni ya mwaka huu? Naomba kujibiwa. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa amesema majibu ni mapesi, mtiririko wa mipango hauonekani vizuri ni kweli. Moja, tunataka kwanza tuwe na chanzo na chanzo ni Malagalarasi. Usanifu unaofanyika ni wa kutoa maji mto Malagalarasi kuleta Kaliua, Urambo na Tabora. Chanzo hicho hicho kikishakamilika ndiyo kitachukua maji kupeleka katika Jimbo lake ndiyo maana kidogo inamchanganya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba mradi upo tukishakuwa na chanzo cha maji tayari kitakachobaki ni kuweka fedha kufanya utafiti mdogo wa kuyatoa maji kwenye chanzo ambacho kipo na kuendelea kukipeleka katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na shilingi milioni 300, ni kweli, tulishaliongea hili nje na Mheshimiwa Mbunge, nikajaribu kufuatilia nikakosa majibu na juzi nilikuwa Kigoma. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba sasa tutaunda Tume ndogo ili kuweza kuangalia kuhusu hizi shilingi milioni 300, moja je, ni kweli zilitolewa, na kama zilitolewa ziko wapi? Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge hapa hakiliwi kitu, kama kuna mtu atakuwa amefanya fujo, taratibu na Sheria za Kiserikali zipo atashughulikiwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha nitaruhusu swali moja tu, Mheshimiwa Issa Mangungu.

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ningombwa Naibu Waziri nami anithibitishie je, ni lini Serikali italeta maji au mtandao wa *DAWASA* utafika katika Kata za Kiburugwa, Kilungule na Chamazi kwa sababu tangu nchi hii kupata uhuru eneo hilo halijawahi kupata maji na wala hakuna mpango wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, visiwa vya Kimbiji vinakamilika lini? Maana yake...

NAIBU SPIKA: Ameshalisikia swali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwangiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilishatamka katika Mbunge hili kwamba vyanzo tumekamilisha, visima vya Mpera pia vimekamilika, Ruvu Chini imekamilika, Ruvu Juu imekamilika. Kilichobaki sasa hivi tayari tunaendelea sasa na mikataba ya kutengeneza usambazaji wa hayo maji kuyapeleka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo napenda, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sasa hivi tuna mkataba mmoja, tumeshapata fedha kutoka Benki ya Dunia dola milioni 50, tunajipanga kuhakikisha maeneo yote ya Dar- es -

Salaam yanapata huduma ya maji kwenye vijiji, vitongoji na mitaa yote. Kwa hiyo asiwe na wasiwasi maji yatapatikana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, nitawaleta matangazo tuliyonayo siku ya leo kabla ya kuendelea na shughuli zetu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza linahusu wageni, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge lakini pia wapo wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo.

Kundi la kwanza ni wageni 14 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, kutoka *Voice of Sober House* Tanzania. Karibuni sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wamekuja kwa ajili ya Maadhimisho ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevyia Duniani ambayo yatafanyika Kitaifa hapa Mkoani Dodoma, siku ya tarehe 29 Juni, 2017 katika viwanja vya Nyerere Square kesho. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni Tuwasikilize na Kuwashauri Vijana na watoto ili Kuwaepusha na Dawa za Kulevyia. Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Jenista anachukua nafasi hii kuwakaribisha Wabunge wote kuanzia saa saba mchana kesho kuhudhuria katika maadhimisho hayo ili kuweza kuungana na nchi zote duniani kupiga vita dawa za kulevyia. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa James Ole Millya ambaao ni Viongozi wa Kimila kutoka Jimboni kwake Simanjiro Mkoani Arusha. Hawa wanaongozwa na Alaigwanani Ole Ngarada. Karibuni sana viongozi wetu. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni Wanafunzi 111 na Walimu 15 kutoka Shule ya Sekondari Ihumwa ambayo iko Mkoani Dodoma. Karibuni sana watoto wetu lakini pia Walimu wetu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 80 kutoka Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Herbert Kairuki cha Jijini Dar es Salaam, karibu ni sana Madaktari wetu na Manesi sijui kama wapo lakini karibuni sana. Naamini mtapata fursa ya kuona namna tunavyofanya kazi Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, anawatangazia kwamba utoaji huduma ya afya katika Zahanati ya Bunge kwa sasa itawakuwa ni saa mbili asubuhi mpaka saa mbili usiku kwa siku za Jumatatu mpaka Ijumaa na kwa siku za Jumamosi na Sikukuu za Serikali kituo kitatoa huduma kuanzia saa mbili hadi saa nane mchana.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnapotitaji huduma mzingatie muda huu na muda ambao huduma hii itakuwa haitolewi katika zahanati hii ya Bunge basi Waheshimiwa Wabunge tunaweza kwenda kwenye hospitali ya Mkoa lakini Madaktari wetu unaweza ukawapa taarifa ili wawze kuweka utaratibu mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linalotoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu anawatangazia kuhusu eneo la huduma ya watoto. Waheshimiwa Wabunge wenye watoto wadogo mnaarifiwa kuwa Ofisi ya Bunge imetenga chumba maalum kwa ajili ya kunyonyeshea watoto.

Chumba hicho kipo kwenye jengo la Msekwa jirani na chumba cha Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi na Usalama wa Bunge, kwa hivyo mnaombwa kutumia chumba hicho kilichotengwa mahsus kwa ajili ya huduma ya kunyonyeshea watoto wadogo ili watoto hawa wawze kupata huduma

ili na ninyi mkiendelea na kazi. Kama tunavyojuua Wizara ya Afya imeshatutangazia kwamba watoto wadogo wanapaswa kunyonya angalau kwa miaka miwili. Kwa hiyo, tujitahidi kunyonyesha watoto na Bunge letu kwa kutambua hilo limeweka utaratibu huo mzuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo anawatangazia kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira, kuanzia saa saba mchana, katika Ukumbi wa Msekwa C. Kwa hiyo Wajumbe wa Kamati hii mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sport Club*, Mheshimiwa William Ngeleja na yeze anawatangazia Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mchezo uliochezwa siku ya Jumamosi tarehe 24 Juni, 2017, kwamba *Bunge Sports Club* ilipata magoli mawili na *Kigamboni Olds Club* ilipata goli moja.

Magoli ya timu ya Bunge yalifungwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Omary Mgumba ambaye ni *Captain Msaidizi*. Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Esther Matiko ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*. (*Makofii*)

Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anatoa pongezi za kipekee kwa Kocha Mkuu Mheshimiwa Venance Mwamoto pamoja na Msaidizi wake Mheshimiwa Ahmed Ngwali kwa namna wanavyoendelea kukisuka kikosi cha Bunge *Sports Club*. (*Makofii*)

Tanganzo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Joseph Selasini ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore ya Bunge, anawatangazia kwamba leo Jumatano tarehe 28 Juni, 2017, kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo wa madhehebu ya Kikatoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa

ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kushiriki ibara hiyo wanakaribishwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mwende kusali muda huo, tukishaahirisha Bunge basi mwelekee katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), nitaisoma pamoja na Kanuni ya 47(1) ikikupendeza sikusudii Bunge lijadili lakini ninachokusudia tupate kauli ya Serikali. Mwezi Mei 2017, Serikali ilitangaza kwamba kutakuwa na utoaji wa *sulphur* bure kwa wakulima wote wa korosho na wananchi wakawa wametegemea. Kwa utaratibu unaotumika wakulima wa korosho huwa wanajewekea fedha ikifika wakati wananunua *sulphur* kutoka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kutangazwa tangazo lile wakulima waliamua sasa kutumia fedha kwenye matumizi mengine, wengine kusomeshea watoto na matumizi mengine ambayo ni ya kawaida. Kilichotokea *sulphur* iliyotolewa haikidhi haja hata theluthi hata robo haifiki. Mtu mwenye mahitaji ya *sulphur* mifuko ishirini wamepewa mfuko mmoja ama wengine wamepewa mfuko mmoja wagawane wakulima wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo pia lilipelekeea pia wafanyabiashara wakubwa wa *sulphur* wasiagize *sulphur* kuleta nchini kwa sababu wanajua Serikali ita-supply *sulphur* bure. Mfuko uliokuwa unauzwa Sh.20,000/=, leo unauzwa kati ya Sh.35,000/= mpaka Sh.45,000/= na maeneo mengine Sh. 50,000/= jambo ambalo wakulima hawawezi ku-afford.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, Serikali haioni haja kwamba sasa wawaeleze hawa matajiri *wa-supply sulphur* kwa wingi ili wakulima waweze kupata *sulphur*? Ama kama ina mkakati mwingine basi hiyo *sulphur* waliyosema watatoa bure waipeleke kwa wingi kwenye maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa hivi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kiti kifanye maamuzi ili ikikupendeze tuweze kujadili ama basi Serikali itoe kauli ndani ya Bunge leo, kwa sababu jambo hili linawaumiza sana wakulima na kiukweli ni jambo *very sensitive* kwa sababu zao la korosho ndio zao liliopatia Serikali fedha nyingi kuliko zao lolote kwa sasa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

MHE. ENG. ATASHATA J. NDITIYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa kanuni ya 46(1) kuhusu swali la kwanza la nyongeza nilouliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alikubaliana na mimi kwamba mtiririko wa *Project management Engineering pattern* haukuatuwa na akanipa maelezo kwamba nimeona hivyo kwa sababu wao walifanya *feasibility study* iliyolenga kupata chanzo cha maji kutoka Mto Malagarasi kupeleka Kaliua. Swali langu nataka mwongozo wako kwa sababu niliyeuliza swali ni mimi kuhusu Kibondo na nikataka njue sasa hayo maji kweli yapo au hayapo? Akanijibu yapo lakini hakujibu ni lini sasa huo mradi utaanza kwa Kibondo wakati sasa kumbe hata *feasibility study* inafanyika kwa ajili ya Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo miwili. Kwanza na Mheshimiwa Bobali na pia Mheshimiwa Atashasta Nditiye.

Kwanza nianze na maelezo ambayo kama nilivyokuwa nimeahidi kwamba sitachoka kuyasema

nitayarudia tena. Hizi kanuni Waheshimiwa Wabunge zinatoa fursa ya Mbunge kupata nafasi ya kuzungumza Bungeni juu ya jambo, kismingi, lolote analoona yeye linawahu su watu wake na lina maslahi kwa watu wake. Isipokuwa kanuni hizi zimeweka utaratibu wa kufanya jambo hilo.

Sasa nirudie tena leo, si kila jambo linaweza kuombewa mwongozo. Yapo mambo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaweza akayaleta Bungeni kuitia kauli yake yeye kama Mbunge. Hasa kwa jambo hili aliloliomba Mheshimiwa Bobali angeweza kutumia kanuni nyininge ambazo kama anazihitaji mimi naweza kumpa, sina haja ya kutoa maelezo marefu, ili jambo lake hilo liweze kusikika na Serikali halafu Serikali iweze kutoa kauli. Lakini ukiomba kwenye mwongozo hiyo nafasi haipo ya Serikali kutoa kauli.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Bobali kama utahitaji msaada wa hizo kanuni ili uilete kauli yako binafsi na kanuni zinakuruhusu. Kwa hiyo, kwa kuwa kanuni zinakuruhusu uombe hiyo fursa ya kulete maelezo yako mahsusili Serikali iweze kutoa hayo maelezo. Na mimi uliomba kwamba mwongozo wangu niiombe Serikali iwaagize wafanyabiashara walete *sulphur* kwa wingi na mambo meningi na ukasema pia niagize Serikali itoe kauli.

Sasa tutumie kanuni zinazohusika ili Serikali iweze kutoa kauli yake, kwa sababu pia kauli ya Serikali iko pia kikanuni. Kwa hivyo, sitaenda kwenye hizo kanuni lakini niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kanuni ya mwongozo inahusu mambo yaliyotokea Bungeni mapema.

Kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Atashasta Nditiye, ameitaja kanuni ya 46(1) inayohusu kujibu maswali kikamilifu. Maelezo yake yanasema kwamba swalii lake la nyongeza la kwanza halikujibiwa kikamilifu kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu ameonyesha kana kwamba huo mradi aliokuwa anauzungumzia ni wa Kaliua wakati Mheshimiwa Nditiye aliuliza kuhusu Kibondo.

Sasa ili niweze kuwa na uhakika wa swali liliulizwa
vipi na majibu yalijibiwa vipi; mwongozo huu ulioombwa
na Mheshimiwa Atashasta Nditiye ntautoa hapo baadaye
baada ya kupitia Taarifa Rasmii za Bunge.

Baada ya kusema hayo tutaendelea, Katibu!

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka
ya Bunge kuhusu Shauri la Kudharau Mamlaka
ya Spika linalomhusu Mheshimiwa
Joshua Samwel Nassari (Mb)**

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI
WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**
Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili
na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la kudharau Mamlaka
ya Spika linalomuhusu Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mamlaka uliyonayo
kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na nyongeza ya Nane ya
Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba
kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya kamati
yangu kuhusu shauri la Mheshimiwa Joshua Nassari la
kudharau Mamlaka ya Spika kinyume cha taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za
Bunge, katika Kikao cha Thelathini na Mbili kilichofanyika
tarehe 30 Mei ulimtaja Mheshimiwa Joshua Nassari kwamba
amedharau Mamlaka ya Spika na uliagiza afike mbele ya
Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma za
kudharau Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chanzo cha Shauri. Mnamo
siku ya terehe 30 Mei katika Mkutano wa Tatoo, Kikao cha
Thelathini na mbili wakati wa asubuhi, Bunge lilikuwa likijadili
hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa

mwaka wa fedha 2016/2017. Katika kikao hicho, Mheshimiwa Juma Nkamia aliomba Mwongozo wa Spika kupitia Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Januari akitaka kujua ni kwa nini Serikali imewafukuza wanafunzi wa Diploma Maalum ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Nkamia alieleza kuwa wanafunzi waliofukuzwa hawakuwa na kosa lolote isipokuwa Serikali ndiyo iliyokuwa na mgogoro na *management* ya Chuo Kikuu cha Dodoma, hivyo alitaka kujua ni kwa nini wanafunzi waadhibiwe kwa makosa ya watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa mwongozo wake kwa kueleza pamoja mambo mengine kuwa Mwongozo wa Spika unapaswa kuombwa kwa mambo yaliyotokea Bungeni mapema na si mambo yanayotokea nje ya Bunge. Hata hivyo, alitaka Serikali kuangalia namna bora ya kulishughulikia suala hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mheshimiwa Naibu Spika kutoa majibu ya mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Nkamia, Mheshimiwa Joshua Nassari alisimama na kutumia Kanuni ya 69 na kuomba Mwongozo wa Spika kwamba Bunge liahirisha kujadili hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji ili kujadili tatizo la wanafunzi waliofukuzwa Chuo Kikuu cha Dodoma. Alieleza zaidi kuwa wanafunzi hao ni vijana wadogo ambao walikuwa wanapata shida hapa Dodoma baada ya kufukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa mwongozo kuwa hakuona kama ni utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kuahirisha shughuli ya Bunge kwa jambo hilo lililokuwa linashughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Mwongozo huo wa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge hawakuridhika na hivyo waliendelea kuomba miongozo huku wakipiga kelele, jambo

ambalo lilituruga shughuli za Bunge zilizokuwa zinaendelea. Mheshimiwa Naibu Spika alilazimika kuahirisha shughuli za Bunge na alitisha kikao cha Kamati ya Uongozi ili kujadili suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kikao cha jioni kiliporejea, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa maelezo kuwa baada ya kutafakari vurugu zilizotokea asubuhi, Kamati ya Uongozi iliamua Waziri wa Elimu atoe Kauli ya Serikali kuhusiana na suala la mgogoro wa management ya Chuo Kikuu cha Dodoma na walimu pamoja na hatima ya wanafunzi waliofukuzwa. Hata hivyo, Profesa Ndalichako hakuwepo Bungeni wakati huo hivyo alimwita Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhitimisha hoja ya bajeti ya wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua hiyo, baadhi ya Wabunge walismama na kuanza kuomba miongozo, kupiga kelele, kugonga meza, kurusha vitabu na kukataa kutii maelekezo ya Naibu Spika yaliyowataka kutulia ili kumruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kuhitimisha hoja yake. Vitendo hivyo vilivuruga shughuli za Bunge kwa muda, jambo liliatosababisha Mheshimiwa Naibu Spika, kuwataja kwa majina Wabunge waliofanya vitendo vyta kudharau Mamlaka ya Spika na kuagiza wafike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Miogoni mwa Wabunge walijotajwa kudharau mamlaka hayo alikuwa ni Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchunguzi wa Kamati. Katika Waraka wako kwa Kamati wa kutaka kufanya uchunguzi kwa Wabunge walijotajwa kufanya vitendo vyta kudharau Mamlaka ya Spika, ulielekeza kama ifuatavyo:-

“...kwa mamlaka niliyopewa chini ya Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaiagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ichunguze na kutoa mapendekezo kuhusu suala hili”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilianza uchunguzi kwa kuandaa Hati ya wito (*summons*) kwa ajili ya kumpa Mheshimiwa Joshua Nassari (Mb) afike mbele ya Kamati. Jitihada za kumtafuta Mheshimiwa Joshua Nassari zilifanyika lakini Mhe. Joshua Nassari (Mb) aliitarifu Kamati kwa njia ya barua pepe kuwa hataweza kufika kwa kuwa alikuwa anafanya mtihani wa shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 16(2) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, mnamo tarehe 2 Juni, 2017 Kamati ilitumia Jeshi la Polisi kufikishia Hati ya Wito iliyomtaka afike mbele ya Kamati tarehe 8 Juni 2017. Hata hivyo, Mheshimiwa Nassari aliomba udhuru kuwa alikuwa anakutana na msimamizi wa mitihani yake (*dissertation*) na kuahidi kufika siku ya Alhamisi tarehe 15 Juni, na Kamati illridhia ombi lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Alhamis tarehe 15 Juni, 2017 Mheshimiwa Joshua Nassari alifika mbele ya Kamati ili kujibu tuhuma dhidi yake kama ifuatavyo:-

- (a) Kuvuruga shughuli za Bunge kwa kupiga kelele na kupiga makofi kwa vurugu jambo ambalo lilimfanya Naibu Waziri wa Maji ashindwe kuendelea na shughuli.
- (b) Kukaidi maelekezo ya Naibu Spika aliyemtaka atulie ili kumruhusu Naibu Waziri wa Maji kuhitimisha shughuli yake.
- (c) Kuendelea kusimama na kupiga kelele wakati Naibu Spika akimtaka utulie.
- (d) Kusambaza karatasi na vitabu hovyo kwa makusudi kitendo ambacho ni dharau kwa Bunge na kudharau Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja za Msingi. Ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo, ilijielekeza kwenye hoja za uchunguzi zifuatazo:-

(a) Kama ni kweli Mheshimiwa Joshua Nassari alifanya vitendo vya utovu wa nidhamu na dharau kwa Mamlaka ya Spika,

(b) Kama itathibitika alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa dhidi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano na Shahidi. Kama ilivyoelezwa awali, siku ya tarehe 15 Juni Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari alifika mbele ya Kamati kama alivyoahidi. Mheshimiwa Joshua Nassari aliposomewa tuhuma dhidi yake alikiri wazi kuwa alitenda matendo yaliyolalamikiwa na Bunge na akaliomba radhi Bunge. Kwa maneno yake mwenyewe, alisema yafuatayo, nanukuu:-.

“...Sitaki kupoteza muda wa Kamati, niombe radhi kwa lolote lillotokea na kukwaza kitu cha Spika, dhamira yangu si kuja Dodoma ili kuletwa kwenye Kamati ya Maadili bali kuwatumikia wananchi na taifa kwa ujumla. Nakiri kosa na naombwa radhi kwa Spika na kwa Bunge”

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati. Kupitia mkanda wa video wa tukio la siku hiyo, Mheshimiwa Joshua Nassari anaonekana akipiga makofi bila utaratibu, akikaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa mezani iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuangalia mkanda wa video, Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari alikiri mbele ya Kamati na kuomba radhi Bunge kwa vitendo vya utovu wa nidhamu vinavyoonesha dharau kwa Bunge na kwa Mamlaka ya Spika, shughuli za Bunge, au mtu anayeongoza Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushahidi huo, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa ni kweli Mheshimiwa Joshua Nassari alifanya vitendo ambavyo ni kudharau Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26(c) (d) (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura

ya 296 pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mantiki hiyo, Kamati inamtia hatiani Mheshimiwa Joshua Nassari kwa Kudharau Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujiridhisha kuwa Mheshimiwa Joshua Nassari alikiuka Sheria na Kanuni za Bunge, Kamati sasa inajielekeza katika hoja kwamba Kama itathibitika ni kweli alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani anatakiwa kuchukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja hiyo kamati ilizingatia yafuatayo:-

(a) Katika shauri hili Mheshimiwa Joshua Nassari alituhumiwa pamoja na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ambaye mnamo tarehe 2 Aprili, 2017 Bunge hili liliazimia kumsamehe kwa kumpa karipio kali baada ya kukiri na kuliomba radhi Bunge na Kamati.

(b) Mheshimiwa Joshua Nassari alikiri na kuliomba radhi Bunge bila kuisumbua Kamati.

(c) Hili ni kosa lake la kwanza kwa Mheshimiwa Joshua Nassari kudharau Mamlaka ya Spika.

(d) Kitendo alichokifanya kilivuruga shughuli za Bunge na kimeshusha hadhi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Sipka, Kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge kinaelekeza kuwa Mbunge ye yeyote atakayefanya kosa la kudharau Mamlaka ya Spika au shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kifungu cha 26 au Kifungu kinginecho, Bunge linaweza kuazimia kumuelekeza Spika kumpa karipio kali (*reprimand*) au kumsimamisha asihudhurie vikao vya Bunge kwa muda litakaloona unafaa, isipokuwa muda huo usizidi siku ya mwisho ya Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya azimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kanuni ya 74 inaeleza kuwa Bunge linaweza kuzingatia ushauri wowote utakaotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sheria, mashauri ya nyuma pamoja na kitendo cha Mheshimiwa Nassari kukiri na kuomba radhi, hivyo Bunge litafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuizingatia wakati wa kupitisha azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilolitenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Napenda kukushukuru wewe na uongozi mzima wa Bunge, nawashukuru na waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati na watendaji ambao wamehudumia kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa shauri hilli naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA
BUNGE KUHSU SHAURI LA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA
LINALOMIHUSU MHESHIMIWA JOSHUA SAMWEL NASSARI
(MB) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mhe. Joshua Nassari (Mb) la kudharau Mamlaka ya Spika, kinyume na kifungu cha 26 (c) (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*]; na kinyume na Kanuni ya 74 (1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa Mamlaka yako kwa mujibu wa Kanuni ya 74(1) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha

Thelathini na Mbili kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 ulimtaja Mhe. Joshua Nassari (Mb) kwamba amedharau Mamlaka ya Spika, na uliagiza afike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kujibu tuhuma za kudharau Mamlaka ya Spika.

2.0 CHANZO CHA SHAURI DHIDI YA MHE. JOSHUA SAMWELI NASSARI (MB)

2.1 **Mheshimiwa Spika**, mnamo Siku ya tarehe 30 Mei, 2016 katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Mbili, wakati wa asubuhi Bunge lilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017. Katika kikao hicho Mhe. Juma Nkamia (Mb) aliomba Mwongozo wa Spika kuitia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 akitaka kujua ni kwa nini Serikali imewafukuza wanafunzi wa Diploma Maalum ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mhe. Juma Nkamia (Mb) alieleza kuwa wanafunzi waliofukuzwa hawakuwa na kosa lolote, isipokuwa Serikali ndiyo iliyokuwa na mgogoro na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma, hivyo alitaka kujua ni kwa nini wanafunzi waadhibiwe kwa makosa ya watu wengine?

2.2 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa Mwongozo wake kwa kueleza pamoja na mambo mengine kuwa, Mwongozo wa Spika unapaswa kuombwa kwa mambo yaliyotokea Bungeni mapema na sio mambo yanayotokea nje ya Bunge. Hata hivyo, alitaka Serikali kuangalia namna bora ya kushughulikia suala husika.

2.3 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Mheshimiwa Naibu Spika kutoa majibu ya Mwongozo ulioombwa na Mhe. Nkamia (Mb), Mheshimiwa Joshua Nassari (Mb) alisimama kwa kutumia Kanuni ya 69 na kuomba Mwongozo wa Spika kwamba Bunge liahirishe kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na badala yake lijadili suala la waliokuwa wanafunzi wa Diploma Maalumu ya Sayansi, Chuo Kikuu cha Dodoma ambao walifukuzwa ndani ya saa 48. Alieleza zaidi kuwa, wanafunzi hao ni vijana wadogo

ambao walikuwa wanapata shida hapa Dodoma baada ya kufukuzwa.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa Mwongozo kuwa hakuona kama ni utaratibu bora wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kuahirisha shughuli za Bunge kwa kuwa jambo hilo lilikuwa linashughulikiwa na Serikali.

2.5 **Mheshimiwa Spika**, kufuatia Mwongozo huo wa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge hawakuridhika na hivyo waliendelea kuomba miongozo huku wakipiga kelele, jambo ambalo liliurvuga shughuli za Bunge zilizokuwa zinaendelea. Mhe. Naibu Spika alilazimika kuahirisha shughuli za Bunge na aliiitisha kikao cha Kamati ya Uongozi ili kujadili suala hilo.

2.6 **Mheshimiwa Spika**, mara kikao cha jioni kiliporejea, Mheshimiwa Naibu Spika alitoa maelezo kuwa, baada ya kutafakari vurugu zilizotokea asubuhi, Kamati ya Uongozi iliamua kuwa, Waziri wa Elimu Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) atoe Kauli ya Serikali kuhusiana na suala la mgogoro wa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma na walimu, pamoja na hatma ya wanafunzi waliofukuzwa. Hata hivyo, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) hakuwepo Bungeni wakati huo, hivyo alimwita Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliji kuhitimisha hoja ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

2.7 **Mheshimiwa Spika**, kufuatia hatua hiyo, baadhi ya Wabunge walismama na kuanza kuomba miongozo, kupiga kelele, kugonga meza, kurusha vitabu na kukataa kutii maelekezo ya Naibu Spika yaliyowataka kutulia ili kumruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri kuhitimisha hoja yake. Vitendo hivyo vilivuruga shughuli za Bunge kwa muda, jambo liliosababisha Mheshimiwa Naibu Spika kuwataja kwa majina Wabunge waliofanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na kuagiza wafike mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Miiongoni mwa wabunge waliotajwa kudharau Mamlaka ya Spika ni **Mhe. Joshua Samwel Nassari, (Mb)**.

3.0 UCHUNGUZI WA KAMATI

3.1 Mheshimiwa Spika, katika Waraka wako kwa Kamati wa kutaka kufanya uchunguzi kwa Wabunge waliotajwa kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika, ulielekeza kama ifuatavyo:-

"...kwa mamlaka nillyopewa chini ya Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Toleo la Januari, 2016, naiagiza Kamati ya Haki,Maadili na Madaraka ya Bunge ichunguze na kutoa mapendekezo kuhusu suala hili".

3.2 Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza uchunguzi kwa kuandaa Hati ya wito (*summons*) kwa ajili ya kumpa Mhe. Joshua Nassari (Mb) afike mbele ya Kamati. Jitihada za kumtafuta Mhe. Joshua Nassari zilifanyika lakini Mhe. Joshua Nassari (Mb) aliitarifu Kamati kwa njia ya barua pepe kuwa hataweza kufika kwa kuwa alikuwa anafanya mtihani wa shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Kwa mujibu wa Kifungu cha 16(2) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, mnamo tarehe 2 Juni 2017 Kamati ilitumia jeshi la polisi kufikishia Hati ya Wito iliyomtaka afike mbele ya Kamati tarehe 8 Juni 2017. Hata hivyo, Mhe. Nassari aliomba udhuru kuwa alikuwa anakutana na msimamizi wa mitihani yake (*dissertation*) na kuahidi kufika siku ya Alhamis tarehe 15 Juni, 2017 na Kamati iliridhia ombi hilo.

3.3 Mheshimiwa Spika, siku ya Alhamis tarehe 15 Juni, 2017 Mhe. Joshua Nassari alifika mbele ya Kamati ili kujibu tuhuma dhidi yake kama ifuatavyo:-

(e) Kuvuruga shughuli za Bunge kwa kupiga kelele na kupiga makofi kwa vurugu jambo ambalo lilimfanya Naibu Waziri wa Maji aliyekuwa ameruhusiwa kuzungumza kushindwa kuendelea kuzungumza kutokana na vitendo hivyo.

(f) Kukaidi maelekezo ya Naibu Spika aliyemtaka atulie ili kumruhusu Naibu Waziri wa Maji kuhitimisha hoja iliyokuwa mezani.

(g) Kuendelea kusimama na kupiga kelele wakati Naibu Spika alikutaka utulie.

(h) Kusambaza karatasi na vitabu hovyo kwa makusudi kitendo ambacho ni dharau kwa Bunge na kudharau Mamlaka ya Spika.

4.0 HOJA ZA MSINGI (*ISSUES*)

4.1 **Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo, ilijielekeza kwenye hoja za uchunguzi (*issues*) zifuatazo:

(c) Kama ni kweli Mhe. Joshua Nassari (Mb) alifanya vitendo vya utovu wa nidhamu na dharau kwa Mamlaka ya Spika,

(d) Kama itathibitika alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa dhidi yake?

4.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchunguzi wake, ilifanya rejea za Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, mashauri mbalimbali yaliyoamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*), na ushahidi wa picha za *video* za Ukumbini kama ifuatavyo:

4.1.1 Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296 R.E. 2015*].

4.1.2 Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

4.1.3 Picha za *video* (*video clip*) za Ukumbini.

5.0 MAHOJIANO YA SHAHIDI MBELE YA KAMATI

5.1 Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali, siku ya tarehe 15 Juni 2017 Mhe. Joshua Samweli Nassari (Mb) alifika mbele ya Kamati kama alivyoahidi. Mhe. Joshua Nassari (Mb) aliposomewa tuhuma dhidi yake alikiri wazi kuwa alitenda matendo yaliyolalamikiwa na Bunge na akaliomba radhi Bunge. Kwa maneno yake mwenyewe alisema yafuatayo:-.

“...Sitaki kupoteza muda wa Kamati, niombe radhi kwa lolote lilitotokea na kukwaza kitu cha Spika, dhamira yangu si kuja Dodoma ili kuletwa kwenye Kamati ya Maadili bali kuwatumikia wananchi na taifa kwa ujumla ... nakiri kosa na naomba radhi kwa Spika na kwa Bunge”

6.0 MAONI YA KAMATI (*FINDINGS*)

6.1 Mheshimiwa Spika, kuititia mkanda wa video wa tukio la siku hiyo, Mhe. Joshua Nassari (Mb) anaonekana akipiga makofi bila utaratibu, akikaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa mezani iendelee jambo ambalo ni dharau kwa Mamlaka ya Spika.

6.2 Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuangalia mkanda wa *video*, Mhe. Joshua Samweli Nassari (Mb) alikiri mbele ya Kamati na kuomba radhi Bunge kwa vitendo vya utovu wa nidhamu vinavyoonesha dharau kwa Bunge na kwa Mamlaka ya Spika, shughuli za Bunge, au mtu anayeongoza Shughuli za Bunge.

6.3 Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi huu, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa ni kweli Mhe. Joshua Nassari (Mb) alifanya vitendo ambavyo ni kudharau Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26(c) (d) (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

6.4 Mheshimiwa Spika, Kwa urahisi wa rejea nanukuu:
26. Any person who:-

- (a)
- (b)

- (c) *causes an obstruction or disturbance within the precincts of the Assembly Chamber during a sitting of the Assembly or of the Committee thereof; or*
- (d) *Shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or*
- (e) *Commit any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person proceeding at such proceedings, Commits an offense.*

"74 (1) Spika anaweza kutaja jina la Mbunge kwamba amedharau Mamlaka ya Spika na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiwa;

(a) Kwa maneno au vitendo, Mbunge huyo anaonyesha dharau kwa Mamlaka ya Spika; au

(b) Mbunge huyo anafanya kitendo chochote kwa makusudi cha kudharau Shughuli za Bunge au Mbunge yoyote anayeongoza shughuli hiyo.

6.5 **Mheshimiwa Spika**, Kwa mantiki hiyo,Kamati inamnia hatiani Mhe. Joshua Nassari (Mb) kwa Kudharau Mamlaka ya Spika.

6.6 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kujiridhisha kuwa Mhe. Joshua Nassari (Mb) alikiuka Sheria na Kanuni za Bunge, Kamati sasa inajielekeza katika hoja kwamba Kama itathibitika ni kweli alifanya vitendo hivyo, ni hatua gani anatakiwa kuchukuliwa?

6.7 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja hiyo kamati ilizingatia yafuatayo:-

(e) Katika shauri hili Mhe.Joshua Nassari alituhumiwa pamoja na Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) ambaye mnamo tarehe 2 Aprili, 2017 Bunge hili liliazimia kumsamehe kwa

kumpa karipio kali baada ya kukiri na kuliomba radhi mbele ya Kamati.

(f) Mhe. Joshua Nassari alikiri na kuliomba radhi Bunge bila kuisumbua Kamati.

(g) Hili ni kosa lake la kwanza kwa Mhe. Joshua Nassari (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika.

(h) Kitendo alichokifanya kilivuruga shughuli za Bunge na kimeshusha hadhi ya Bunge.

6.8 **Mheshimiwa Sipka**, Kifungu cha 33(1) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge kinalekeza kuwa Mbunge yeoyote atakayefanya kosa la kudharau Mamlaka ya Spika au shughuli za Bunge kwa mujibu wa Kifungu cha 26 au Kifungu kinginecho, Bunge linaweza kuazimla kumuelekeza Spika kumpa karipio kali (*reprimand*) au kumsimamisha asihudhurie vikao vya Bunge kwa muda litakaloona unafaa, isipokuwa muda huo usizidi siku ya mwisho ya Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya azimio hilo. Kifungu cha 33(1) kinasomeka ifuatavyo:

"33(1) Where any member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine".

7.0 UZOEFU WA MASHAURI YA YALIYOAMULIWA NA KAMATI

7.1 **Shauri lililomhusu Mhe. Salim Khamis Juma (Mb) aliyekuwa Mbunge kuitia Chama Cha Wananchi (CUF)**

Wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 1999/2000 alitamka maneno yalikuwa yanamtuhumu Spika wa Bunge kuwa ana maslahi ya Chama na anajihuisha na rushwa katika kuteua Wabunge kusafiri

nje ya nchi kikazi, alipoitwa mbele ya Kamati kuthibitisha alishindwa hivyo Kamati ilimtia hatiani kwa kudharau Mamlaka ya Spika. Kamati iliwasilisha taarifa ya uchunguzi kwa Spika na shauri lilimalizika kwa Mhe. Salim K. Juma kumwomba radhi Spika na Spika aliridhia.

7.2 Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria, uzoefu wa uamuzi uliotolewa katika Shauri la Mhe. Salim Khamis Juma (Mb) mashauri ya nyuma pamoja na kitendo cha Mhe. Joshua Nassari (Mb) kukiri na kuomba radhi, Hivyo, Bunge litafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuizingatia wakati wa kupitisha Azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilotenda.

8.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi ya kujadili na kuchambua kwa umakini shauri la kudharau Mamlaka ya Spika. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Kapt (Mst), George H. Mkuchika (Mb) M/Kiti
- (ii) Mhe. Almas A. Maige (Mb) - Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (iv) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (v) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)-Mjumbe
- (vi) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe

- (vii) Mhe. Rose Kamil Sukum (Mb)-Mjumbe
- (viii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (ix) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (x) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)-Mjumbe
- (xi) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)-Mjumbe
- (xii) Mhe. Asha Abdullah Juma (Mb)-Mjumbe
- (xiii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)-Mjumbe
- (xiv) Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka (Mb)-Mjumbe
- (xv) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)- Mjumbe; na
- (xvi) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)- Mjumbe

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudens R. Rweyongeza, Ndugu Mossy Lukuvi ambao ni Manaibu Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Mariamu Mbaruku Makatibu wa Kamati, na Ndugu Editruda Kilapilo na Ndugu Joyce Chuma kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadiri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

19 Juni, 2017

**Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya
ya Bunge Kuhusu Malalamiko ya MheshimiwaProfesa
Anna Kajumulo Tibaijuka dhidi ya Mheshimiwa
Conchesta Rwamlaza Aliyelalamikiwa Kusema
Uongo Bungeni**

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI
WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**
Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu malalamiko ya Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka dhidi ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza aliyelalamikiwa kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya nne (4) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza kudaiwa kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mamlaka ulionayo chini ya Kanuni ya tano (5) na 72 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliwasilisha malalamiko ya Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, Mbunge wa Jimbo la Muleba dhidi ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka alilalamika kuwa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alikiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) kwa kusema uongo Bungeni wakati alipokuwa akichangia mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uliagiza Kamati ichunguze na kutoa maoni yake kuhusiana na shauri hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chimbuko la Shauri. Mnamo tarehe 23 Mei, 2016 Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza wakati alipokuwa akichangia mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na mambo mengine alieleza kwamba Mheshimiwa Profesa

Anna Tibaijuka alipokuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alitumia madaraka yake vibaya kwa kujimilikisha zaidi ya ekari 4,000 katika Kijiji cha Kyamyowa na kwamba kiasi hicho cha ardhi ni zaidi ya kiasi alichokiomba kihalali ambacho ni ekari 1,098.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 23 Mei, 2016 katika ukurasa wa 124 na 125 zinaonesha kuwa Mhe. Rwamlaza pamoja na mambo mengine, alisema Bungeni maneno yafuatayo, ninanukuu:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye wawekezaji, Wabunge wengi sana wamelalamika kuhusu wawekezaji lakini wawekezaji hawa wako hata wanasiasa ambaao nao wanakwenda kwa ulaghai wao, wanakwenda kuhodhi ardhi kubwa katika Halmashauri zao. Mfano katika Mkoa wa Kagera tuna mgogoro mkubwa katika Wilaya ya Muleba. Mgogoro huu nina uhakika upo mezani kwa Mheshimiwa Waziri, kama haupo nina documents hapa akihitaji, kama hana nitampa.

Tuje kwa aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sijui nimitaje jina, aliyemfuata huko nyuma, Mheshimiwa Waziri anamjua. Yeye kwenye kata hiyo katika Kijiji cha Kyamyowa allomba ardhi ekari 1,098, sasa hivi anahodhi ardhi zaidi ya eka 4,000, kwa hiyo mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti namtaja si Profesa Tibaijuka ni dada yangu, si kwamba namsema ndani ya Bunge, lakini nakataa hii tabia ya kila kitu changu, kila kitu changu hapana. Ukiwa kiongozi wakati mwingine na wewe uwaachie wengine. Kama ni kiongozi huwezi kuhodhi ardhi, watu wanakuja kukodi kwako au watu hawawezi kufanya nini, ni tabia mbaya ambayo lazima tuikemee."

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maneno hayo ya tarehe 31 Mei, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka alimwandikia Mheshimiwa Spika malalamiko dhidi ya maneno hayo. Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka (Mheshimiwa Mbunge) alieleza kuwa madai hayo ni ya uongo na yanamchonganisha yeye na wananchi wa jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, waraka wako ulielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguza iwapo tuhuma zilizoelekezwa zilitolewa Bungeni na kama maelezo hayo ni ya uongo kisha ishauri kuhusu hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, taratibu za kuanza kusikiliza shauri hili zilianza ikiwa ni pamoja na kukusanya ushahidi na kuwaita mashahidi kupitia wito wa hati. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alitakiwa kufika mbele ya Kamati kujibu ni kwa nini asichukuliwe hatua za kisheria kwa kukiuka Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati. Kwa mujibu wa waraka ulioletwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maudhui katika malalamiko ya Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Kamati ilichunguza malalamiko hayo kwa kuzingatia hoja mbili muhimu ambazo ni zifuatazo:-

(a) Iwapo tuhuma zilizotolewa ni za kweli, kwamba Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na Kanuni za Bunge.

(b) Ikiwa hoja (a) itathibitika, ni hatua gani zinaweza kupendekezwa kuchukuliwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya uchambuzi Kamati ilianza kwa kujielekeza katika kujibu hoja ya kwanza, kwamba iwapo tuhuma zilizotolewa ni za kweli, kwamba

Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojano Mbele ya Kamati. Katika juhudhi ya kupata jibu la hoja hii, Kamati iliwahoji mashahidi, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza; tarehe 21, Aprili, Mheshimiwa Rwamlaza alifika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kama hati ya wito ilivyoelekeza. Kamati ilimhoji kuhusu tuhuma zinazomkabili na alieleza kuwa ni kweli alichangia mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi lakini hakusema Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka alipata ardhi kwa ulaghai.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliendelea kueleza kuwa ardhi hiyo ipo na kuna malalamiko ya wananchi ya kutaka ardhi hiyo ipimwe ili ekari 1,098 alizopewa Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka zifulikane na kiasi kilichoongezeka kirudishwe kwa wanakijiji. Alipouliwa kama ana uhakika kuwa ardhi anayomiliki Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ni zaidi ya ekari 4,000 alieleza kuwa hana uhakika huo bali ni jambo ambalo ameelezwa na wanakijiji na akasema, namnukuu;

"Hata Diwani wao alisema hivyo na ndiyo maana wanakijiji wanaomba eneo hilo lipimwe ili wajue eneo halali la Tibaijuka ambalo ni ekari 1,098"

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza aliwasilisha nyaraka zifuatazo kuhusiana na kile alichokisema Bungeni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nakala ya baruu yenye kumbukumbu tumeitaja hapo, ya tarehe 10, Februari kutoka kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda ya Ziwa aliyeko Mwanza kwenda kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera kuhusu mgogoro wa shamba hilo katika Kijiji cha

Kyamnyorwa, Kata ya Kasharunga, Wilaya ya Muleba. Barua hii inayohusu mgogoro wa ardhi inaonesha shamba hilo linamiliikiwa kihalali na haioneshi kuwa shamba hilo lina zaidi ya ekari 4,000 bali yapo maelekezo ya kupimwa kwa ardhi hiyo ili kumaliza mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, aliwasilisha nakala ya muhtasari wa mkutano wa hadhara wa Kijiji cha Kyamnyorwa wa tarehe 12, Machi, 2013 ulioambatanishwa majina ya wanakijiji 301 waliohudhuria mkutano huo. Muhtasari huo una malalamiko kwamba shamba linamiliikiwa visivyo halali na kuazimia lipimwe ili ekari zilizozidi zirudi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka. Kamati ilimsikiliza Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka siku ya tarehe 08 Juni, 2017 ili kupata ufanuzi kuhusu malalamiko yake. Mheshimiwa Profesa Tibaijuka alieleza kuwa katika Kijiji cha Kyamnyorwa kuna shamba la marehemu mume wake ambalo aliomba na kumilikishwa rasmi tangu mwaka 1991.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliendelea kueleza kuwa wakati marehemu mume wake anafanya maombi ya kupewa shamba hilo eneo hilo lilikuwa ni pori. Alifafanua kuwa mwaka 1997 alikabidhiwa hati namba 11304 ya tarehe Mosi Julai, 1997 ya shamba hilo baada ya kuwa limepiwa. Nakala ya hati hiyo ilipokelewa kama kielelezo. Ilifafanuliwa zaidi kuwa, shamba hilo lipo katikati ya hifadhi ya mazalia ya samaki, hivyo, haiwezekani kupanuliwa au kuongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, akijibu hoja ya kujilikisha akiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka alieleza kuwa shamba hilo lilikuwa la marehemu mume wake tangu mwaka 1991 kabla halijapimwa na alipatiwa hati mwaka 1997 baada ya kupimwa. Aliendelea kufafanua pia kuwa wakati marehemu mume wake anamilikishwa shamba hilo, yeye, Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka hakuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na aliteuliwa kuwa Waziri

wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwaka 2010, hivyo, madai ya Mheshimiwa Conchesta kwamba ye ye alijimilikisha hayana ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kamati. Baada ya kusikiliza maelezo ya mashahidi wote, Kamati ilijiridhisha kuwa suala la kwamba Mheshimiwa Profesa Tibaijuka anamiliki kihalali shamba katika Kijiji cha Kyamnyorwa, lenye ukubwa wa ekari 1,098 halibishaniwi. Uthibitisho huo upo katika maelezo ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka pamoja na hati ya shamba iliyowalishwa na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linalobishaniwa hapa ni kama Mheshimiwa Profesa Tibaijuka anamiliki ekari zaidi ya zile alizopewa, yaani sasa anamiliki ekari 4,000 ambazo amejiongezea visivyo halali. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alieleza Kamati kuwa hana uhakika kuhusu Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kumiliki ekari 4,000 isivyo halali bali aliambiwa hivyo na wanakijiji. Aidha, nyaraka alizowasilisha zinasisitiza kuwa eneo hilo lipimwe, hivyo, hazioneshi kuwa ni ekari 4,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitafakari ushahidi uliotolewa na kujiridhisha kuwa hakuna ushahidi kuwa eneo hilo lina ekari zaidi ya 4,000, tofauti na ukubwa uliopo kwenye hati ambao ni hekta 444, sawa na ekari 1,098. Aidha, kama ingekuwa ukubwa wake ungekuwa unajulikana, Mheshimiwa Conchesta asingeomba eneo lipimwe. Vile vile, kikao cha dharura cha kijiji kingekuwa kinajua kwamba ni 4,000, pamoja na barua ya Katibu Tawala, zisingetoa maelekezo ya kuomba eneo hilo lipimwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza hakuwahi kufanya utafiti wa kutosha ili kujiridhisha kuwa Mheshimiwa Profesa Tibaijuka anamiliki zaidi ya ekari 4,000 katika kijiji hicho kama alivyolieleza Bunge badala ya hekta 444, sawa na ekari 1,098 zilizopo katika hati anazomiliki kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za 63(1) na 64(1) za Kanuni za Kudumu za Bunge, zinaeleza kuwa Mbunge haruhusiwi kutoa taarifa au kusema uongo Bungeni. Kanuni hizo zinamtaka Mbunge kusema au kutoa taarifa ambazo ana uhakika nazo. Kanuni hizo zinaweka masharti kwa Mbunge anayezungumza ndani ya Bunge kuwa na uhakika wa jambo analolisema na si kuegemea maelezo ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(6) inamtaka Mbunge anayelalamikiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge ndani ya muda atakaopewa na Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sheria na Kanuni za Bunge pamoja na ushahidi ulliotolewa na mlalamikiwa, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kwamba Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alisema uongo Bungeni kinyume cha Kanuni za 63 na 64 za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; kwa mantiki hiyo, Kamati inamtia hatiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja ya kwanza sasa tujielekeze katika hoja ya pili, kwamba, ikiwa hoja ya kwanza imethibitika ni hatua gani zinaweza kupendekezwa kuchukuliwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(8) inaeleza kuwa Mbunge aliyetakiwa kutoa uthhibitisho kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge ikiwa atashindwa kufanya hivyo au atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi wake, Spika atamuadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi vitano. Katika kupendekeza adhabu, Kamati ilizingatia mambo yafuatayo:-

(a) Hili ni kosa la kwanza kwa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza (Mbunge).

(b) Kauli alizotoa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza zilimshushia heshima Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka mbele ya Bunge na mbele ya jamii anayoiongoza.

(c) Kauli hizo pia zilikuwa za kumgombanisha Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka na wananchi wa eneo hilo ambalo lipo ndani ya jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo, Kamati inapendekeza kuwa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza asimamishwe kuhudhuria Vikao vitatu vya Mkuutano wa Saba unaoendelea wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kukushukuru wewe, Katibu wa Bunge na watendaji wa Bunge walioituwezesha kutekeleza majukumu yetu. Napenda kuwashukuru pia Wajumbe wenzangu wa Kamati ambao kwa pamoja, bila kujali itikadi zetu tulitafuta haki na kufikia uamuzi muafaka wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA
YA BUNGE KUHSU MALALAMIKO YA MHESHIMIWA
PROFESA ANNA K. TIBAIJUKA (MB) DHIDI YA
MHESHIMIWA CONCHESTA RWAMLAZA (MB)
ALIYELALAMIKIWA KUSEMA UONGO BUNGENI
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 4(3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza (Mb) kudaiwa kusema Uongo Bungeni.

1.2 Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 5 na 72 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la

Januari, 2016, tarehe 11 Julai, 2016, uliwasilisha Malalamiko ya Mheshimiwa Prof.Anna Tibaijuka, Mbunge wa jimbo la Muleba dhidi ya Mhe. Conchesta Rwamlaza Mbunge wa viti Maalum kutoka Mkao wa Kagera. Mhe.Prof Anna Tibaijuka alilalamika kuwa Mhe.Conchesta Rwamlaza alikiuka Kanuni ya 63(1) na 64(1)(a) kwa kusema uongo Bungeni wakati alipokuwa akichangia mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uliagiza Kamati ichunguze na kutoa maoni yake kuhusiana na shauri hili.

2.0 CHIMBUKO LA SHAURI LA MALALAMIKO YA MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA (MB) DHIDI YA MHE. CONCHESTA RWAMLAZA (MB)

2.1 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 23 Mei, 2016 Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) wakati alipokuwa akichangia mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na mambo mengine alieleza kwamba Mhe. Prof. Anna K. Tibaijuka alipokuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alitumia madaraka yake vibaya kwa kujimilishwa zaidi ya ekari 4,000 katika Kijiji cha Kyamyorwa na kwamba kiasi hicho cha ardhi ni zaidi ya kiasi alichokionomba kihalali ambacho ni ekari 1,098.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 23 Mei, 2016 katika ukurasa wa 124 na 125 zinaonesha kuwa Mhe. Rwamlaza pamoja na mambo mengine, alisema Bungeni yafuatayo:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye wawekezaji, Wabunge wengi sana wamelalamika kuhusu wawekezaji lakini wawekezaji hawa wako hata wanasiasa ambao nao wanakwenda kwa ulaghai wao, wanakwenda kuhodhi ardhi kubwa katika Halmashauri zao. Mfano katika Mkao wa Kagera tuna mgogoro mkubwa katika Wilaya ya Muleba. Mgogoro huu nina uhakika upo mezani kwa Mheshimiwa Waziri, kama haupo nina documents hapa akihitaji kama hana nitampa

...tuje kwa aliyekuwa Waziri wa ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sijui nimirage jina, aliyeemuata huko nyuma, Mheshimiwa Waziri anamjua. Yeye kwenye kata hiyo katika Kijiji cha Kyamyorwa aliomba ardhi ekari 1,098 sasa hivi anahodhi ardhi zaidi ya eka 4,000 kwa hiyo mgogoro mkubwa....

Mheshimiwa Mwenyekiti namtaja si Profesa Tibaijuka ni dada yangu si kwamba namsema ndani ya Bunge, lakini nakataa hii tabia ya kila kitu changu, kila kitu changu hapana. Ukiwa kiongozi wakati mwingine na wewe uwaachie wengine. Kama ni kiongozi huwezi kuhodhi ardhi, watu wanakuja kukodi kwako au watu hawawezi kufanya nini, ni tabia mbaya ambayo lazima tuikemee..”

2.3 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na maneno hayo, tarehe 31 Mei, 2016 Mhe. Prof. Tibaijuka (Mb) alimwandika Mhe. Spika malalamiko dhidi ya maneno hayo. Mhe. Prof. Anna K. Tibaijuka alieleza kuwa madai hayo ni ya uongo na yanamchonganisha na wananchi wa Jimbo lake.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, waraka wako uliilekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuchunguza iwapo tuhuma zinazoelezwa zilitolewa Bungeni, na kama maelezo hayo ni ya uongo kisha ishauri kuhusu hatua za kuchukua.

2.5 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelekezo hayo taratibu za kuanza kusikiliza shauri hili zilianza ikiwa ni pamoja na kukusanya ushahidi na kuwaita mashahidi kupitia hati za wito. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza (Mb) alitakiwa kufika mbele ya Kamati kujibu ni kwanini asichukuliwe hatua za kisheria kwa kukiuka Kanuni ya 63 (1) na 64 (1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

3.0 MAMLAKA YA KAMATI KUSHUGHULIKIA SUALA HILI

3.1 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 4(1) (a) na (b) inaipa Kamati mamlaka ya kusikiliza shauri hili. Kwa urahisi wa rejea nanukuu Kanuni hiyo:

"4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) *Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika; na*
- (b) *Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika".*

4.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU SHAURI LA KUDAIWA KUSEMA UONGO BUNGENI DHIDI YA MHESHIMIWA CONCHESTA RWAMLAZA (MB)

4.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa waraka ulioletwa mbele ya Kamati na kwa kuzingatia maudhui katika malalamiko ya Mhe. Prof. Anna K. Tibaijuka (Mb) Kamati ilichunguza malalamiko hayo kwa kuzingatia hoja mbili muhimu ambazo ni:-

(a) Iwapo tuhuma zilizotolewa ni za kweli kwamba, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na Kanuni ya 63(1) na 64(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

(b) Ikiwa hoja (a) itathibitika, ni hatua gani zinaweza kupendekewa kuchukuliwa na Bunge kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge.

4.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kufanya uchambuzi wa kina na kujibu kikamilifu suala hili, Kamati imefanya rejea sheria na nyaraka zifuatazo;

- (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.
- (ii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.
- (iii) Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 23 Mei, 2016.

4.3 **Mheshimiwa Spika**, Katika kufanya uchambuzi Kamati ilianza kwa kujielekeza katika kujibu hoja ya kwanza kwamba, *Iwapo tuhuma zilizotolewa ni za kweli kwamba, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alisema uongo au kutoa taarifa ambazo hazina ukweli kinyume na Kanuni ya 63(1) na 64(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.*

5.0 MAHOJIANO MBELE YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kupata jibu la hoja hii, Kamati iliwahoji mashahidi Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) na Prof. Anna Tibaijuka (Mb) kama ifuatavyo:-

5.1 Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 21 Aprili, 2017 Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) alifika mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kama Hati ya wito ilivyoelekeza. Kamati ilimhoji kuhusu tuhuma zinazomkabili na alieleza kuwa ni kweli alichangia mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi lakini hakusema Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (Mb) alipata ardhi kwa ulaghai.

Aliendelea kueleza kuwa ardhi hiyo ipo na kuna malalamiko ya wananchi ya kutaka ardhi hiyo ipimwe ili ekari 1,098 alizopewa Mhe. Anna K. Tibaijuka zijulikane na kiasi kilichoongezeka kirudishwe kwa wanakijiji. Alipoulizwa kama ana uhakika kuwa ardhi anayomiliki Mhe. Prof Anna Tibaijuka ni zaidi ya ekari 4,000 alieleza kuwa hana uhakika huo bali ni jambo ambalo ameellezw na Wanakijiji

“...hata diwani wao alisema hivyo na, ndiyo maana wanakijiji wanaomba eneo hilo lipimwe ili wajue eneo halali la Tibaijuka ambazo ni eka 1,098 zijulikane...”.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) aliwasilisha nyaraka zifuatazo kuhusiana na kile alichokisema Bungeni

- (i) Nakala ya barua yenyewe Kumb. Na. LD/LZ/GF/54/18 ya tarehe 10 Februari, 2016 kutoka kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda ya Ziwa kwenda kwa Katibu Tawala Mkoa wa Kagera kuhusu mgogoro wa shamba Na. 270 katika Kijiji cha Kyamyorwa, Kata ya Kasharunga, Wilaya ya Muleba. Barua hii inahusu mgogoro wa ardhi inaonesha shamba hilo linamilikiwa kihalali na haioneshi kuwa shamba hilo lina zaidi ya ekari 4,000 bali yapo maelekezo ya kupimwa kwa ardhi hiyo ili kumaliza mgogoro.
- (ii) Nakala ya Muhtasari wa mukutano wa dharura wa hadhara wa Kijiji cha Kyamyorwa wa tarehe 12 Machi, 2013, ulioambatinishwa majina ya wanakijiji 301 waliohudhuria kikao hicho. Muhtasari una malalamiko kuwa shamba linamilikiwa visivyo halali na kuazimia lipimwe ili ekari zilizozidi zirudi kwa wananchi.

5.2 **Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (mb)**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimsikiliza Mhe. Prof. Anna Tibaijuka siku ya tarehe 8 Juni, 2017 ili kupata ufanuzi kuhusu malalamiko yake. Mhe. Prof. Anna Tibaijuka alieleza kuwa katika Kijiji cha Kyamyorwa kuna shamba la marehemu mume wake ambalo aliomba na kumilikishwa rasmi tangu mwaka 1991. Aliendelea kueleza kuwa wakati marehemu mume wake anafanya maombi na kupewa shamba hilo, eneo hilo lilikuwa ni pori. Alifafanua kuwa mwaka 1997 alikabidhiwa Hati Namba 11304 ya 1 Julai 1997 ya shamba hilo baada ya kuwa limepimwa. Nakala ya Hati hiyo ilipokelewa kama kielelezo.

Mheshimiwa Spika, Ilifafanuliwa zaidi kuwa, shamba hilo lipo katikati ya hifadhi ya mazalia ya samaki hivyo haiwezekani kupanuliwa au kuongeza. Akijibu hoja ya kuwa alijimilikisha akiwa waziri wa Ardhi, Mhe. Prof. Anna Tibaijuka alieleza kuwa shamba hilo lilikuwa la marehemu mume wake tangu mwaka 1991 kabla halijapimwa na alipatiwa Hati mwaka 1997 baada ya kupimwa. Aliendelea kufafanua pia kuwa wakati marehemu mume wake anamilikishwa shamba hilo yeche (Mhe. Prof. Anna Tibaijuka) hakuwa waziri wa Ardhi,

nyumba na Maendeleo ya Makazi na aliteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi mwaka 2010 hivyo madai ya Mhe. Conchesta hayana ukweli.

6.0 MAONI YA KAMATI

7.1 Mheshimiwa Spika, Baada ya kusikiliza maelezo ya mashahidi wote Kamati ilijiridhisha kuwa suala la kwamba Mhe. Anna Tibaijuka anamiliki kihalali shamba katika Kijiji cha Kyamyorwa lenye ukumbwa wa ekari 1,098 halibishaniwi. Uthibitisho huo upo katika maelezo ya Mhe. Conchesta Rwamlaza na Mhe. Prof. Anna Tibaijuka pamoja Hati ya Shamba iliyowasilishwa na Mhe. Prof. Anna Tibaijuka. Suala linalobishaniwa ni kama Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (Mb) anamiliki zaidi ya ekari 4000 ambazo amejiongezea visivyo halali.

7.2 Mheshimiwa Spika, Mhe. Conchesta Rwamlaza aliieleza Kamati kuwa hana uhakika kuhusu Mhe. Prof. Anna Tibaijuka kumiliki zaidi ekari 4,000 isivyo halali bali aliambiwa hivyo na wanakijiji. Aidha, nyaraka alizowasilisha zinasisitiza kuwa eneo hilo lipimwe hivyo hazioneshi kuwa ni ekari zaidi ya 4000. Kamati ilitafakari ushahidi uliotolewa na kujiridhisha kuwa hakuna ushahidi kuwa eneo hilo lina ekari zaidi ya 4000 tofauti na ukubwa uliopo kwenye Hati ambao ni hekta 444 sawa na ekari 1098. Aidha, kama ingekuwa ukubwa wake ungekuwa unajulikana Mhe. Conchesta, asingeomba lipimwe. Vilevile kikao cha dharura cha kijiji pamoja barua kwa Katibu tawala zisingetoa maelekezo ya kupima eneo hilo.

7.3 Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo ni dhahiri kuwa Mhe. Conchesta hakuwahi kufanya utafiti wa kutosha ili kujiridhisha kuwa Mhe. Tibaijuka anamiliki zaidi ya ekari 4,000 katika kijiji hicho kama alivyolieza Bunge badala hekta 444 sawa na ekari 1,098 zilizopo katika Hati anazomiliki kihalali.

7.4 Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 63 (1) na 64(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinaleza kuwa Mbunge haruhusiwi kutoa taarifa au kusema uongo Bungeni. Kanuni

hizo zinamtaka Mbunge kusema au kutoa taarifa ambazo ana uhakika nazo. Nanukuu:

"63(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge ye yote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo ye ye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu".

"64(1) (a) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(c) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli".

7.5 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni hizi zinaweka masharti kwa mbunge anayezungumza ndani ya Bunge kuwa na uhakika wa jambo analolisema na siyo kuegemea maelezo ya mtu mwengine.

7.6 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 63(6) inamtaka Mbunge anayelalamikiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatao Bungeni kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge ndani ya muda atakaopewa na Spika.

7.7 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sheria na Kanuni za bunge pamoja ushahidi uliotolewa na mlalamikaji na mlalamikiwa, Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) alisema uongo Bungeni kinyume cha Kanuni ya 63 na 64 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2017. Kwa mantiki hiyo Kamati ilimtia hatiani.

7.8 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kujibu hoja ya Kwanza, sasa tujielekeze katika hoja ya Pili kwamba: Ikiwa hoja ya Kwanza itathibitika, ni hatua gani zinaweza kupendekezwa kuchukuliwa na Bunge kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge

7.9 **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 63(8) inaeleza kuwa Mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitisho kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge ikiwa atashindwa kufanya hivyo au atakataa kujirekebisha, kwa kufuta kauli au usemi wake, Spika atamwadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi vitano.

Mheshimiwa Spika, katika kupendekeza adhabu Kamati ilizingatia yafuatayo:

(a) Hili ni kosa la kwanza kwa Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb).

(b) Kauli alizotoa Mhe. Conchesta Rwamlaza zilimshushia heshima Mhe. Prof. Anna Tibaijuka mbele ya Bunge na jamii anayoiongoza.

(c) Kauli hizo pia zillikuwa za kumgombanisha Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (Mb)na wananchi wa eneo hilo ambalo lipo ndani ya Jimbo lake

7.10 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia misingi hiyo Kamati inapendekeza kuwa Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) asimamishwe kuhudhuria vikao vitatu vya Mkutano wa Saba unaendelea wa Bunge la Bajeti.

7.0 HITIMISHO

8.1 **Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu

8.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini shauri la kusema uongo bungeni. Wajumbe hawa walifanya kazi kwa kuzingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- (xvii) Mhe. Kapt. Mst, George H. Mkuchika(Mb) -M/Kiti
- (xviii) Mhe. Almas A. Maige (Mb) - Makamu Mwenyekiti
- (xix) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (xx) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (xxi) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)-Mjumbe
- (xxii) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe
- (xxiii) Mhe. Rose Kamil Sukum (Mb)-Mjumbe
- (xxiv) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (xxv) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (xxvi) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)-Mjumbe
- (xxvii) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)-Mjumbe
- (xxviii) Mhe. Asha Abdullah Juma (Mb)-Mjumbe
- (xxix) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)-Mjumbe
- (xxx) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)-Mjumbe
- (xxxi) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)- Mjumbe; na
- (xxxii) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)- Mjumbe

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudens R. Rweyongeza, Ndugu Mossy Lukuvi ambaao ni Manaibu Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Seraphine Tamba na Mariam Mbaruku Makatibu wa Kamati,Bi.Joyce Chuma na Ndg. Editruda Kilapilo kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

19 Juni, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshasikia na kusoma Ripoti ya Kamati kuhusu Waheshimiwa Wabunge wawili; Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Joshua Nassari.

Nimeletewa hapa wachangiaji, upande wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo sijapata bado jina. Tutaanza na Mheshimiwa Hamidu Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Khadija Aboud ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wenzangu hapa wanankumbusha kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti hakutoa hoja na wala haikuungwa mkono sasa sijui niendelee tu, maana yake hoja haikutolewa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali, naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hoja ya Kamati hii, tofauti na Kamati nyingine, sisi ndio tunaotaka kufanya jambo hapa ndani. Sasa ye ye akitoa hoja tunaunga mkono hoja ipi, kwa sababu sisi ndio tunaotaka kulifanya jambo, wao walichotusaidia ni kuongea na wale watu ili watuletee sisi tufanye maamuzi. Sasa akitoa hoja maana yake tunaungana na alichosema, ndiyo maana tunataka kuzungumza sisi hapa ndani kuhusu hoja yake ye ye, tofauti na nyingine. Ndiyo maana wakishaleta hapa tunaanza mjadala, tunaanza Serikali, tunaanza upande huu na upande huu na kitu kama hicho, lakini Kamati hii iko tofauti kidogo.

Mheshimiwa Bobali!

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nikubaliane kabisa na pendekezo la Kamati kuhusu Mheshimiwa Joshua Nassari na kwa kuwa Mheshimiwa Nassari alivyokwenda alieleza ukweli na Kamati imependekeza jambo jema, kwamba Mheshimiwa Nassari ni bora asamehewe. Kwa hiyo, naunga mkono, Bunge hili tumsamehe Mheshimiwa Joshua Nassari kwa sababu

alichokieleza amekubali na amesema kwamba jambo liishe, hakutaka kuchelewesha, kwa hiyo naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la Mheshimiwa Conchesta; Mheshimiwa Mwenyekiti wakati anasema ameelezea kabisa mwishoni, kwamba hili ni kosa lake la kwanza, na kama ni kosa lake la kwanza mimi naona pia kuna haja na yeye ya kumsamehe kwa sababu ni kosa lake analifanya kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ukipima athari ya kile alichokisema na mwathirika mwenyewe, mimi sioni kama jambo hili litakuwa limemuathiri sana Mheshimiwa Profesa Tibaijuka. Kama Mbunge alishindwa kuthibitisha tayari amepata sehemu ya kwenda kuanzia kuwaeleza wananchi wake kama itakuwa wananchi wake wamepata *confusion*, kwamba jambo hili lilijadiliwa Bungeni na likaonekana kwamba halina ukweli. Kwa hiyo, kama haliwezi kumuathiri Mheshimiwa Profesa Tibaijuka kwa nini tumwadhibu Mheshimiwa Conchesta?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana, na kwa kuwa tunamaliziamalizia Bunge na kwa kuwa tumekuwa na sikukuu tu, wengine tumemaliza jana, naomba tumalize vizuri. Tuondoke hapa vizuri kabisa, isiwe wengine wanasimamishwa wanatoka hapa *confusion* ya kusimamishana, tuondoke vizuri kabisa, tuagane vizuri kabisa, tukutane mwezi wa Nane, mwezi wa Tisa tukiwa wote tuko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niombe Bunge libatilishe au liridhie kwamba adhabu ya Mheshimiwa Conchesta isiendolee, badala yake tumpe msamaha kwa kuwa yeche na kosa lake la kwanza na athari yake si kubwa sana kwa Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo tu hoja ilio mbele yetu. Hata hivyo, naomba tu nitoe ufanuzi kidogo; mimi naitwa Juma Nkamia na si Mkamia kama ambavyo amekuwa akinitamka kaka yangu hapa, Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na hili suala la Mheshimiwa Joshua Nassari. Mimi nilisimama hapa Bungeni kuomba Mwongozo kuhusu wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma amba walikuwa wameondolewa chuoni. Ni kweli wanafunzi walikuwa katika hali tete wakati huo, lakini pengine tu kulikuwa na mawasiliano kati ya Serikali na uongozi wa chuo na ndicho kilichotufanya hata sisi wengine tukalizungumza. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais alikuja kulitolea ufanuzi vizuri sana na Mheshimiwa Nassari alikuja akalichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme, kuna Mheshimiwa, kaka yangu pale, amesema hapa kwamba kwa kuwa ni kosa la kwanza basi wasamehewe; na mimi naamini kabisa kama tutafikia hatua kwamba kila mtu akifanya kosa la kwanza anasamehewe, kwa hiyo hata anayeua anaweza kwenda Mahakamani akasema ni kosa la kwanza niacheni, unaweza ukaamua ukabaka ukasema ni kosa la kwanza niacheni. Mimi nadhani Kanuni ya 74, ile fasili ya 3(a) na (b) ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kiongozi yejote, kama tulivyo sisi Waheshimiwa Wabunge kwanza anatakiwa adhibiti msongo wa mawazo ili kufanya akili yake ifikie maamuzi sahihi bila kunyemelewanyemelewa na tabia za utotoutoto katika /eve/ hii tuliyonayo. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Nassari alifanya vile, ni kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kiongozi anatakiwa kufuata haki katika kuongoza kwake, asijione mwenye haki zaidi ya watu wengine. Mimi uliponiomba; bahati nzuri ulikaa hapo kwenye Kiti; kwamba Mheshimiwa Nkamia mwongozo wako labda haukuata taratibu nilikaa kimya na sikufanya pupa yoyote kwa sababu nazingatia nini maana ya kile yule anayekuongoza anakwambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Nassari nafikiri yeye alifanya pupa, ndiyo maana nikasisitiza kwamba sheria tu ichukue mkondo wake, lakini kuchukua habari kwamba hili ni kosa la kwanza tuwasamehe, itafika wakati tutasamehe watu wote, hata kwenye Mahakama zetu kutakuwa hakuna kazi kwa sababu akifika Mahakamani kosa la kwanza aondoke tu; na watu wamefanya mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bado sielewi sana ndani ya Bunge hili, Bunge linaendeshwa kwa Kanuni lakini kuna watu wanasema uongo sana ndani ya Bunge hili. Tukiacha mchezo huu ukaendelea, utaendelea kujirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Mheshimiwa Conchesta sitaki kulisemea sana lakini mimi narudia tu kwamba sheria...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia, muda wako umekwisha.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja na naomba adhabu kali ichukuliwe.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati yetu ya Maadili kwa kazi kubwa wanayoifanya kila yanapotokea matatizo ya ukosefu au utovu wa nidhamu ndani ya Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mheshimiwa Nassari, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati, lakini kwa kulinda heshima ya Bunge na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tujitambue kama ni Waheshimiwa Wabunge wawakilishi wa wananchi, napendekeza apewe karipio kali ili ive fundisho kwa sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe tunajitambua wakati wa kutenda shughuli zetu kama Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mheshimiwa Conchesta nakubaliana na mapendekezo ya Kamati. Kamati imejitahidi, imetumia busara, imetumia pia na huruma hapa, lakini nakubaliana na mapendekezo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo, tutamalizia na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Mheshimiwa Musukuma!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, natafuta *microphone*.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, *microphone* hii hapa.

MBUNGE FULANI: *Microphone* hii hapa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mimi nimeshampatia tayari.

MBUNGE FULANI: Njoo utumie hii hapa, mimi naondoka.

NAIBU SPIKA: ...Basi acha Mheshimiwa Bulembo aanze lakini zimeni hizo *Microphones* zote ili ziweze kufanya kazi

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siungani mkono kabisa na mapendekezo ya Kamati kwa sababu moja. Kwanza suala la Mheshimiwa Tibaijuka; kama alivyozungumza Mbunge kwamba suala hili halina madhara makubwa; mimi nadhani ye ye haelewi ugumu wa ugombeaji kwenye Jimbo. Maneno yale yalivyokwenda Jimboni, gharama ya kujisafisha Tibaijuka hailingani na hata adhabu tutakazompa humu ndani. Kwa hiyo, nadhani waliloguswa ni wapigakura...

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: ...wa Mheshimiwa Tibaijuka...

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, na naomba...

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: ...ukisoma hizi Kanuni, Kanuni ya 74...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali unataka kumpa taarifa kuhusu nini kwenye hili? Kwa sababu anayozungumza ni wewe umesema ama?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba mimi niliyesema haina madhara makubwa sijui gharama ya ugombeaji, mimi ni Mbunge wa Jimbo.

NAIBU SPIKA: Sawa wewe ni Mbunge wa Jimbo pengine Jimbo lako ndiyo maana anazungumza vile, nadhani hata ye ye anajua kwamba wewe ni Mbunge mwanaume kwahiyu huwezi kuwa umekuja na Viti Maalum humu ndani, Mheshimiwa Kasheku

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru anatafuta umaarufu kwenye *media* kwamba alinipa mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya Mheshimiwa Tibaijuka kujisafisha kule Jimboni Kyamyorwa si sawa na adhabu tutakayotoa huku; na wananchi wale hata huo mgogoro aliousema pale; mimi nimeenda pale na Mama Tibaijuka kwenye shamba lake wakati akiwa mlezi wa Mkoa wa Geita; wala hakuna mgogoro na wananchi wengi wallioko pale ni Wasukuma, mgogoro huu unatengenezwa kwa Wanasiasa kwa vivu. Kwani mtu kumiliki hekari 1,500 kuna matatizo gani kwa Mbunge anayepata mshahara na ana mkopo? Tusitishane!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachoona, ni haki yake. Kwa bahati nzuri au mbaya Mheshimiwa Rais alisimama pale akawatolea maelekezo kwamba shamba ni lake halali sasa bado tunajadili kitu gani kupakana matope? Naomba ile adhabu twende kwenye Kanuni ya tatu (3) na sita (6) kutoka kwenye Kanuni ya 74, ina maelekezo ya kosa la kwanza kuna vikao nane ambavyo anatakiwa asihudhurie, twende kwenye msimamo huo lakini tusitoe msamaha. Hii misamaha tukiendelea kuitoa watu wote tutakuwa tunafanya makosa, tunategemea misamaha, tunakiri tu kwa Mkuchika halafu tunakuja kuomba msamaha humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, suala la Nassari; kwanza Nassari ni Mbunge mzoefu wa awamu ya pili na sisi Wabunge wengine tunatamani kujifunza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa zamani na Kanuni hizi wanazisoma vizuri na ye ye ni Msomi anafanya Shahada ya Uzamili, Kanuni ziko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili si kosa la kwanza kama Kamati ilivyoeleza. Mheshimiwa Nassari amebebwa hapa msobe msobe kipindi kile alifanya fujo anatupa makaratasi akatolewa; hili ni la pili la kudharau Mamlaka ya Spika. Sasa kama Spika au Naibu Spika tutakuwa tunakudharau humu ndani, kuna wengine wana mawazo ya ajabu kabisa humu ndani wewe, ndiwe unayetakiwa kutu-control/sisi; halafu mtu anafanya makosa ya kudharau kiti cha Spika, tunasema tumsamehe, tuenze upya, kulikuwa na *Eid*, sikukuu ziko nyingi, baada ya *Eid* tuna...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: ...kwenye Kanuni hiyo hiyo.

MHE. ALH. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mzee Mkuchika na Kamati yake kwa kazi kubwa waliyofanya, ni nzuri sana. Mzee Mkuchika namheshimu sana na ni Mzee wa busara sana, Kamanda wa Kijeshi huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Musukuma Kanuni ya 74; mimi juzi hapa nilikuwa mmajawapo nilyemtetea Halima Mdee na Esther Bulaya humu humu ndani kwamba ni vijana wetu, tuwasamehe, tufanye nini haikwisha wiki, moto ukawashwa. Sasa vitabu hivi mmeweka vyatini? Mmendika vyatini kama haviwezi kutumika? Tunatengeneza Kanuni, Mzee Mkuchika ninavyokuheshimu kwa heshima yako yote unasema tunasamehe, tutasamehe wangapi? Hoja ya kusamehe inapatikanaje? Kwa sababu hawa ni watoto wetu ukimsamehe leo kesho atakuja na *style* nyingine, hoja jamani si kusameheana; hoja ni Kanuni mliziandika, mzfanyie kazi.

Katika Kanuni ya 74, Mzee Mkuchika mna kakipengele kadogo mlilikatumbia hapa namba nne (4), Bunge linaweza kuzingatia, yaani huo ushauri; lakini tano (5) na sita (6) imesema inaweza kukubali Bunge au lisikubali. Vile vifungu vinavyozungumzia vikao 10, vikao 20 vinatakiwa vifanyiwe kazi ili tupeane heshima humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo mnayaona ni mdogo, watoto wetu, vijana wetu, hapana. Akikosea mtu; kama alivyosema Mheshimiwa Nkamia, ina maana mtu akifanya kesi ya kuua kosa la kwanza basi hatanyongwa? Hapana, suala la kusamehe limetuletea madhara na madhara yamerudi humu ndani. Leo waliosamehewa wakatolewa nje leo wako Mahakamani wana-*file case*. Ina maana Bunge kila likiamua kuna watu watakwenda kufungua kesi? Hapana, ili mradi wale wa kwanza walismehewa, wakarudia leo wametolewa wamekwenda Mahakamani kulishtaki Bunge na kumshtaki Spika, lazima tuheshimu nafasi ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu waliokosa wale vile vikao 10 na vikao 20 kwa mujibu wa Kanuni inavyosema, Kanuni tumeandika za nini? Mzee Mkuchika tunakuheshimu, katika hili mimi nakuheshimu labda kuliko watu wengi umenilea tangu mdogo, lakini katika hili msamaha wako umefika mwisho, huwezi kusamehe kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachukuliwe adhabu kwa mujibu wa Kanuni, naomba...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana muda wako umekwisha.
Mheshimiwa Fatma Toufiq

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami pia naomba niungane na wenzangu kwa kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya, ila nami naomba niungane na wasemaji waliopita kwamba hebu

tufuate Kanuni zinasemaje. Kwa sababu haya mambo ukichelea mwana kulia mwisho wa siku utalia wewe. Kwa hiyo naomba kushauri kwamba, adhabu zitolewe kwa jinsi Kanuni inavyotaka, hakuna msamaha kwa sababu tumetoa msamaha kwa wenzenetu, tumeona kabisa mambo ya hovyo ambayo wameyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nalishauri Bunge lako Tukufu kwamba tufuate zile Kanuni jinsi zilivyo, Kanuni ya 74(3)(a) na (b) ili adhabu zitolewe kwa jinsi utaratibu ulivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru, naunga mkono kwamba lazima waadhibiwe kulingana na utaratibu, hakuna msamaha hapa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Toufiq. Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili.

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kunipa nafasi ya kujibu hoja zilizotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema moja la jumla. Sisi kwenye Kamati yetu kama mmesikiliza tangu mwanzo mpaka mwisho tumekuwa tunataja vifungu tulivyovitumia. Kwa hiyo, naomba niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge mlio sema kwamba pengine Kanuni hatuzifuati. Kanuni tumezifuata na kila uamuvi tuliofanya, tumeufanya kwa kuzingatia Kanuni, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; ndugu yangu Bobali unasema Mheshimiwa Nassari anakubali, Mheshimiwa Conchesta asamehewe, Tibaijuka hakuathirika. Naomba humu ndani; ndiyo maana nadhani kabla hatujaanza Ubunge kila mtu anashika Msahafu anaouamini kula kiapo; kwamba ukiwa humu ndani siku zote utasema kweli. Hivi ni kweli kwamba Mbunge ana shamba kwenye Jimbo lake,

anamiliki kwa hati aliyopewa na Serikali, anatuhumiwa na watu kwamba amejiongezea eneo bila utaratibu; ni kweli ndugu yangu Bobali ukishamsema hivyo ndani ya Bunge ni kweli kwamba hajaathirika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikubaliani na yeye. Ndiyo maana Kanuni zetu zinasema Mbunge akiona kwamba amekuwa *aggrieved*, akijiona kwamba yeye ametendewa visivyo analalamika kwa Spika na ndiyo maana Mheshimiwa Tibaijuka amelalamika kwa Spika kwamba “*sikutendewa haki, nimegonganishwa, nimechonganishwa na wapiga kura wangu kwamba shamba walilonipa mimi nimejiongezea kwa kutumia madaraka yangu ya Uwaziri wa Ardhi*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechunguza wakati mumewe anapewa shamba Tibaijuka hakuwa Waziri wa ardhi. Mimi humu ndani jamani yale mambo ambayo ni dhahiri, ambayo yako wazi siku nydingine tuwe tunanusuru muda, tufanye mambo waliyotutuma wananchi. Katika hili nataka niseme hakuna ushahidi mkubwa katika kesi hii ni hati anayomiliki Mheshimiwa Tibaijuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa eneo umetajwa mule ndani. Kwamba amejiongezea tumelelezea; Kamati imejiridhisha kwamba hakuna ushahidi wa kuongezewa eneo kwa sababu hata yule Afisa Mfawidhi wa Kanda pale Mwanza ameshauri, wale wanaolalamika eneo lipimwe, eneo halijapimwa. Kwa hiyo huyu anayesema hekta 4,000 ni maneno ya barabarani, hakuna aliyepima akapata hiyo 4,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemuuliza Mheshimiwa Conchesta tueleze hiyo 4,000 umeipata wapi akasema “*nimewasikia walalamikaji*” hivi Mbunge unaokota maneno ya walalamikaji unayaleta hapa bila kuyafanyia *research?* *Mao Tse Tung* anasema “*no research, no right to speak*”. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Nkamia anasema Mheshimiwa Nassari ni Mbunge mzoefu, kwa hiyo kidogo hukuridhishwa na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Wabunge wenzangu; shauri la Nassari si la juzi, Mheshimiwa Nassari alishtakiwa siku moja yeye na Bulaya. Tumechelewa kulimaliza Shauri Lake, hakuwepo alikuwa anasoma Uingereza. Aliporudi ndiyo maana leo linaonekana kama ni jambo jipywa la juzi. Alitenda kosa siku moja na Esther Bulaya na Bunge hili hili lilipitisha azimio la kumsamehe Esther Bulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi tukawa na *double standard* kwamba wametenda kosa siku moja, mmoja tunamuadhibu mmoja tunamsamehe. Wote wallombwa radhi ndiyo maana na sisi tumesema kama vile tulivyomsamehe Bulaya siku ile na huyu Nassari naye tumsamehe kwa sababu kwa Nassari hili ni kosa lake la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu karipio tulisema safari ile Esther Bulaya apewe karipio kali kwa sababu ilikuwa anajirudia, huyu ni kosa lake la kwanza ndiyo maana hatukupendekeza karipio kali. Ukishaweka karipio kali sasa unamfananisha Bulaya na Nassari ambao wote wameomba radhi, mwingine amerudia makosa, mwingine anafanya kwa mara ya kwanza, tukaona kwamba tuwatofautishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja ya Mheshimiwa Khadija, nadhani nimejibu kwamba Nassari apewe karipio kali hatukuona sababu. Kanuni zetu zinasema; kama mtu ni mkosaji mara ya kwanza, atapewa adhabu ya kutohudhuria vikao humu ndani visivyozidi siku tano, sisi tumeona siku tatu zinatosha. Hoja ya msingi hapa ndugu zangu ni kuwaambia wananchi wa Muleba kwamba Mbunge wenu kasingiziwa na kwa shughuli hii tunayoifanya leo nina uhakika tutakuwa tumempunguzia makali Mheshimiwa Tibaijuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma nadhani umenisaidia kumweleza mdogo wangu hapa Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga kwamba, kisaikolojia Mheshimiwa Tibaijuka alikuwa ameathirika. Kuhusiana na kwamba adhabu iongezwe, tunasema sisi kwa upande wetu tuliyoyapendekeza yale mimi kama Mwenyekiti wa Kamati

siwezi nikabadili jambo hapa ndiyo maana sisi tunalileta jambo mbele yenu, miljadili, mfanye maamuzi. Sisi tuliona na Kanuni zinasema kwa mtu anayefanya kosa kwa mara ya kwanza, adhabu ya kukosekana humu ndani isizidi siku tano. Tungeliweza kuchukua tano, tatu, mbili, nne, moja, sisi tumechangua tatu kwamba siku tatu kwa yule ambaye amefanya kosa la kwanza.

Ndugu yangu Mheshimiwa Bulembo nakushukuru kuunga mkono maoni ya Kamati japo kama umehitilafiana na adhabu lakini kama tulivyosema, huyu ni mara yake ya kwanza. Kuna mwingine alisema kwamba Nassari mzoefu, Nassari hii ni mara yake ya kwanza kuja kwenye Kamati kwa hiyo sisi kama Kamati tumechukulia kama ni kosa lake la kwanza. Kwa hiyo ndiyo maana tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Toufiq pia unaunga mkono, unasema Kanuni zifuatwe. Nataka nikuhakikishieni kabisa kabisa Kamati yetu sisi tuna wanasheria waliobobe, wanaoishauri Kamati na siku zote tunafanya mambo ndani ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja hizo, naomba uniruhusu sasa nisome azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Joshua Nassari kwa kuhusika na vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha 32 kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muunganio wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: ...za kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA Sheria, kanuni na uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkuchika kwa kuwa sasa ni kuhusu utaratibu maana yake tunachokifanya hapa tunavunja Kanuni anataka kutukumbusha Mheshimiwa Mbunge. Naomba ukae kiti cha karibu hapo Mheshimiwa Mbunge atuonyesha Kanuni inayovunjwa, Mheshimiwa Nkamia

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), Mheshimiwa Mkuchika hakunielewa nilichosema. Amekuja hapa anasema.....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia

MHE. JUMA S. NKAMIA: Samahani kidogo

NAIBU SPIKA: Ngoja nikueleze kidogo ili tuende sawa sawa. Utaratibu ni Kanuni ya 68(1) na inataka utaje Kanuni ambayo inavunjwa sasa. Sasa kama unasema 68(7) huo ni Mwongozo ambao huwezi kuomba mwingine akiwa anazungumza. Sasa wewe kwa sababu umeomba utaratibu na nimekukumbusha Kanuni ya 68(1) inataka utaje Kanuni inayovunjwa na Mheshimiwa Mkuchika

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mkubwa huwa hakosei, anaghafilika tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichosema mimi sijatetea mtu kama ambavyo Mheshimiwa Mkuchika anasema kwamba mimi nimekwenda kuwatetea. Angenisikiliza vizuri nimesema adhabu kali zichukuliwe kwa mujibu wa Kanuni, lakini wakati anajibu hoja amesema, Mheshimiwa Nkamia kama alivyosema lakini...

No mimi siku-side mtu hapa, nimesema adhabu kazi zichukuliwe ndicho hicho nilichokuwa nataka afanye marekebisho tu hapa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Nkamia. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa hizi Kanuni zetu sina cha kusema hapo kuhusu utaratibu kwa sababu hajaonesha Kanuni yoyote ambayo ilikuwa inavunjwa. Mheshimiwa Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge endelea

MHE. CAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA – MWENYEKITI KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama mdogo wangu Nkamia alinisikiliza vizuri, nimeandika maneno aliyoyasema hapa; hata ikiwa mara ya kwanza utasamehewa, sheria ichukue mkondo wake kuhusu Mheshimiwa Nassari, wala sijasema kama Nkamia kamwombea mtu radhi, amesema Sheria ichukue mkondo wake nimeandika hapa. Kwa hiyo usitie maneno mdomoni mwangu ambayo sikuyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza tena.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

NA KWA KUWA katika kikao cha 32 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 30 Mei, Bunge lilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya

Spika kwa kukaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa imepangwa iweze kuendelea;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mheshimiwa Joshua Nassari kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 12 Juni hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mheshimiwa Joshua Nassari na kumtia hatiani;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Nassari alitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote na alipohojwa na kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Nassari (Mb) alivunja kanuni ya 74(1)(a)na (b) na kifungu cha 26 cha Sheria ya Kinga, Madaraka ya Haki za Bunge, Sura ya 299 kwa kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA kwa kuzingatia kuwa Mheshimiwa Joshua Nassari hii ni mara yake ya kwanza kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau mamlaka ya Spika;

HIVYO BASI Bunge linaazimia Mheshimiwa Joshua Nassari Mbunge, kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kiungwana cha kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika kwa Bunge na kwa watu wengine wote aliyorakwaza kutokana na matendo yake;

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba linakubaliana na kuitisha mapendekezo kuhusu Mheshimiwa Joshua Nassari Mbunge kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

AZIMIO LA BUNGE KUHUSU HATUA ZA KUCHUKUA DHIDI YA MHE. JOSHUA NASSARI (MB) KWA KUHUSIKA NA VITENDO VYA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA KATIKA MKUTANO WA TATU, KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI KILICHOFANYIKA TAREHE 30 MEI, 2016 KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI

[Limetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge (The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, [CAP 296 R:E 2015].

KWA KUWA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA, Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Bunge zimeweka utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge, na kwamba kwa taratibu hizo Wabunge wanatakiwa kuheshimu Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa ujumla;

NA KWA KUWA, katika Kikao cha Thelathini na mbili cha Mkutano wa Tatu wa Bunge kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 Bunge ilikuwa likijadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017, Mhe. Joshua Nassari (Mb) alifanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika kwa kukaidi maelekezo ya Spika ya kumtaka atulie ili shughuli iliyokuwa imepangwa iweze kuendelea.

KWA KUWA, Mheshimiwa Spika kwa Mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mhe. Joshua Nassari (Mb) kwa makosa ya kudharau Mamlaka ya Spika

NA KWA KUWA, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 15 Juni, 2017 hapa Dodoma na kusikiliza shauri la Mhe. Joshua Nassari (Mb) na kumtia hatiani;

NA KWA KUWA, Mhe. Joshua Nassari (Mb) alitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu wa aina yoyote, na alipohojwa na Kamati alikiri wazi kosa lake na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika na Bunge;

NA KWA KUWA, Mhe. Joshua Nassari (Mb) alivunja Kanuni ya 74(1) (a) na (b) na Kifungu cha 26 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kwa kufanya vitendo vyatia kudharau Mamlaka ya Spika;

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kuwa Mhe. Joshua Nassari (Mb) hii ni mara ya kwanza kutiwa hatiani kwa kosa kama hili la kudharau Mamlaka ya Spika;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia:-

KUMSAMEHE Mhe. Joshua Nassari (Mb) kutokana na kitendo chake cha kuonesha ushirikiano kwa Kamati na pia kitendo chake cha kiungwana cha kuomba radhi kwa Mheshimiwa Spika, kwa Bunge na kwa watu wengine wote aliwakwaza kutokana na matendo yake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, linakubaliana na kupitisha mapendekezo kuhusu Mhe. Joshua Nassari (Mb) kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

19 Juni, 2017

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkuchika pengine ungemaliza maazimio na ya Mheshimiwa Conchesta, kwa sababu nimepata taarifa hapa ya Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Musukuma, ameleta hoja ya kubadilisha maazimio.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA
HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Naam!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkuchika inabidi urudie tena maazimio kuhusu Mheshimiwa Rwamlaza pia, kwa sababu yale uliyasoma pamoja na ile taarifa uliyoisema mwanzo.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA
HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wanasheria wanasesma yule ambae ametiwa hatiani na kutoa adhabu, tunatamka moja kwa moja. Kwa hiyo Rwamlaza tumemtia hatiani. Kanuni zinasema anayefanya kosa kwa mara ya kwanza anaadhibiwa kutokuingia Bungeni kwa siku zisizozidi tano, kwa hiyo kwa Rwamlaza, Kamati imependekeza apewe adhabu ya siku tatu.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu Bunge ndilo linaloamua, ninyi mmeleta mapendekezo, nyinyi mmeleta mapendekezo kwa hiyo Bunge ni lazima lihojiwe. La sivyo maana yake ninyi mmeshamaliza hiyo adhabu.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA - MWENYEKITI WA
HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siku zote tunapendekeza adhabu Bunge ndilo linaloamua. Kwa hiyo ile ya Rwamlaza si kama ni *final*, sisi kazi yetu tukimaliza hii kazi tunawasilisha kwa Spika, Spika analileta humu ndani, Bunge linafanya maamuzi. Kama mlivyofanya safari iliyopita, mlifanya maamuzi tofauti na tulivyopendekeza, uwezo huo mnao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nimeletewa taarifa ya Mheshimiwa

Mbunge mmoja anayetaka kutoa hoja ya kubadilisha Maazimio yaliyotolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Mheshimiwa Joshua Nassari na pia Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimeomba kutoa hoja chini ya Kanuni ya 57 1(a) 58(1) na 74 (3), Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, maazimio yaliyowasilishwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge yafanyiwe mabadiliko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio la Kamati kuhusu shauri la kudharau mamlaka ya Spika, linalomhusu Mheshimiwa Joshua Nassari libadilishwe kwa kufuta aya ya tisa na kuiandika upya kama ifuatavyo:-

KWA KUWA hili ni kosa lake la pili na kanuni ya 74 3(b) inatoa maelezo ya adhabu kwa Mbunge ambaye anafanya kosa la kudharau mamlaka ya Spika mara mbili au zaidi, Bunge liazimie kwamba Mheshimiwa Joshua Nassari asimamishwe kuhudhuria vikao 20 vya Bunge kuanzia tarehe 28 Julai na kuendelea hadi Mkutano ujao wa Bunge ili kukamilisha jumla ya vikao 20.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma naomba ukae, Mheshimiwa Peter Serukamba.

T A R I F A

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nimemsikia vizuri Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, amesema mara mbili hapa, kwamba Nassari ni

kosa lake la kwanza kufika kwenye Kamati ya Maadili. Sasa Mheshimiwa Msukuma anatuambia ni mara ya pili, sasa ni mara ya pili kwa maana kwa kamati ipi labda atupe *clarification*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma subiri kidogo. Mheshimiwa Peter sasa hapo umeuliza swalii. Nadhani ye ye amalize hoja yake, Bunge lifanye uamuizi. Hata hivyo, hili jambo kama si la pili, itabidi tujiridhishe hapa, wakati anaendelea kusoma ngoja nifuatilie na Makatibu hapa kama hili ni kosa la pili ama la kwanza. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, labda ndugu yangu Serukamba hajakumbuka, hata kosa la kuingia na chupa ya konyagi na lenyewe ni kosa ambalo lilitakiwa liainishwe hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Kamati Kuhusu Ushauri wa Kusema Uongo Bungeni linalomhusu Conchesta Rwamlaza, libadilishwe kwa kufuta aya ya saba (7) na 10 na kuliandika upya kama ifuatavyo:-

KWA KUWA hili ni kosa la kwanza na kanuni ya 74 (3)(a) inatoa maelekezo ya adhabu inayotakiwa kuchukuliwa, Bunge liazimie kwamba Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza asimamishwe kuhudhuria vikao 10 vya Bunge kuanzia tarehe 28 Juni na kuendelea hadi mkutano huo wa Bunge ili kukamilisha jumla ya vikao hivi 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye kanuni, Mheshimiwa Mkuchika alivyokuwa anasema, anasema kanuni inasema kutohudhuria vikao vitano, lakini kanuni hiyo ya 74(3) inaeleza ni vikao 10. Kwa hiyo, nilikuwa nalishawishi Bunge tuweze kujadili na kuweza kukubaliana na pendekeso langu hili nililolitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, lakini sasa nalazimika kutoa ufanuzi kidogo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, Kamati imeleta mapendekezo ili Bunge liweze kuamua kuhusu makosa yaliyofanywa na Mheshimiwa Joshua Nassari na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Mapendekezo ya adhabu ambayo Kamati imeleta, Mheshimiwa Joshua Nassari ni kwamba asemehewe kwa kuwa ni kosa lake la kwanza, lakini Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza pamoja na kwamba naye ni kosa lake la kwanza, lakini Kamati inapendekeza kuwa Bunge kutoa adhabu ya kutokuhudhuria vikao vitatu nya mkutano huu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Musukuma akizungumza, Mheshimiwa Peter Serukamba anasema azimio la marekebisho ya Azimio la Kamati ili Bunge liweze kuamua juu ya haya, imetaja kwamba Mheshimiwa Nassari amefanya hili ni kosa lake la pili. Mheshimiwa Peter Serukamba ametujulisha kwamba, Kamati imesema hili ni kosa la kwanza, lakini azimio la Mheshimiwa Musukuma linasema hili ni kosa la pili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni ya 74 inapohesabu makosa ya Mbunge, inahesabu makosa ambayo Mbunge alipelekwa kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Kwa hivyo kama Mbunge alifanya kosa ambalo hakupelekwa kwenye Kamati husika basi, Kamati itakuwa hajahesabu hilo kama ni kosa kwao.

Kwa hivyo ndiyo maana Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, imesema kosa hili la Mheshimiwa Nassari ni kosa la kwanza kwa sababu kwa Bunge hili la 11, Kamati hii inapofanya kazi Mheshimiwa Nassari amepelekwa katika Kamati hii kwa mara ya kwanza kwenye kosa hili, ambalo leo imeleta mapendekezo.

Sasa kwenye hoja ya Mheshimiwa Musukuma hapa, nilikuwa nimeuliza upande wa Katibu lakini siwezi kulipata hilo jibu sasa kuona kama kuna kosa ambalo liliifanyika, lakini Kamati imesahau, lakini sitaki kufikiri kwamba Kamati imesahau.

Sasa kwa sababu azimio la Mheshimiwa Musukuma linahusu wakosaji wote wawili, kwa maana ya kwamba Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye Kamati ilitaka asamehewe, Mheshimiwa Musukuma anasema hili ni kosa lake la pili, kwa hiyo kanuni ya 74(b) itumike, wakati azimio la kumhusu Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza anasema hili ni kosa lake la kwanza na kanuni ya 74(3)(a) iweze kutumika kwa maana ya kwamba asihudhurie. Yeye ametoa asimamishwe na asihudhurie vikao 10, japokuwa kanuni inasema visivyozidi, kwa hiyo maana yake ni 10 na kushuka chini.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hili azimio la pili naweza kulihoji Bunge, lakini sasa hili la kwanza napata shida kidogo, kuona kama ni kosa la pili ama kosa la kwanza. Kwa sababu hiyo, kwa sababu kwa utaratibu tulionao leo hili jambo lipo kwenye ratiba tuliyonayo sasa hivi na kama Bunge tutakiwa kuliamua, mimi nitazuia hili zoezi la kulihoji Bunge mpaka nipate taarifa kutoka kwa Katibu kama ni kosa la kwanza ama la pili ili Maazimio ya Bunge yaende sawa sawa. Kwa sababu mwisho wa haya natakiwa kulihoji bunge kama linakubaliana na Mheshimiwa Musukuma ama linakubaliana na mapendekezo ya Kamati. Kwa hivyo, nitasubiri taarifa kutoka kwenye meza ya Makatibu halafu nitatoa maelezo baadaye kidogo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba iliyopo, tutalirudia jambo hili kwenye maamuzi, kwa sababu mjadala tumeshafanya, kila jambo tumefanya, kwenye kuwahoji tutasubiri jambo hili nitaarifiwe na meza ya Makatibu halafu tutalirejea. Kwa hiyo tutaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu kwa sasa.

Katibu!

NDG.THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa
wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani
(International Labour Organization (ILO) –
Maritime Labour Convention, 2006)**

na

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa
Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa
Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani
(International Labour Organization (ILO)
Seafarers' Identity Documents
Convention (Revised 2003)]**

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, ili twende na muda vizuri, Mheshimiwa Waziri, atazungumza kuhusu Maazimio yote mawili na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati pia, yote mawili na atakapokuja Msemaji wa Upinzani pia atazungumza pia kuhusu Maazimio yote mawili, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuweka mezani Azimio la Bunge la Kuridhia Kkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), (The Maritime Labor Convention, 2006).

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambalo lina jukumu la kusimamia viwango vya kazi vya Kimataifa. Kupitia mapendekezo itifaki na mikataba inayopitishwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ILO. Katika

kikao cha 94 cha Mkutano Mkuu maalum wa *ILO* uliofanyika tarehe 23 Februari, 2006 Geneva Uswisi, Nchi Wanachama ikiwemo Tanzania, ilisaini na kuitisha mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*The Maritime Labour Convention, 2006*).

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuitishwa kwa mkataba huu yalitokana na uamuzi wa Nchi Wanachama wa *ILO* kuifanyia marekebisho mikataba 37 ya *ILO* inayohusu kazi za Ubaharia ili kuwa na mkataba mmoja ambao unahusisha viwango vya kazi vya Kimataifa vya Mabaharia kwa lengo la kukuza kazi za staha na kuboresha mazingira ya kazi ya Mabaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tanzania inazo sheria mbalimbali zinazosimamia masuala ya Mabaharia kwa pande zote mbili za Muungano ambazo hazikinzani na matakwa ya Mkataba wa *ILO* wa kazi za ubaharia wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania Bara sheria zinazosimamia masuala ya Mabaharia ya kazi za Mabaharia ni pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na. 6 ya Mwaka 2004; Sheria ya Taasisi za Kazi, Na. 7 ya Mwaka 2004; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Na. 5 ya Mwaka 2003; Sheria ya Usafiri wa Majini, Na. 9 ya Mwaka 2001; Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Na. 20 ya Mwaka 2008; Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Na. 8 ya Mwaka 2008; na Sheria Mbalimbali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa upande wa Zanzibar, sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ajira, Na. 11 ya Mwaka 2005; Sheria ya Mahusiano Kazini, Na. 1 ya Mwaka 2005; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Na. 8 ya Mwaka 2005; Sheria ya Usafiri Baharini, Na. 5 ya Mwaka 2006; na Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi, Na. 5 ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Mkataba huu ni uamuzi wa nchi wanachama wa Shirika la Kazi la

Kimataifa, kuifanyia marejeo mikataba 37 ya *ILO* inayohusu kazi za ubaharia ili kuwa na mkataba mmoja unaokidhi mahitaji ya kukuza kazi za staha kwa mabaharia. Kulingana na uamuzi huo, nchi wanachama wanapaswa kusaini na kuridhia mkataba huo kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 14 ya mkataba. Chimbuko pia linatokana na Mkataba wenyewe unaopendekeza nchi wanachama kuridhia kwa mujibu wa katiba za nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipengele muhimu vya mkataba huu ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya kwanza inazitaka nchi wanachama zitakazoridhia mkataba huu kuhakikisha uwepo wa kazi za staha kwa mabaharia. Pia inatoa wajibu wa kila nchi mwanachama, kushirikiana na nchi nyingine katika utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya pili inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali ikiwemo mamlaka yenyе dhamana ya kusimamia masuala ya mabaharia, mkataba wa kazi za ubaharia na masharti yake kati ya baharia na mmiliki wa meli, taratibu za ajira kwa mabaharia na neno baharia ambalo linatafsiriwa kuwa ni mtu ye yeyote aliyejiriwa au anayefanya kazi katika nafasi yoyote kwenye meli ambayo si ya kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tatu inazitaka nchi wanachama kuzingatia haki za msingi kwa kazi za ubaharia, haki hizo ni pamoja na kuondoa utumikishwaji wa mtoto, kutokomeza kazi za shuruti, uhuru wa kuijunga na vyama vya wafanyakazi, kuondoa ubaguzi na pia kuzingatia usawa katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne, pamoja na mambo mengine inaanisha haki za ajira ambazo ni masharti stahiki ya mikataba ya ajira, afya na usalama mahala pa kazi. Hifadhi ya jamii na huduma za matibabu. Aidha, haki za kijamii zinazoainishwa ni pamoja na mazingira yenyе staha ya kuishi melini na huduma za chakula pamoja na malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano, ambayo pamoja na mambo mbengine, inabainisha wajibu wa nchi wanachama katika kusimamia na kutekeleza sheria na kanuni zinazohusiana na meli na mabaharia. Vile vile inazitaka nchi wanachama kuimarisha usimamizi wa meli zinazotumia bendera zao kwa kuanzisha mfumo wa utekelezaji wa mkataba ikiwemo kufanya kaguzi za mara kwa mara ili kuhakikisha matumizi sahihi ya bendera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya sita, inaaishwa mwongozo wa kanuni za utekelezaji wa mkataba, ambazo zinajumlisha maeneo makuu matano, ambayo ni pamoja na sifa za msingi za baharia kuajiriwa kwenye meli, masharti ya ajira, makazi huduma za burudani na chakula, huduma za afya, matibabu, ustawi wa hifadhi ya jamii na usimamizi wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba inafafanua utaratibu kuwa, mkataba utaanza kutumika miezi sita baada ya nchi kuridhia na kuwasilisha hati za kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ya nane na ibara ya tisa inaeleza utaratibu kuwa, nchi iliyoridhia mkataba inaweza kujitoa kwenye mkataba baada ya miaka 10 tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa nchi husika iliyoridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za *ILO* hadi kufikia June, 2017, jumla ya nchi wanachama 91 kati ya nchi 187 zilikuwa zimesharidhia mkataba huu, zikiwemo nchi 15 kutoka Bara la Afrika ambazo ni Benin, Congo, Gabon, Ghana, Kenya, Liberia, Mauritius, Morocco, Nigeria, Algeria, Schelles, Cape Verde, Afrika Kusini, Togo na Tunisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya Tanzania kuridhia mkataba huu ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za ajira kwa mabaharia wa Kitanzania katika meli za ndani naza nje ya nchi; na hivyo kuchangia katika kupunguza

umaskini wa kipato. Kupata fursa za mafunzo na utalaam katika tasnia ya ubaharia na mabaharia, kuwezesha nchi yetu kutekeleza viwango vya kimataifa vya kazi za staha kwa mabaharia, ambayo itachangia kuongezeka tija katika kazi za ubaharia na kukuza mahusiano baina ya nchi yetu na nchi wanachama zilizoridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*the Maritime Labour Convention*) ya mwaka 2006 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*):

NA KWA KUWA kikao cha 94 cha Mkutano Mkuu Maalum wa *ILO* uliofanyika tarehe 23 Februari mwaka 2006 *Geneva Uswiss* uliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Baharia wa Shirika la Kazi Duniani (*the Maritime Labour Convention*) ya Mwaka 2006;

NA KWA KUWA Tanzania ni mjambe na ilishiriki katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*the Maritime Labour Convention*) ya Mwaka 2006;

NA KWA KUWA nchi wanachama wa *ILO* ilifanya marejeo ya mikataba 37 ya *ILO* inayohusu kazi za ubaharia ili kuwa na mkataba mmoja ambao unahusisha viwango vya kazi vya Kimataifa vya mabaharia kwa malengo ya kuhimiza na kukuza kazi za staa na kusimamia viwango vya kazi Kimataifa;

NA KWA KUWA mkataba huu unalenga kukuza kazi za staha kwa mabahari, kuondoa utumikishwaji wa watoto, kutokomeza kazi za shuruti, kuwepo na uhuru wa kujinga na vyama vya wafanyakazi, kuondoa ubaguzi pia kuzingatia usawa katika ajira;

NA KWA KUWA Ibara ya VIII ya mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuridhia na kuwasilisha hati kwa Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*;

NA KWA KUWA Tanzania kwa kuridhia mkataba huu itanufanika na mambo ya fuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa mabaharia wa Kitanzania katika meli za ndani na za nje ya nchi na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini wa kipato;

(ii) Kupata fursa za mafunzo na utalaam katika tasnia ya ubaharia na mabaharia;

(iii) Kuwezesha nchi yetu kutekeleza viwango vya Kimataifa vya kazi za staa kwa mabaharia wetu, ambayo itachangia kuongeza tija katika kazi za ubaharia; na

(iv) Kukuza mahusiano baina ya nchi yetu na nchi wanachama zilizoridhia mkataba huu;

NA KWA KUWA uchambuzi wa kina uliofanyika umebaini kuwa mkataba wa Kimataifa wa kazi za ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani yaani *the Maritime Labour Convention* haukinzani na Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala masuala ya kazi za mabaharia nchini bali uchambuzi umebaini kuongezeka kwa fursa za kazi kwa mabaharia wa Tanzania.

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya mkataba huu kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Saba kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*the Maritime Labour Convention*) ya Mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hoja zote mbili nizitoe kwa pamoja; kwa kuzingatia maelezo yako naomba niendelee na mkataba wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuweka tena mbele ya meza yako Tukufu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani [*the ILO Seafarers Identity Documents Convention (revised)*] ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambalo lina jukumu la kusimamia viwango vya kazi vya kimataifa kupitia mapendekezo, itifaki, mikataba inayopitishwa na mukutano mkuu wa mwaka (ILO).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha 91 cha Mkutano Mkuu wa *ILO* kilichofanyika tarehe 3 Juni, 2003 Geneva Uswis nchi wanachama ikiwemo Tanzania zilisaini na kupitisha mkataba wa Kimataifa wa vitambulisho vya mabaharia namba 185 wa mwaka 2003 [*the Seafarers Identity Documents Conversion (revised)*] ya Mwaka 2003 Na.185.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu ulipitishwa kwa lengo la kurekebisha na kuhusisha Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 108 wa Mwaka 1958. Kulingana na mkataba huu vitambulisho vya mabaharia si hati za kuruhusu mabaharia kuishi kwenye nchi husika bali ni hati ya kumruhusu baharia huyo wakati meli imetia nanga kutoka kwenda nchi kavu kujipatia mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kupitisha kwa Mkataba Na. 185 ni kuweka viwango vya kazi vya Kimataifa ili kulinda maslahi na usalama wa baharia, abiria na meli na kuwawezesha mabaharia kuingia katika nchi kupitnia nchi moja kwenda nchi nyingine wakiwa melini au wanaporudishwa kwenye nchi zao. Pia mkataba unazingatia Azimio la Umoja wa Mataifa linalohusu ulinzi wa haki za binadamu na mapambano dhidi ya ughaidi, uharamia na vitisho vya usalama baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mkataba huu unatambua mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Bahari

Duniani (*International Maritime Organization*) inayohusu huduma za kibahari ulinzi na usalama wa meli na kuzuia uchafuzi wa bahari kutokana na taka toka melini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini upo mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia masuala ya mabaharia kwa pande zote mbili za Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara ipo Sheria ya Usafiri wa Majini, namba 9 ya mwaka 2001 ambayo ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Tanzania Zanzibar ipo Sheria ya Usafiri Baharini, Na. 5 ya Mwaka 2006 ambayo pia ilianzisha mamlaka ya usafiri baharini (*SMA*). Sheria hizo hazikinzani na matakwa ya mkataba huu. Hata hivyo Tanzania haina vitambulisho vinavyotolewa kwa mabaharia wa Kitanzania kwa kuzingatia mkataba huu bali mabaharia hutumia hati za kusafiria pamoja na kitabu cha kutunza kumbukumbu za wafanyakazi melini.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la mkataba huu ni uamuji wa nchi wanachama wa Shirika la Kazi la Kimataifa (*ILO*) kuufanya marejeo mkataba namba 108 wa mwaka 1958 uliobainika kutokidhi mahitaji ya utambuzi na haki za mabaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipengele muhimu vyta mkataba huu ni pamoja na Ibara namba moja, inayotoa tafsiri ya wigo (*scope*) pamoja na mambo mengine; ambayo inatoa tafsiri ya neno baharia kuwa ni mtu yoyote aliyeajiriwa au anayefanya kazi katika nafasi yoyote kwenye meli isipokuwa meli za kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya pili inaelezea wajibu wa nchi wanachama kutoa vitambulisho kwa mabaharia ambaeo ni raia wake kwa kuzingatia matakwa ya mkataba. Aidha, Ibara hii inaelekeza kuwa masharti ya vigezo ya utoaji wa hati za kusafiria yatatumika pia kwa vitambulisho vyta mabaharia kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za nchi husika.

Ibara ya tatu pamoja na mambo mengine inaainisha taarifa muhimu na aina za malighafi zitakazotumika kutengeneza vitambulisho vya mabaharia. Aidha, ibara hii inabainisha taarifa muhimu zinazopaswa kuwemo kwenye kitambulisho kuwa ni pamoja na jina la baharia, jinsi, tarehe na sehemu aliyozaliwa; picha, saini na alama nyingine muhimu za utambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vitambulisho vya baharia vinapaswa kutengenezwa katika mfumo rahisi unaosomeka kielektroniki usioweza kughushiwa na kwa kutumia malighafi isiyoharibika krahisi katika mazingira ya bahari. Hali kadhalika ibara hii inaelekeza kuwa muda wa matumizi wa vitambulisho vya mabaharia utazingatia sheria na kanuni za nchi husika ambapo kulingana na mkataba huu muda wa matumizi ya vitambulisho hautazidi miaka 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne; pamoja na mambo mengine inaelekeza wajibu wa nchi wanachama kuanzisha na kusimamia *kanzidata* ya kutunza kumbukumbu za vitambulisho vya mabaharia vinavyotolewa kusitishwa au kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tano pamoja na mambo mengineyo inabainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa na nchi wanachama katika utengenezaji, utoaji na utunzaji wa vitambulisho vya mabaharia ili kulinda ubora na usalama wa vitambulisho. Aidha, inazitaka nchi wanachama kuanda vitambulisho katika muundo rahisi utakaohimili mazingira ya baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kila nchi mwanachama inapaswa kuwa na kituo cha maulizo chini ya mamlaka inayohusika na ajira za mabaharia kwa lengo la kuhakiki vitambulisho vya ubaharia vilivyotolewa na nchi mwanachama. Pia Ibara hii inatoa utaratibu wa kutoa vitambulisho ambao utazingatia sheria, Miongozo na taratibu za nchi husika katika kutoa hati za kusafiria nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya sita inaainisha hatua na taratibu za kuzingatiwa na nchi mwanachama katika kuruhusu mabaharia wenye vitambulisho halali kuingia na kutoka nchini kwa lengo la kuwawezesha kujipatia ya msingi au kupita kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba inaelekeza kuwa kitambulisho kitakachotolewa kwa baharia kitaendelea kuwa mali ya baharia isipokuwa tu kwa ridhaa yake kama ataamua kitunzwe na kiongozi wa meli. Aidha, baharia anaweza kunyang'anywa na kufutiwa umiliki wa kitambulisho alichopewa endapo atashindwa kutimiza vigezo na masharti yalijowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 inafafanua utaratibu kuwa mkataba utaanza kutumika miezi sita baada ya nchi kuridhia na kuwasilisha hati za kuridhia kwa Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 inaelezea utaratibu kuwa nchi iliyoridhia mkataba inaweza kujitoa kwenye mkataba baada ya miaka 10 tangu tarehe ya kuanza kutumika kwa nchi husika iliyoridhia.

Kwa mujibu wa takwimu za *ILO* hadi kufikia Juni, 2017 nchi wanachama 35 kati ya nchi wanachama 187 zilikuwa zimeridhia mkataba huu. Zikiwemo nchi nne kutoka Bara la Afrika ambazo ni Congo, Madagascar, Nigeria na Tunisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya Tanzania kuridhia mkataba huu ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za ajira kwa Mabaharia wa Kitanzania katika meli za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini wa kipato, kuongezeka kwa fursa za kiuchumi na ujasiriamali pembezoni mwa bahari na maeneo mengine, kupata fursa za mafunzo na utalaam katika tasnia ya ubaharia na mabaharia kutoka nchi wanachama; na kuwepo kwa mfumo madhubuti wa utambuzi wa mabaharia na hivyo kuimarisha usalama wa nchi na mabaharia wa Kitanzania wanaofanya kazi kwenye meli za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani yaani *IMO*;

NA KWA KUWA katika kikao cha 91 cha mkutano mkuu wa *IMO* kilichofanyika tarehe 3 Juni, 2003 Geneva Uswisi nchi wanachama zilisaini na kupitisha Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa mwaka 2003 (*The Seafarers Identity Document Convention (Revised)* ya mwaka 2003 Na. 185;

NA KWA KUWA Tanzania ni mjumbe na ilishiriki katika majadiliano yaliyowezesha kusainiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa mwaka 2003.

NA KWA KUWA malengo ya *IMO*ni kuhimiza na kukuza kazi za staa na kusimamia viwango vya kazi vya Kimataifa;

NA KWA KUWA mkataba huu unalenga kuweka viwango vya kazi vya Kimataifa ili kulinda maslahi na usalama wa mabaharia, abiria, meli na kuwawezesha mabaharia kuingia katika nchi kupitia nchi moja kwenda nchi nyingine wakiwa melini au wanaporudishwa kwenye nchi zao;

NA KWA KUWA mkataba huu unazingatia azimio la Umoja wa Mataifa linalohusu ulinzi wa haki za binadamu na mapambano dhidi ya ugaidi, uharamia na vitisho vya usalama baharini;

NA KWA KUWA mkataba huu unatambua mikataba ya Kimataifa ya Shirika la Bahari *Duniani* (*International Maritime Organization*) inayohusu huduma za kibahari na usalama baharini;

NA KWA KUWA Ibara ya 11 ya mkataba huo inazitaka nchi wanachama kuridhia na kuwasilisha hati kwa Mkurugenzi Mkuu wa *ILO*;

NA KWA KUWA Tanzania kwa kuridhia mkataba huu itanufaika na mambo yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa mabaharia wa kitanzania katika meli za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini wa kipato;

(ii) Kuongezeka kwa fursa za kiuchumi na ujasiliamali pembezoni mwa bahari na maeneo mengine;

(iii) Kupata fursa za mafunzo na utalaam katika tasnia ya ubaharia na mabaharia kutoka nchi wanachama;

(iv) Kuwepo na ulinzi wa haki za binadamu kwa mabaharia, mapambano dhidi ya ugaidi, ugharamia, vitisho vya usalama baharini; na

(v) Kuwepo kwa mfumo madhubuti wa utambuzi wa mabaharia na hivyo kuimarisha usalama wa nchi na mabaharia wa Kitanzania wanaofanya kazi kwenye meli za nje;

NA KWA KUWA uchambuzi wa kina uliofanywa umebaini kuwa Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 haukinzani na sheria, kanuni na taratibu zinazotawala masuala ya vitambulisho vya Mabaharia;

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya mkataba huu kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) Kifungu (e) cha Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho

vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 [*Seafarers Identity Document Convention (revised) 2003*] ya Mwaka 2003 Na. 185.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kutoa hoja kwa mikataba yote miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa hoja imeungwa mkuu lakini nitawahoji badaye kidogo tukimaliza utaratibu wetu.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amewasilisha taarifa yetu imegawanyika katika sehemu mbili na sehemu ya kwanza ina kurasa 25 ambayo nitasoma mimi na sehemu ya pili itasomwa na Mheshimiwa Hongoli, Mbunge wa Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari mwaka 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani (*Intenation Labour Organization ILO, Seafarers Identity Documents Convention Revised 2003*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari mwaka 2016 inazipa kamati za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inayoisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63 (3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane Kifungu cha 6(2) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari Mwaka 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inasimamia Wizara tatu ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 uliwasilishwa mbele ya Kamati yangu tarehe 30 mwezi Mei, 2017 na Waziri wa nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari Mwaka 2016, Kamati ilipokea maoni ya wataalam waliobobe katika masuala ya bahari na ubaharia na hivyo kujenga uwezo katika kuelewa maudhui ya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam waliosaidia kamati katika uchumbuzi huu nikiwataja kwa uchache, wa kwanza ni Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (*Dar es salaam Maritime Institute*), Chama cha Wanasheria wa Masuala ya Bahari (*Tanzania Maritime Law Association*), Wakala wa Mabaharia Zanzibar (*Zanzibar Maritme Authority*), Shirika la

Kazi Duniani (*International Labour Organization*), Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Idara ya Mikataba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 mwezi Juni, mwaka 2017, Ofisi ya Bunge kuitia mradi wa Shirika la Maendleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) wa Kuwajengea Uwezo Wabunge (*Legislative Support Program*) iliwezesha Kamati kupata uelewa kuhusu kanuni za misingi za kisheria za kimataifa katika kuridhia mikataba ya namna hii na utaratibu wa kikatiba na kisheria wa Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Uelewa huu ulisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo ya Msingi Yaliyozingatiwa na Kamati. Ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) ya Katiba, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanya kazi hoja ya Serikali iliyo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitazama matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria mbalimbali zinazohusiana na kazi, ajira na haki za binadamu, uzoefu wa nchi nyininge pamoja na kutazama faida na hasara za mikataba husika kwa ujumla wake. Kamati pia ilijiridhisha na matakwa ya kisheria za kimataifa kuhusu uridhishaji wa mikataba iliyowekwa katika Mkataba wa Vienna wa mwaka 1969 yaani *Vienna Convention of Law Treats* 1969.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele yake, Kamati ilifanya utafiti wa kutosha kuitia vyanzo mbalimbali ili kujiridhisha kuhusu mataifa yaliyosaini mkataba huu mwanzoni yaliyojiunga baadaye na yale ambayo tayari yamesharidhia. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha kuhusu misimamo ya Mataifa mbalimbali juu ya maudhui ya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitaka kujiridhisha kuhusu nafasi ya Tanzania katika diplomasia na uhusiano na Mataifa mengine kutokana na hatua ya kuridhia au kutoridhia mkataba huu hasa katika kipindi hiki ambacho Jumuiya ya Kimataifa inachukua jitihada za kutosha kuzuia mianya yote inayotishia usalama wa dunia hasa masuala ya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*). Jukumu la shirika hili ni kusimamia viwango vya kazi vya Kimataifa, kupitia mapendekezo itifaki, na mikataba mbalimbali inayopitishwa na Mkutano Mkuu wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha 91 cha Mkutano Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani kilichofanyika tarehe 3 Juni, 2003, Geneva Uswisi Nchi Wanachama ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilisaini na kupitisha mkataba huu kwa lengo la kuhakikisha kuwa Mabaharia wanajasiriwa na kutambulika kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko, madhumuni na faida ya mkataba wa vitambulisho Mabahari; chimbuko la mkataba wa vitambulisho mabahari mchakato wa vitambulisho wa Kimataifa wa Mabaharia, ulianzishwa na Shirika la Kimataifa la Wasafirishaji, (*International Workers Federation*) mwaka 1954. Shirika hili lilipendekeza kuanzishwa kwa utambulisho wa pamoja wa Kimataifa wa Mabahari, *International Identity Document for Seafarers'* chini ya usimamizi wa Shirika la kazi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya mkataba wa vitambulisho vya Mabaharia; dhunumi la kusaini mkataba namba 185 wa mwaka 2003 ni kuweka usawa katika viwango vya kazi Kimataifa kwa kutumia vitambulisho maalum vya Mabahari pamoja na kuimarisha usalama wa meli, abiria na Mabaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia vitambulisho vilivyopendekezwa kwenye mkataba huu, Mabaharia wataweza kuingia au kupitia katika nchi moja, kwenda nchi nyine wakiwa melini au kurudi kwenye nchi zao kwani watakuwa wanatambulika kirahisi. Ikilinganishwa na wakati wa sasa ambapo hawatambuliki Kimataifa hivyo kusababisha utendaji wao wa kazi kuwa mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu ni muhimu sana kwani utawezesha Mabahari wote duniani kuwa na usawa katika maslahi yao ya kikazi, kupata stahiki mbalimbali, kwa usawa pamoja na kuwawezesha kupata huduma mbalimbali za msingi katika nchi mbalimbali wanazopita na hivyo kuweza kuishi katika mazingira mazuri zaidi ya kikazi wanapokuwa safarini, yaani melini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Mabaharia vitaweka utambulisho wa pamoja na wa Kimataifa wa Mabaharia *International Identity*, vitambulisho hivyo vitarahisisha mambo mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya kibaharia, kwa mfano vitawarahisishia Mabaharia kupata huduma muhimu na za msingi katika nchi za kigeni wanazopita kama vile matibabu, mapumziko ya muda ya nchi kavu katika nchi za kigeni na kupata mahitaji yao ya msingi ikiwa ni pamoja na burudani. Hata hivyo, vitambulisho hivi havitakuwa mbadala wa *pass* za kusafiria bali itatumika sambamba na *pass* zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Mabaharia vilevile vina umuhimu katika suala zima la usalama wa nchi wanachama wa dunia kwa ujumla, ikikumbukwa kuwa tukio la shambulio la kigaidi nchini Marekani, linalojulikana kama Septemba, 11 mwaka 2001 ni tukio lilioshtua Mataifa mengi duniani na kuanza kuchukua hatua mbalimbali za kiusalama ikiwa ni pamoja na kuzuia Mabaharia kuingia katika nchi zao katika kuhakikisha kuwa nchi zao haziingiliwi na Magaidi kwa kutumia mgongo wa Mabaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugaidi nchini Marekani vile vile lilikumbusha dunia kuhusu tukio la utekaji wa meli nchini Italia na *Ms Achilli Lauro* ambalo ilitekwa na Mabahari wa Maharamia wa Kipalestina tarehe 7 Oktoba, 1985.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na matukio haya mawili ya kigaidi pamoja na mengine, Jumuiya za Kimataifa, zilliona umuhimu wa kuchukua tahadhali dhidi ya ugaidi kwene y meli na hivyo Shirika la Kazi Duniani lilionna umuhimu wa kuandaa mkataba mpya wa mwaka 2003 kwa kuzielekeza Nchi Wanachama kuanzisha utaratibu wa vitambulisho maalum vya Mabaharia (*Biometric based personal identification*) ili kudhibiti suala hili la ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu unaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhia, ni mwendelezo wa utaratibu ulioanza miaka mingi iliyopita ambao ulihitaji kufanyika kwa jithihad za kutosha katika kushawishi Nchi Wanachama kuukubali na hatimaye kuuridhia. Mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 9 Februari, 2005, nchi yetu imechelewa sana kuuridhia mkataba huu kwani hadi sasa ni takribani miaka 12 imepita toka mkataba huu ulipoanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu unatambua uwepo wa mikataba mingine ya Kimataifa, Shirika la Bahari Duniani yaani *International Maritime Organisation* inayohusu huduma za bandari pamoja na usalama baharini. Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Kazi Duniani, hadi kufikia mwezi Disemba, 2016 Nchi Wanachama 34 zilikuwa zimesharidhia mkataba huu ikiwemo Nchi za Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Madagascar, Nigeria pamoja na Tunisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa masuala ya Mabaharia nchini; masuala ya Mabaharia kwa upande wa Tanzania Bara yanaratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, yaani *SUMATRA*, pamoja na Sheria ya Usafiri Majini namba 21 ya mwaka 2003. Kwa upande wa

Tanzania Zanzibar unaratibiwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar yaani Zanzibar *Maritime Authority*pamoja na Sheria za Usafiri Baharini Sheria Na. 5 ya Mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria na Kanuni zinazotumika wakati huu nchini hazikinzani na matakwa ya mkataba huu, bali zinahitaji kuhuishwa ili kuweza kutumika kwa pamoja na kuwezesha kutolewa kwa vitambulisho hivi na kuwezesha Mabaharia wote waweze kutambulika Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiutaratibu nchi yetu haina vitambulisho kulingana na matakwa ya Mkataba huu, bali Mabaharia hutumia hati za kusafiria *passport* pamoja na kitabu cha kutunza kumbukumbu za wafanyakazi melini kama utambulisho wao. Pamoja na kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wadau, Kamati ilianza kazi ya kipitia, kuchambua maudhui yaliyomo katika mkataba huu, Ibara kwa Ibara kama inavyoonekana katika sehemu inayofuata katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya mkataba wa vitambulisho wa Mabaharia; Ibara ya kwanza ya mkataba huu, wanatoa tafsiri ya neno Baharia, kuwa ni mtu ye yeyote aliyeajiriwa au anayejihuisha, au anayefanya kazi yoyote kwenye meli, lakini haihusishi wale waliomo katika meli za kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hii inaendelea kufafanua kuwa endapo hoja itajitokeza kuwa ni watu gani wanaweza kuingizwa kwenye tafsiri ya neno Baharia, kama ilivyotafsiriwa katika mkataba huu, basi hoja hiyo itaamuliwa na chombo chenye mamlaka cha nchi husika, ambapo mtu huyo ana uraia yaani *Nationality* au hata hati ya kudumu ya kuishi *Permanent Resident* pamoja na kuwasiliana na mmiliki wa meli pamoja na Chama cha Mabaharia kutoka nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya pili ya mkataba inaeleza Nchi Wanachama kutoa vitambulisho kwa

Mabaharia ambapo ni raia katika nchi zao kwa kuzingatia maelezo yaliyomo kwenye Ibara ya tatu ya mkataba huu. Aidha, Ibara hii inasisitiza kuwa Sheria, Kanuni, au Taratibu zillizotumika kwenye nchi husika za utoaji *passza* kusafiria ndiyo hizo hizo zitakazotumika katika utoaji vitambulisho vya Kimataifa vya Mabaharia. Vilevile Ibara hii, inazihusu Nchi Wanachama kutoa vitambulisho vya Kimataifa vya Mabaharia, kwa Mabaharia wanaotoka nchi zingine ambapo wamepata hati za kudumu za makazi katika nchi zao (*Permanent Resident Permits*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya tatu inaainisha muundo na muda wa matumizi ya vitambulisho vya Mabahari, vile vile Ibara hii inaweka vigezo vya taarifa muhimu zinazopaswa kuwepo katika vitambulisho, ikiwa ni pamoja na Jina la Baharia, Jinsia, tarehe na sehemu ya kuzaliwa, picha, saini na alama nyingine za utambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mkataba huu, vitambulisho vya Mabaharia vinapaswa kutengenezwa katika Mfumo rahisi unaosomeka kielektroniki, usioweza kughushiwa na kutumia mali ghafi isiyoharibika kira hisi katika mazingira ya bahari. Muda wa matumizi ya Vitambulisho hivi utazingatia Sheria na Kanuni za nchi husika ambapo kulingana na Mkataba huu matumizi yake hayatazidi miaka kumi (10).

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya nne inaweka wajibu kwa Nchi Wanachama kuanzisha na kusimamia Kanzidata (*Database*) ya kutunza kumbukumbu za vitambulisho vinavyotolewa, kusitishwa au kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Ibara ya tano inaelekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Nchi Wanachama katika uzalishaji, utoaji na utunzaji wa vitambulisho ili kulinda ubora na usalama wa vitambulisho husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya sita inaainisha hatua na taratibu za kuzingatiwa na Nchi Wanachama katika

kuruhusu Mabaharia wenye vitambulisho halali vya Kimataifa kuingia na kutoka katika nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya saba inaweka vigezo na masharti ya umiliki na ufutaji wa vitambulisho. Katika Ibara hii inaelekezwa kuwa, kitambulisho kitakachotolewa kwa Baharia kitaendelea kuwa mali ya Baharia na kutunzwa na Baharia mwenyewe isipokuwa tu, kwa ridhaa yake, kama ataamua, kitatunzwa na Kiongozi wa Meli (*Master*) kwa ajili ya usalama. Aidha, Baharia anaweza kunyang'anywa na kufutiwa umiliki wa kitambulisho alichopewa endapo hatakuwa tena na vigezo vya kumwezesha kupata kitambulisho hicho kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Faida ya Kuridhia Mkataba huu; endapo Mkataba huu utaridhiwa, nchi yetu itapata faida nyingi kama ambavyo nimeziorodhesha hapa chini:-

(i) Kuongezeka na kukua kwa fursa za ajira kwa Mabaharia wa Kitanzania katika meli za ndani za Kimataifa na hivyo kupunguza umaskini wa kipato na kuchangia ukuaji wa uchumi na pato la Taifa kwa ujumla;

(ii) Kuongezeka kwa fursa za kiuchumi kwa Wajasiriamali waliopo pembezoni mwa Bahari na maeneo mengine;

(iii) Kuwepo kwa vitambulisho vya Mabaharia vyenye viwango vya Kimataifa;

(iv) Kuimarika kwa Mfumo wa Kisheria na Kitaasisi wa kusimamia masuala ya Mabaharia;

(v) Kuwepo na Mfumo wa utambuzi wa Mabaharia wa Tanzania na wa nchi za nje na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu na dunia nzima dhidi ya ugaidi;

(vi) Kuweza kubadilishana uzoefu na ujuzi kuhusu masuala ya Mabaharia;

(vii) Kuwezesha kufanyika kwa biashara za Kimataifa kwa kutumia meli kwa urahisi kwani kutakuwa hakuna haja ya kuwa na *visa* kwa Mabaharia;

(viii) Kuwezesha Mabaharia kuwa na uhuru na urahisi katika kutenda majukumu yake na nchi mbalimbali bila kuwa na vikwazo;

(ix) Kuwapunguzia Mabaharia usumbufu katika utaratibu wa kupata *visa* kwa ajili ya kuingia katika nchi wanazosafiri; na

(x) Kuwawezesha Mabaharia kupata haki zao za msingi za kibinadamu kama kupata mapumziko, burudani, huduma muhimu kama matibabu na kupata mahitaji mbalimbali ya msingi katika nchi za kigeni;

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhara ya Kutoridhia Mkataba huu; endapo Mkataba huu hautaridhiwa, nchi yetu itapata madhara yafuatayo:-

(i) Mabaharia wa nchi yetu kukosa utambulisho wa Kimataifa na hivyo kukosa haki zao za kimsingi za kisheria wakati wa utendaji wao wa kazi katika meli za kigeni;

(ii) Mabaharia wetu wapatao hamsini elfu (50,000) wako kwenye mazingira hatarishi ya kupoteza ajira zao katika meli pamoja na za Kimataifa zikiwemo meli ambazo zinapeperusha Bendera ya Tanzania na hivyo kuathiri mapato yao;

(iii) Nchi yetu kukosa mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na malipo ya Mabaharia hao wanapokuwa kazini kwenye meli za kigeni;

(iv) Kupunguza kwa fursa za Mabaharia wetu kupata uzoefu wa Kimataifa katika meli nyingine;

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti kengele imegonga, una mikataba miwili ya kuiwasilisha, nadhani bado uko kwenye mkataba wa kwanza kwa hiyo naomba uzingatie hilo kwamba kengele ya kwanza imeshagonga kuhusu mkataba wa kwanza.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maoni yote ambayo nimeyatoa katika mkataba huu wa kwanza, basi yaiingie kwenye *Hansard* yetu, yale ambayo sijayasoma na yale mengine ambayo nimekwishayasoma. Naomba sasa mwenzangu asome mkataba wa pili. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA VITAMBULISHO VYA MABAHARIA NA. 185 WA MWAKA 2003 WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (*SEAFARER'S IDENTITY DOCUMENTS CONVENTION (REVISED), 2003*) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho Vya Mabaharia Namba 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation (ILO) Seafarers' Identity Documents Convention (Revised)*, 2003).

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria

na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane Kifungu cha 6 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inasimamia Wizara tatu ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Namba 185 wa Mwaka 2003, uliwasilishwa mbele ya Kamati yangu tarehe 30 Mei, 2017 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama, Mb.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilipokea Maoni ya Wataalamu waliobobea katika masuala ya Bahari na Ubaharia na hivyo kujenga uwezo katika kuelewa maudhui ya Mkataba huu. Wataalamu walioisaidia Kamati Katika uchambuzi huu nikiwatataja kwa uchache ni pamoja na:-

- (i) Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (*Dar es Salaam Maritime Institute*);
- (ii) Chama cha Wanasheria wa Masuala ya Bahari (*Tanzania Maritime Law Association*);
- (iii) Wakala wa Mabaharia Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*); na
- (iv) Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*).
- (v) Shule ya Sheria, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

(vi) Idara ya Mikataba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia mradi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuwajengea uwezo wabunge (*Legislative Support Programme- LSP*) iliwezesha Kamati kupata uelewa kuhusu Kanuni za misingi za Sheria za Kimataifa katika kuridhia mikataba ya namna hii na utaratibu wa Kikatiba na Kisheria wa Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Uelewa huu ulisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri kuifanyia kazi hoja hii.

1.1 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani. Kamati ilitazamwa matakwa ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria mbalimbali zinazohusiana na Kazi, Ajira na Haki za Binadamu, Uzoefu wa nchi nyingine pamoja na kutazama faida na hasara za Mkataba husika kwa ujumla wake. Kamati pia ilijiridhisha na matakwa ya Sheria za Kimataifa kuhusu uridhiaji wa Mikataba yaliyowekwa katika Mkataba wa Vienna wa Mwaka 1969 (*Vienna Convention on the Law of Treaties, 1969*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele yake, Kamati ilifanya utafiti wa kutosha kupitia vyanzo mbalimbali ili kujiridhisha kuhusu mataifa yaliyosaini Mkataba huu mwanzoni, yaliyojunga baadae na yale ambayo tayari yamesharidhia. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha kuhusu msimamo wa mataifa mbalimbali juu ya maudhui ya Mkataba huu. Kamati pia ilitaka kujiridhisha kuhusu nafasi ya Tanzania katika diplomasia na uhusiano na mataifa mengine kutokana na hatua ya kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu hasa katika kipindi hiki ambacho Jumuiya ya Kimataifa

inachukua jitihada za kutosha kuzuia mianya yote inayotishia usalama wa dunia hasa masuala ya Ugaidi.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Mwananchama wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*). Jukumu la Shirika hili ni kusimamia viwango vyta kazi ya Kimataifa, kuitia mapendekezo, Itifaki na Mikataba mbalimbali inayopitishwa na Mkutano Mkuu wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Tisini na Moja (91) cha Mkutano Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani, kilichofanyika tarehe 03 Juni, 2003 – Geneva Uswisi, Nchi Wanachama, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilisaini na kuitisha Mkataba huu kwa lengo la kuhakikisha kuwa mabaharia wanasajiliwa na kutambulika kimataifa.

2.0 CHIMBUKO, MADHUMUNI NA FAIDA YA MKATABA WA VITAMBULISHO VYA MABAHARIA

2.1 Chimbuko la Mkataba wa Vitambulisho vya Mabaharia

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Vitambulisho vya Kimataifa vya Mabaharia, ulianzishwa na Shirika la Kimataifa la Wasafirishaji (*International Workers' Federation (ITF)*) Mwaka 1954. Shirika hili lilipendekeza kuanzishwa kwa utambulisho wa pamoja wa Kimataifa kwa Mabaharia (*International Identity Documents for Seafarers'*) chini ya usimamizi wa Shirika la Kazi Duniani.

2.2 Madhumuni ya Mkataba wa Vitambulisho Vya Mabaharia

Mheshimiwa Spika, dhumi la kusainiwa Mkataba Namba 185 wa Mwaka 2003, ni kuweka usawa katika viwango vya kazi Kimataifa kwa kutumia vitambulisho maalum kwa Mabaharia pamoja na kuimarisha usalama wa Meli, Abiria na Mabaharia.

Mheshimiwa spika, kwa kupitia vitambulisho vinavyopendekezwa kwenye Mkataba huu, Mabaharia wataweza kuingia au kupita katika Nchi moja kwenda Nchi nyingine wakiwa Melini au kurudi kwenye Nchi zao kwani watakuwa wanatambulika kirahisi ikilinganishwa na wakati wa sasa ambapo hawatambuliki Kimataifa hivyo kusababisha utendaji kazi wao kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ni muhimu sana kwani utawezesha Mabaharia wote Duniani kuwa na usawa katika maslahi yao ya kikazi, kupata stahiki mbalimbali kwa usawa pamoja na kuwawezesha kupata huduma mbalimbali za msingi katika Nchi mbalimbali wanazopita na hivyo kuweza kuishi katika mazingira mazuri zaidi ya kikazi wanapokuwa safarini (Melini).

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Mabaharia vitaweka utambulisho wa pamoja na wa Kimataifa kwa Mabaharia (*International Identity*). Vitambulisho hivyo vitarahisisha mambo mbalimbali yanayohusu utekelezaji majukumu ya kibaharia. Kwa mfano, vitawarahisishia Mabaharia kupata huduma muhimu na za msingi katika nchi za kigeni wanazopita, kama vile, matibabu, mapumziko ya muda nchi kavu katika Nchi za kigeni na kupata mahitaji yao ya msingi ikiwa ni pamoja na burudani. Hata hivyo, Vitambulisho hivi havitakuwa mbadala wa pasi za kusafiria, bali vitatumika sambamba na pasi zao.

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Mabaharia vilevile vina umuhimu katika suala zima la Usalama wa Nchi Wananchama na Dunia kwa ujumla. Ikumbukwe kuwa, tukio la shambulio la kigaidi Nchini Marekani, 11 Septembe, 2001, ni tukio lilioshitua Mataifa mengi Duniani na kuanza kuchukua hatua mbali mbali za kiusalama ikiwa ni pamoja na kuzuia Mabaharia kuingia katika Nchi zao katika kuhakikisha kuwa Nchi zao haziingiliwi na Magaidi kwa kutumia mgongo wa Ubaharia.

Mheshimiwa Spika, suala la Ugaidi Nchini Marekani, vilevile, liliikumbusha Dunia kuhusu tukio la utekaji wa Meli ya Nchini

Italia- Ms ACHILLI LAURO ambayo ilitekwa na Maharamia wa Kipalestina tarehe 7 Oktoba, 1985.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matukio hayo mawili ya kigaidi pamoja na mengine, Jumuiya za Kimataifa zilionna umuhimu wa kuchukua tahadhari dhidi ya Ugaidi kwenye Meli na hivyo Shirika la Kazi Duniani, liliona umuhimu wa kuandaa Mkataba mpya wa Mwaka 2003 kwa kuzielekeza Nchi Wanachama kuanzisha utaratibu wa Vitambulisho Maalum vya Mabaharia (*Biometric – based personal Identification*) ili kudhibiti suala hili la Ugaidi.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu unaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuuridhia, ni mwendelezo wa utaratibu ulioanza miaka mingi iliyopita ambao ulihitaji kufanyika kwa jitihada za kutosha katika kushawishi Nchi Wanachama kuukubali na hatimaye kuuridhia.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulianza kutumika rasmi tarehe 9 Februari, 2005. Nchi yetu imechelewa sana kuridhia Mkataba huu kwani kwa sasa ni takriban Miaka Kumi na Mbili (12) imepita toka Mkataba huu ulipoanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu, unatambua uwepo wa Mikataba mingine ya Kimataifa ya Shirika la Bahari Duniani (*International Maritime Organisation*) inayohusu huduma za bandari pamoja na Usalama Baharini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Takwimu za Shirika la Kazi Duniani, hadi kufikia Disemba , 2016, Nchi Wanachama 34 zilikuwa zimesharidhia Mkataba huu ikiwemo Nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Madagascar, Nigeria na Tunisia.

2.3 Uratibu wa Masuala ya Mabaharia Nchini

Mheshimiwa Spika, masuala ya Mabaharia kwa upande wa Tanzania Bara yanaratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) pamoja na Sheria ya Usafiri Majini, Namba 21 ya Mwaka 2003. Kwa upande wa Tanzania

Zanzibar, unaratibiwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*) pamoja na Sheria ya Usafiri Baharini, Namba 5 ya Mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni zinazotumika kwa wakati huu Nchini, hazikinzani na matakwa ya Mkataba huu bali zinahitaji kuhuishwa ili ziweze kutumika kwa pamoja na kuwezesha kutolewa kwa vitambulisho hivi na kuwawezesha Mabaharia wetu waweze kutambulika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu, Nchi yetu haina vitambulisho kulingana na matakwa ya Mkataba huu, bali Mabaharia hutumia hati za kusafiria (*Passports*) pamoja na kitabu cha kutunza kumbukumbu za wafanyakazi melini kama utambulisho wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata maoni mbalimbali kutoka kwa Wadau, Kamati ilianza kazi ya kuitia na kuchambua maudhui yaliyomo kwenye Mkataba huu Ibara kwa Ibara kama inavyoonekana katika sehemu inayofuata katika Taarifa hii.

2.4 Maudhui ya Mkataba wa Vitambulisho vya Mabaharia

Mheshimiwa Spika, Ibara ya kwanza ya Mkataba huu unatoa tafsiri ya neno Baharia kuwa ni mtu yoyote aliyejiriwa au anayejihuisha au anafanya kazi yoyote kwenye Meli lakini haihusishi wale waliomo kwenye Meli za kivita. Ibara hii inaendelea kufafanua kuwa, endapo hoja itajitokeza kuwa ni Watu gani wanaweza kuingizwa kwenye tafsiri ya neno "Baharia" kama ilivyotafsiriwa katika Mkataba huu, basi hoja hiyo itaamuliwa na Chombo chenye Mamlaka cha Nchi husika ambapo mtu huyo ana Uraia (*Nationality*) au ana Hati ya Kudumu ya Kuishi (*Permanent Resident*), baada ya kuwasiliana na Mmiliki wa Meli pamoja na Chama cha Mabaharia kutoka Nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya pili (2) ya Mkataba inaelekeza Nchi Wananchama kutoa Vitambulisho vya Mabaharia

ambao ni Raia katika Nchi zao kwa kuzingatia maelezo yaliyomo kwenye Ibara ya Tatu (3) ya Mkataba huu. Aidha, Ibara hii inasisitiza kuwa, Sheria, Kanuni au taratibu zinazotumika kwenye Nchi husika za utaoji pasi za kusafiria, ndio hizo hizo zitakazotumika katika utoaji wa Vitambulisho vya Kimataifa vya Mabaharia. Vilevile, Ibara hii inaziruhusu Nchi Wanachama kutoa Vitambulisho vya Kimataifa vya Mabaharia kwa Mabaharia wanaotoka Nchi zingine ambao wamepata Hati za Kudumu za Makazi katika Nchi zao (*Permanent Resident Permits*).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Tatu (3) inaainisha Muundo na muda wa matumizi ya Vitambulisho vya Mabaharia. Vilevile Ibara hii inaweka vigezo vya Taarifa muhimu zinazopaswa kuwemo kwenye vitambulisho, ikiwa ni pamoja na Jina la Baharia, Jinsia, tarehe na sehemu ya kuzaliwa, picha, saini na alama nyingine za utambuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba huu, vitambulisho vya Mabaharia vinapaswa kutengenezwa katika Mfumo rahisi, unaosomeka kielektroniki, usioweza kugushwa na kutumia mali ghafi isiyoharibika kirahisi katika mazingira ya Bahari. Muda wa matumizi ya Vitambulisho hivi utazingatia Sheria na Kanuni za Nchi husika ambapo kulingana na Mkataba huu matumizi yake hayatazidi Miaka Kumi (10).

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne (4) inaweka wajibu kwa Nchi Wanachama kuanzisha na kusimamia Kanzidata (*Database*) ya kutunza kumbukumbu za vitambulisho vinavyotolewa, kusitishwa au kufutwa. Pamoja na mambo mengine, Ibara ya Tano (5) inaelekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Nchi Wanachama katika uzalishaji, utoaji na utunzaji wa vitambulisho ili kulinda ubora na Usalama wa Vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Sita (6) inaainisha hatua na taratibu za kuzingatiwa na Nchi Wanachama katika kuruhusu Mabaharia wenye vitambulisho halali vya Kimataifa kuingia na kutoka katika Nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Saba (7) inaweka vigezo na masharti ya umiliki na uftutaji wa vitambulisho. Katika Ibara hii inaelekezwa kuwa, kitambulisho kinachotolewa kwa Baharia kitaendelea kuwa mali ya Baharia na kitatunzwa na Baharia mwenyewe isipokuwa tu, kwa ridhaa yake, kama ataamua, kitatunzwa na Kiongozi wa Meli (*Master*) kwa ajili ya usalama. Aidha, Baharia anaweza kunyang'anywa na kufutiwa umiliki wa kitambulisho alichopewa endapo hatakuwa tena na vigezo vya kumwezesha kupata Kitambulisho hicho kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Mkataba huu.

2.5 Faida za Kurudhia Mkataba

Mheshimiwa Spika, endapo Mkataba huu utaridhiwa, Nchi yetu itapata faida zifuatazo:-

- (i) Kuongezeka na kukua kwa fursa za ajira kwa Mabaharia wa Kitanzania katika Meli za ndani za Kimataifa na hivyo kupunguza umaskini wa kipato na kuchangia ukuaji wa uchumi na pato la Taifa kwa ujumla;
- (ii) Kuongezeka kwa fursa za kiuchumi kwa Wajasiriamali waliopo pembezoni mwa Bahari na maeneo mengine;
- (iii) Kuwepo kwa vitambulisho vya Mabaharia vyenye viwango vya Kimataifa;
- (iv) Kuimarika kwa Mfumo wa Kisheria na Kitaasisi wa kusimamia masuala ya Mabaharia;
- (v) Kuwepo na Mfumo wa utambuzi wa Mabaharia wa Tanzania na wa Nchi za nje na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama wa Nchi yetu na Dunia nzima dhidi ya Ugaidi;
- (vi) Kuweza kubadilishana uzoefu na ujuzi kuhusu masuala ya Mabaharia;
- (vii) Kuwezesha kufanyika kwa biashara za Kimataifa kwa kutumia Meli kwa urahisi kwani kutakuwa hakuna haja ya kuwa na Visa kwa Mabaharia;
- (viii) Kuwezesha Mabaharia kuwa na uhuru na urahisi katika kutenda majukumu yao katika Nchi mbalimbali bila kuwa na vikwazo;
- (ix) Kuwapunguzia Mabaharia usumbufu katika utaratibu wa kupata visa kwa ajili ya kuingia katika nchi wanazosafiri ;

(x) Kuwawezesha Mabaharia kupata haki zao za msingi za kibinadamu kama kupata mapumziko, burudani, huduma muhimu kama matibabu na, kupata mahitaji mbalimbali ya msingi katika nchi za kigeni;

2.6 Madhara ya Kutoridhia Mkataba

Mheshimiwa Spika, endapo Mkataba huu hautaridhiwa, Nchi yetu itapata madhara yafuatayo:

- (i) Mabaharia wa Nchi yetu kukosa utambulisho wa Kimataifa na hivyo kukosa haki zao za Kimsingi za Kisheria wakati wa utendaji wao wa kazi katika Meli za kigeni;
- (ii) Mabaharia wetu wapatao Hamsini Elfu (50,000) wako kwenye mazingira hatarishi ya kupoteza ajira zao kwenye Meli za Kimataifa zikiwemo Meli ambazo zinapeperusha Bendera ya Tanzania na hivyo kuathiri mapato yao;
- (iii) Nchi yetu kukosa mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na malipo ya Mabaharia hao wanapokuwa kazini kwenye Meli za kigeni ;
- (iv) Kupungua kwa fursa za Mabaharia wetu kupata uzoefu wa Kimataifa katika Meli nydingine;
- (v) Mabahari wetu kutokuwekwa kwenye Mfumo mahsus wa Kimataifa wa Utambulisho hivyo kuwasababishia adha ya kupata Visa kwenye Nchi za kigeni kwani watakuwa hawatambuliki kirahisi;
- (vi) Nchi yetu kutokuwa salama kiulinzi kwani kuwapo kwa utambulisho wa pamoja, vyombo vyetu vya usalama vitapata urahisi wa kuwatambua Mabaharia kutoka Nchi zingine kwa urahisi;
- (vii) Kutoa mwanya kwa Watu ambaio sio Mabaharia ambaio wanaweza kujipenyeza na kuleta madhara Nchini hasa ya Ugaidi;

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa Mkataba wa Vitambulisho vya Mabaharia, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

- (i) Elimu ya kutosha itolewe kwa Wabunge kuhusu Mikataba yote inayowasilishwa Bungeni kwa ajilli ya kuridhiwa ili waweze kufanya maamuzi sahihi kwa manufaa ya nchi;
- (ii) Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba huu kwani una manufaa makubwa sana kwa Nchi yetu na kwa Mabaharia wenyewe na kuweza kudumisha Usalama katika Nchi yetu dhidi ya Ugaidi;
- (iii) Utekelezaji wa matakwa ya Mkataba huu ufanyike kwa haraka ili Mabaharia wetu waweze kutambulika Kimataifa na kupata haki zao za kimsingi wanapokuwa nje ya Nchi yetu;
- (iv) Sheria zinazotumika kwa sasa kuhusiana na kazi za Mabaharia zihuishwe ili kuuzeugesa matakwa ya Mkataba huu kutekelezeka;
- (v) Serikali itunge Sheria mahsusitakayotekeliza matakwa ya Mkataba huu (Domestication).

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, sina budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mb kwa ushirikiano mkubwa alioutoa wakati Kamati ilipokuwa inajadili Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kuupitia, kuuchambua na hatimaye kutoa mapendelekezo katika Mkataba huu. Wajumbe wamefanya kazi kwa uzalendo mkubwa pamoja na ushirikiano wa dhati hadi kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivoorodheshwa hapa chini.

- (i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, Makamu Mwenyekiti
- (iii) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb, Mjumbe
- (iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe
- (v) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe
- (vi) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe
- (vii) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb, Mjumbe
- (viii) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe
- (ix) Mhe. Wanou Hafidhi Ameir, Mb, Mjumbe
- (x) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe
- (xi) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe
- (xii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe
- (xiii) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe
- (xiv) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe
- (xv) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe
- (xvi) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe
- (xvii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe
- (xviii) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe
- (xix) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe
- (xx) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe
- (xxi) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe
- (xxii) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe
- (xxiii) Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe
- (xxiv) Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb, Mjumbe

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vilevile napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Sanga kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Stella Bwimbo na Ndg. Dunford Mpelumbwe wakisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa

kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI,KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA KATIBA NA SHERIA**
JUNI, 2017

NAIBU SPIKA: Sasa tumsikilize Mheshimiwa Hongoli kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati

MHE. JORAM I. HONGOLI - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria naomba kuwasilisha maoni na ushauri ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Azimio la Bunge kuridhia mkataba wa Kimataifa wa kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani yaani *Maritime Labour Convention 2006*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kifungu cha 6 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inasimamia Wizara tatu ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu sababu za Serikali kuamua kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa kazi za ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*Maritime Labour Convention of 2006*), kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, tarehe 30 Mei, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilipokea Maoni ya Wataalam waliobobea katika masuala ya Bahari na Ubaharia na hivyo kujenga uwezo katika uelewa wa maudhui ya Mkataba huu. Wataalam waliosaidia Kamati katika uchambuzi huu ni pamoja na:-

Dkt. Tumaini Ngurumo mwanamke wa kwanza kupata Shahada ya Uzamivu, *Doctorate* katika Sheria za Bahari hapa Tanzania. Capt. Ibrahim Mbiu Bendera ambaye ni Wakili na Captain wa meli ambaye amefanya kazi katika Sekta ya Bahari kwa miaka 23, Ndugu Antony Lutabanzibwa ambaye ni Afisa Mwandamizi wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), Profesa Koti Kamanga, Profesa Mshiriki yaani *Associate Professor* kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule ya Sheria na Wataalam kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Masuala ya Sheria wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam hawa walitoka katika Taasisi zifuatazo:-

- (i) Mamlaka ya Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*)
- (ii) Chuo cha Bahari Dar es Salaam (*Dar es Salaam Maritime Institute*)
- (iii) Chama cha Wanasheria wa Masuala ya Bahari Tanzania (*Tanzania Maritime Law Association*);
- (iv) Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*).
- (v) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- (vii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia mradi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) kwa kuwawezesha Wabunge kwenye Masuala ya Kibunge (*Legislative Support Programme- LSP*) iliiwezesha Kamati kupata uelewa kuhusu Kanuni za msingi za Sheria ya Kimataifa katika kuridhia mikataba ya namna hii na utaratibu wa Kikatiba na Kisheria wa Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Uelewa huu ulisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo ya Msingi yaliyozingatiwa na Kamati; ili kuiwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba, Kamati ilizingatia mambo yaliyo muhimu katika kuifanya kazi hoja hii ya Serikali. Kamati iliifanyia mapitio ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria mbalimbali zinazohusiana na Kazi, Ajira na Hakika Binadamu, uzoefu wa nchi nyiningine pamoja na kutazama faida na hasara za Mikataba husika kwa ujumla wake. Kamati pia iliridhia na matakwa ya Sheria za Kimataifa kuhusu uridhiaji wa Mikataba yaliyowekwa katika Mkataba wa Vienna wa Mwaka 1969 (*Vienna Convention on the Law of Treaties, 1969*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele yake, Kamati ilifanya utafiti wa kutosha kupitia vyanzo mbalimbali ili kujiridhisha kuhusu Mataifa yaliyosaini Mkataba huu mwanzoni, yaliyojunga baadaye na yale ambayo tayari yamesharidhia. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujadili kuhusu msimamo wa Mataifa mbalimbali juu ya Mkataba huu na nafasi ya Tanzania katika diplomasia na uhusiano na Mataifa mengine kutokana na hatua ya kuridhia au kutoridhia Mkataba huu hasa katika kipindi hiki ambacho Sera ya Mambo ya Nje ya Nchi imeegemea katika diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu wa Shirika la Kazi Duniani ni moja kati ya mikataba mikuu ya Shirika la Kazi Duniani ambao unahusisha meli zote zinazoingia katika

Bandari za Nchi Wanachama wa *ILO* au meli ambazo zinapepea bendera za Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu ulitiwa saini mwaka 2006 na kuanza kutumika mwaka 2013 baada ya kuridhia na nchi 30 kulingana na vigezo vya Mkataba vilivyowekwa wakati wa kutia saini mkataba huu mwaka 2006 mpaka kufikia mwaka 2016 mkataba huu umeridhiwa na nchi 80. Baadhi ya Nchi za Afrika ambazo zimeridhia mkataba huu ni Kongo DRC 2015, Nigeria 2014, Gabon Septemba, 2015 Ghana Agosti, 2014, Kenya 31 Julai, 2015 Liberia tarehe 20 Agosti, 2013, Mauritius 30 Mei, 2015. Kwa nchi za Jumuiya za Ulaya hadi kufikia mwaka 2016 Nchi 24 kati ya 27 za Jumuiya ya Ulaya zimeridhia mkataba huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chanzo na Malengo ya Madhumuni ya Mkataba; Mkataba huu una maeneo makuu matano, sifa za msingi za Mabaharia kufanya kazi katika meli, masharti ya ajira, malazi, chakula na huduma za kijamii, afya na ustawi wa hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba huu, umri wa Baharia kufanya kazi katika Meli ni miaka 16 na 18 ni kwa kazi za usiku na kazi za Ubaharia katika mazingira hatarishi. Mabaharia wanatakiwa kuwa na afya njema na vyeti vya afya vinavyowawezesha kufanya kazi za ubaharia. Mabaharia wanatakiwa kupata mafunzo maalum ya ubaharia na mafunzo ya usalama kuhusu ubaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masharti ya ajira za Mabaharia, mkataba huu unazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Mabaharia wanapata mikataba ya kazi yenye masuala yote msingi kama malipo stahiki, likizo, bima, haki ya baharia kurudishwa katika nchi yake, yaani *repatriation* endapo meli imepotea au imeachwa kufanya kazi wakati akiwa katika nchi iliyosajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mavazi, chakula, huduma kijamii, mkataba huu unazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Mabaharia wanafanya kazi katika

mazingira mazuri, ambayo yanajenga afya zao na usalama wao kazini, Mabaharia pia wana haki ya kupata chakula na malazi mazuri wanapokuwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya na ustawi wa jamii; mkataba huu unazitaka Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba mabaharia wanapata haki zote za kupata huduma za afya wakiwemo kazini na katika nchi wanazokwenda au wanazopita yaani *on transit states*. Nchi Wanachama zinatakiwa kuwa na mazingira salama kwa ajili ya afya na usalama wa mabaharia, mifumo mizuri ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya mabaharia. Mabaharaia wana haki pia ya kupata huduma za ustawi wa jamii katika nchi wanazofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wake, mkataba huu unazitaka nchi wanachama, Wakala wa Meli na usalama baharini, nchi zenyenye bendera yaani (*flag states*) na nchi zilizo na bandari (*port states*) kutekeleza mkataba huu na ukaguzi wa mara kwa mara kuwa unafanyika ili kuona kwamba wahusika wote wanatekeleza mkataba huu. Vyeti vya utekelezaji wa mkataba huu yaani *certificates of marine compliance* huwa vinatolewa na meli zote na wakala wote wanaohusika na masuala ya kazi za mabaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pamoja na nchi nyingine wanachama wa Shirika la Kazi Duniani zilishiriki katika mchakato wote uliopelekea kupatikana kwa mkataba huu mwaka 2006, Jijini Geneva Uswiswi. Ujumbe wa Tanzania katika mchakato huu uliongozwa na aliyekuwa Balozi wa Tanzania Geneva – Switzerland Mheshimiwa Balozi Charles Mutalemwa pamoja na wawakilishi kutoka Vyama vya Wafanyakazi na Chama cha Waajiri Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kuridhia mkataba huu; endapo Tanzania itaridhia mkataba huu ziko faida nyingi ambazo zitapatikana kwa nchi na Mabaharia wa Kitanzania. Faida hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mabaharia Watanzania watakuwa na fursa ya ajira ya sawa na mabaharia wa nchi nyingine katika soko la ajira la Kimataifa;

- (ii) Nchi yetu kuweza kutambuliwa kama nchi mojawapo zinazojali viwango vya ajira za ubaharia;
- (iii) Mishahara ya mabaharia wa Kitanzania itakuwa bora zaidi na nchi yetu itapata pato kubwa la fedha za kigeni kuititia ajira za Mabaharia;
- (iv) Mabaharia wa Tanzania watapata mafao ya hifadhi ya jamii na hivyo kuleta tija na hali bora katika ajira melini;
- (v) Kuongezeka kwa mapato ya nchi kutokana na fedha zinazotumwa na mabaharia wa Kitanzania wakiwa nje ya nchi yaani *remittances*; na
- (vi) Kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri majini na kuongezeka kwa fursa za mafunzo ya ubaharia kwa mamlaka za usafiri majini Tanzania na Watanzania wanaofanya kazi katika sehemu hiyo kuititia mashirika mbalimbali ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kuridhia mkataba huu; Iwapo Tanzania itaridhia mkataba huu zipo changamoto mbalimbali za kiutendaji na kiutaalam ambazo tutalazimika kuzikabili ili kutekeleza kwa ufanisi matakwa ya mkataba huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

Nchi italazimika kuongeza idadi ya wataalam watakaosimamia masuala ya kitaalam katika utekelezaji wa mkataba huu hasa katika maeneo ya ukaguzi (*audit and inspection*). Nchi pia itakuwa na changamoto ya kuendeleza kutoa mafunzo stahiki katika Sekta ya Ubaharia na hivyo kuzidi kutoa wataalam wengi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kutoridhia mkataba huu; Mkataba wa kazi za Mabaharia ni mkataba mama ambao umeunganishwa (*consolidation*) na Mikataba ya 37 ambayo ilikuwa inatoa haki mbalimbali kwa mabaharia na watu wanaofanya kazi katika Sekta ya Bahari. Baada ya hii mikataba kuunganishwa, upatikanaji wa mkataba huu ambao kwa sasa ni moja kati ya mikataba minne mikubwa katika Sekta ya Kazi ya Baharini kwa kwa kutoridhiwa

mkataba huu Tanzania na Mabaharia wa Tanzania wataendelea kupoteza fursa nyingi za ajira na uchumi ambao zinatokana na nchi kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Katiba. Marekebisho ya ndani ya Sheria ili kuendana na matakwa ya mkataba huu (*domestication*). Ibara ya tano ya mkataba huu inazitaka nchi wanachama kutunga sheria, kanuni na kuunda taasisi zitakazotekeleza matakwa ya mkataba huu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya marekebisho katika Sheria ya Meli za Biashara (*Maritime Shipping Act 2003*) kwa upande wa Tanzania Bara na Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 kwa upande wa Zanzibar yaani *Maritime Transport Act of 2006* ili kuendana na matakwa ya mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya jumla ya Sheria nyingine zinazohusiana na ajira; Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio na kurekebisha sheria zote zinazohusiana na haki za mabaharia ili kuendana na haki za msingi za Mabaharia zinazotajwa katika mkataba huu. Kwa mfano, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Na. 6 ya Mwaka 2004; Sheria ya Taasisi za Kazi, Na. 7 ya Mwaka 2004; Sheria ya Usalama wa Afya Mahali pa Kazi, Na.5 ya Mwaka 2003; Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Na. 20 ya Mwaka 2008; na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii, Na. 8 ya mwaka 2008 kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkataba huu unaridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa rai kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mapitio na maboresho ya Sheria zinazohusika na masuala ya kazi za Mabaharia na hasa Sheria ya Ajira, Na. 11 ya Mwaka 2005; Sheria ya Mahusiano Kazini, Na. 1 ya Mwaka 2005; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Na. 8 ya Mwaka 2005; na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Na. 5 ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, uundaji wa taasisi maalum inayosimamia Sekta ya Usafiri Majini. Kutokana na umuhimu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli, dakika moja umalizie. Muda umekwisha!

MHE. JORAM I. HONGOLI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba hotuba yote au taarifa yote ya Azimio hili iweze kuingia kwenye kumbukumbu yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti kwa uendeshaji mzuri wa Bunge letu nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuwasilisha na ufanuzi wa kina aliota kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa mkataba huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru sana wataalam wote waliofika mbele ya Kamati na kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kitaalam wa faida na changamoto za kuridhia mkataba huu. Wapo wadau ambao walisafiri kutoka Zanzibar kwa ajili ya kazi hii, tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilllah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman B. Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Angelina Lingisi Sanga kwa kuiwezesha Kamati wakati wote kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii ndugu Stella Bwimbo, ndugu Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati ndugu Rahel Masima kwa kuihudumia Kamati vyema na bila kuchoka na kuhakikisha...

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli.
Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Unga mkono Azimio.

MHE. JORAM I. HONGOLI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono Azimio na ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA KIMATAIFA WA KAZI ZA UBAHARIA WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (*MARITIME LABOUR CONVENTION, 2006*) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*Maritime Labour Convention, 2006*).

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, Jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane Kifungu cha 6(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inasimamia Wizara tatu ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu sababu za Serikali kuamua kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*Maritime Labour Convention, 2006*) kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu Mhe.Jenista Mhagama tarehe 30 Mei, 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilipokea Maoni ya Wataalamu wallobobe katika masuala ya Bahari na Ubaharia na hivyo kujenga uwezo katika kuelewa wa maudhui ya Mkataba huu. Wataalamu walioisaidia Kamati Katika uchambuzi huu ni pamoja na Dr. Tumaini Gurumo, Mwanamke wa kwanza kupata Shahada ya uzamivu (*Doctorate*) katika Sheria za Bahari hapa Tanzania, Kapteni Ibrahimu Mbiu Bendera ambaye ni Wakili na Kapteni wa Meli ambaye amefanya kazi katika Sekta ya Bahari kwa Miaka 23 , Ndugu Antony Rutabanzibwa ambaye ni Afisa Mwandamizi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO),Profesa Khoti Khamanga,profesa mshiriki (Associate Professor) kutoka chuo kikuu cha Dar es Salaam,shule ya Sheria na wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Masuala ya Sheria wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wataalamu hawa walitoka katika Taasisi zifuatazo;

- (i) Mamlaka ya Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*)
- (ii) Chuo cha Bahari Dar es Salaam (*Dar es Salaam Maritime Institute*)
- (iii) Chama cha Wanasheria wa Masuala ya Bahari Tanzania (*Tanzania Maritime Law Association*)

- (iv) Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organisation*)
- (v) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- (vi) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mikataba

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Juni, 2017 Ofisi ya Bunge kupitia mradi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) wa kuwawezesha Wabunge kwenye masuala ya Kibunge (*Legislative Support Program - LSP*) iliiwezesha Kamati kupata uelewa kuhusu Kanuni za msingi za Sheria za Kimataifa katika kuridhia mikataba ya namna hii na utaratibu wa Kikatiba na Kisheria wa Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa.Uelewa huu uliisaidia Kamati kuwa katika nafasi nzuri kuifanyia kazi hoja hii.

2.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja hii ya Serikali . Kamati ilifanya mapitio ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria mbalimbali zinazohusiana na Kazi, Ajira na Haki za Binadamu, Uzoefu wa nchi nyingine pamoja na kutazama faida na hasara za Mkataba husika kwa ujumla wake. Kamati pia ilijiridhisha na matakwa ya Sheria za Kimataifa kuhusu uridhiaji wa Mikataba yaliyowekwa katika Mkataba wa Vienna wa Mwaka 1969 (*Vienna Convention on the Law of Treaties, 1969*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele yake, Kamati ilifanya utafiti wa kutosha kupitia vyanzo mbalimbali ili kujiridhisha kuhusu mataifa yaliyosaini Mkataba huu mwanzoni , yaliyojunga baadae na yale ambayo tayari yameridhia .

Mheshimiwa Spika, mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha kuhusu msimamo wa Mataifa mbalimbali juu ya Mkataba huu na nafasi ya Tanzania katika Diplomasia

na Uhusiano na Mataifa mengine kutokana na hatua ya kuridhia au kutokuridhia Mkataba huu hasa katika kipindi hiki ambacho Sera ya Mambo ya Nje ya Nchi imeegemea katika diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu wa Shirika la Kazi Duniani ni moja kati ya Mikataba Mikuu ya Shirika la Kazi Duniani ambaao unahusisha Meli zote zinazoingia katika Bandari za nchi Wanachama wa ILO au Meli ambazo zinapepea Bendera za nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulitiwa saini Mwaka 2006 na kuanza kutumika Mwaka 2013 baada ya kuridhiwa na nchi 30 kulingana na vigezo vya Mkataba vilivyowekwa wakati wa kutia saini Mkataba Mwaka 2006. Mpaka kufikia Mwaka 2016, Mkataba huu umeridhiwa na nchi 80. Baadhi ya nchi za Afrika ambazo zimeridhia Mkataba huu ni Congo DRC (2015), Nigeria (2014), Gabon (Septemba, 2015), Ghana (Agosti, 2014), Kenya (31 Julai 2015), Liberia (20 Agosti 2013) na Mauritius (30 Mei, 2015). Kwa nchi za Jumuia ya Ulaya, hadi kufikia Mwaka 2016, nchi 24 kati ya 27 za Jumuia ya Ulaya zimesharidhia Mkataba huu.

2.1 CHANZO, MALENGO NA MADHUMUNI YA MKATABA

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu una maeneo Makuu Matano; sifa za msingi za Mabaharia kufanya kazi katika Meli, masharti ya ajira, malazi, chakula na huduma za kijamii, afya, ustawi na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba huu umri wa Baharia kufanya kazi katika Meli ni Miaka 16 na Miaka 18 ni kwa kazi za usiku au kazi za Ubaharia katika mazingira hatarishi. Mabaharia wanatakiwa kuwa na afya njema na vyeti vya afya vinavyowawezesha kufanya kazi za Ubaharia. Mabaharia wanatakiwa kupata mafunzo maalumu ya Ubaharia na mafunzo ya usalama kuhusu Ubaharia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masharti ya ajira za Mabaharia, Mkataba huu unazitaka nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Mabaharia wanapata Mikataba ya kazi yenye

masuala yote ya msingi kama malipo stahiki, likizo, Bima, haki ya Baharia kurudishwa katika nchi yake (*Repatriation*) endapo Meli imepotea au imeacha kufanya kazi wakati ikiwa katika nchi iliyosajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malazi, chakula na huduma za Kijamii, Mkataba huu unazitaka nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Mabaharia wanafanya kazi katika mazingira mazuri ambayo yanajenga afya zao na usalama wao kazini. Mabaharia pia wana haki ya kupata chakula na malazi mazuri wanapokua kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya, Ustawi na Hifadhi ya Jamii, Mkataba huu unazitaka nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Mabaharia wanapata haki zote za kupata huduma za afya wakiwepo kazini na katika nchi wanazokwenda au wanazopita (*Transit States*). Nchi Wanachama zinatakiwa kuwa na mazingira salama kwa ajili ya afya na usalama wa Mabaharia na Mifumo mizuri ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya Mabaharia. Mabaharia wana haki pia ya kupata huduma za Ustawi wa Jamii katika nchi wanazofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wake, Mkataba huu unazitaka nchi Wanachama , Wakala wa Meli na Usalama wa Baharini, Nchi zenye Bendera (*Flag States*) na nchi zilizo na Bandari (*Port States*) kutekeleza Mkataba huu na ukaguzi wa mara kwa mara huwa unafanyika ili kuona kwamba wahusika wote wanatekeleza Mkataba huu. Vyeti vyaa utekelezaji wa Mkataba huu (*Certificates of Maritime Compliance*) huwa vinatolewa kwa Meli zote na Wakala wote wanaohusika na masuala ya kazi za Mabaharia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pamoja na nchi nyingine Wanachama wa Shirika la Kazi Duniani zilishiriki katika mchakato wote uliopelekea kupatikana kwa Mkataba huu Mwaka 2006 Jijini Geneva, Uswisi. Ujumbe wa Tanzania katika mchakato huu uliongozwa na aliyekua Balozi wa Tanzania Geneva, Switzerland Mhe. Balozi Charles Mutalemwa pamoja na wawakilishi kutoka Vyama vyaa Wafanyakazi na Chama cha Waajiri Tanzania.

2.2 FAIDA ZA KURIDHIA MKATABA HUU

Mheshimiwa Spika, endapo Tanzania itaridhia Mkataba huu, zipo faida nyingi ambazo zitapatikana kwa nchi na Mabaharia wa Kitanzania. Faida hizo ni kama ifuatavyo;

- (i) Mabaharia wa Tanzania watakuwa na fursa ya Ajira sawa na Mabaharia wa nchi nyingine katika Soko la Ajira la Kimataifa;
- (ii) Nchi yetu kuweza kutambulika kama nchi mojawapo zinazojali viwango vya ajira za Ubaharia;
- (iii) Mishahara ya Mabaharia wa Kitanzania itakua bora zaidi na nchi yetu itajipatia pato kubwa la fedha za kigeni kuititia ajira za Mabaharia;
- iv) Mabaharia wa Tanzania watapata mafao yao ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuleta tija na hali bora katika ajira Melini;
- (iv) Kuongezeka kwa mapato ya Nchi kutokana na fedha zinazotumwa na Mabaharia wa Kitanzania wakiwa nje ya nchi (*Remittances*);
- (v) Kuimariika usalama wa vyombo vya usafiri majini na kuongezeka kwa fursa za mafunzo ya Ubaharia kwa Mamlaka za usafiri majini Tanzania na Watanzania wanaofanya kazi katika Sekta hiyo kuititia Mashirika mbalimbali ya Kimataifa.

2.3 CHANGAMOTO ZA KURIDHIA MKATABA HUU

Mheshimiwa Spika, iwapo Tanzania itaridhia Mkataba huu, zipo changamoto mbalimbali za Kiutendaji na Kiutaalamu ambazo italazimika kuzikabili ili kutekeleza kwa ufanisi matakwa ya Mkataba huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo; nchi italazimika kuongeza idadi ya Wataalamu watakaosimamia masuala ya Kitaalamu katika utekelezaji wa Mkataba huu hasa katika maeneo ya ukaguzi (*Audits na Inspection*). Nchi pia itakua na changamoto ya kuendelea kutoa mafunzo stahiki katika Sekta ya Ubaharia na hivyo kuzidi kutoa Wataalamu wengi zaidi katika eneo hili.

2.4 MADHARA YA KUTORIDHIA MKATABA

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kazi za Mabaharia ni Mkataba Mama ambao umeunganisha (*Consolidation*) Mikataba 37 ambayo ilikua inatoa haki mbalimbali kwa Mabaharia na Watu wanaofanya kazi katika Sekta ya Bahari. Baada ya hii Mikataba kuunganishwa ukapatikana Mkataba huu ambao kwa sasa ni moja kati ya Mikataba Minne mikubwa katika Sekta ya kazi za Baharini. Kwa kutokuridhia Mkataba huu Tanzania na Mabaharia wa Tanzania wataendelea kupoteza fursa nyngi za ajira na uchumi ambazo zinatokana na nchi kuridhia Mkataba huu.

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

i) **Marekebisho ya Sheria za ndani ya Nchi ili kuendana na matakwa ya Mkataba huu (*Domestication*)**

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Tano (V) ya Mkataba huu inazitaka Nchi Wanachama kutunga Sheria, Kanuni na kuunda Taasisi zitakazotekeleza matakwa ya Mkataba huu kwa ufanisi. Kamati inatoa Rai kwa Serikali kuititia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya marekebisho katika Sheria ya Meli za Biashara (*Merchantile Shipping Act, 2003*) kwa upande wa Tanzania Bara na Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2006 kwa upande wa Zanzibar (*Maritime Transport Act, 2006*) ili kuendana na matakwa ya Mkataba Huu.

ii) **Maboresho ya ujumla ya Sheria nyngine zinazohusiana na Ajira za Mabaharia**

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio na kurekebisha Sheria zote zinazohusiana na haki za Mabaharia ili kuendana na haki za msingi za Mabaharia zilizotajwa katika Mkataba huu. Kwa mfano, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Namba 6 ya Mwaka 2004, Sheria ya Taasisi za Kazi Namba 7 ya Mwaka 2004, Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Namba 5 ya Mwaka 2003, Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Namba 20 ya Mwaka 2008 na Sheria ya Usimamizi na Udhhibit wa Hifadhi ya Jamii, Namba 8 ya Mwaka 2008 kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkataba huu unaridhiwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa rai kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufanya mapitio na maboresho ya Sheria zinazohusika na masuala ya kazi za Mabaharia na hasa Sheria ya Ajira, Namba 11 ya Mwaka 2005, Sheria ya Mahusiano Kazini, Namba 1 ya Mwaka 2005, Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Namba 8 ya Mwaka 2005 na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Namba 5 ya Mwaka 2005.

iii) Uundaji wa Taasisi Maalumu itakayosimamia Sekta ya Usafiri Majini

Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu wa Sekta hii na ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa Sekta ya Usafiri Majini na utekelezaji wa matakwa ya Mkataba huu, Kamati inashauri iundwe Taasisi itakayosimamia Sekta ya Usafiri Majini tu kwa upande wa Tanzania Bara kama ilivyo Taasisi ya usimamizi wa Sekta hiyo kwa upande wa Zanzibar (*Zanzibar Maritime Authority*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inafahamu kwamba tayari kuna SUMATRA (Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini) ambayo pia inasimamia Sekta ya Usafirishaji Majini. Kwa kuridhia Mkataba huu, Kamati inaona kwamba huu ni muda muafaka wa kuwa na chombo mahususi kitakachosimamia Sekta ya Usafirishaji Majini. Uamuzi huu pia utaongeza ufanisi kwa Mamlaka ambayo itakua inasimamia Usafiri wa Nchi Kavu tu.

iv) Utoaji zaidi wa mafunzo

Mheshimiwa Spika, Kwa kuridhia Mkataba huu Tanzania itatengeneza fursa zaidi za Ajira kwa Vijana wa Kitanzania ndani na nje ya Tanzania katika Sekta ya Ubaharia. Kamati inatoa wito kwa Serikali kupanua wigo wa Taaluma ya Ubaharia na Taaluma nyingine zinazoendana na Ubaharia kama Upishi kuititia Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam na vyuo vingine binafsi vilivyopo Zanzibar ili kuongeza nafasi ya Mabaharia wa Tanzania kukubalika na kuajiriwa nje ya Nchi.

v) Utengenezaji na uboreshwaji wa Kanuni husika

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa Rai kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufanya mapitio na maboresho ya Kanuni zilizo chini ya Sheria mbalimbali ambazo zinahusika na masuala ya kazi na haki za Mabaharia ili kurahisisha upatikanaji wa haki hizo.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa michango mizuri wakati wa kuchambua Azimio hili ambayo imesaidia kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa Majina kama ifuatavyo:-

Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa,	Mb - Mwenyekiti
Mhe. Najma Murtaza Giga,	Mb – Makamu /Mwenyekiti
Mhe. Ajali Rashid Akbar,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Ally Saleh Ally,	Mb -Mjumbe;
Mhe. Anna Joram Gidarya,	Mb -Mjumbe;
Mhe. Asha Abdallah Juma,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Juma Hamad Kombo,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Joram Ismael Hongoli,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Joseph Kizito Mhagama,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Makame Mashaka Foum,	Mb - Mjumbe;-
Mhe. Mboni Mohamed Mhita,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Nassor Suleiman Omar,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Omary Ahmad Badwel,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Wanou Hafidhi Ameir,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Riziki Shahari Mngwali,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Saumu Heri Sakala,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Seif Ungando Ally,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Selemani Jumanne Zedi,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Taska Restitura Mbogo,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Twahir Awesu Mohammed,	Mb - Mjumbe;
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi,	Mb - Mjumbe
Mhe. David Mathayo David,	Mb - Mjumbe

Mhe. Ussi Pondeza,

Mb – Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uendeshaji mzuri wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu Mhe.Jenista Mhagama kwa uwasilishaji na ufanuzi wa kina alioutoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru sana Wataalamu wote waliofika mbele ya Kamati na kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa Kitaalamu wa Faida na changamoto za kuridhia Mkataba. Wapo wadau ambao walisafiri kutoka Zanzibar kwa ajili ya kazi hii.Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Langisi Sanga kwa kuiwezesha Kamati wakati wote kutekeleza majukumu yake bila kukwama. Aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndugu Stella Bwimbo, Ndugu Dunford Mpelumbwe na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia Kamati vyema na bila kuchoka na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio na naomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja. (*Makofii*)

Mohamedi Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA NA SHERIA
28 JUNI, 2017

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. ESTER A. BULAYA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni hayo, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunjaalia uhai na kuniwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge nikiwa na afya njema. Pia napenda kutumia fursa hii kumpongeza kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbewe kwa uongozi wake mahili na busara zake ambazo zimeifanya Kambi kuendelea kuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Wabunge wote wa Upinzani kwa ujumla wao kwa kutimiza wajibu wao kikamilifu wa kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mustakabali mwema wa Taifa letu lakini pia kwa ushirikiano wanaonipa ili kuendelea kutekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Temeke kwa kuendelea kunipa ushirikiano mzuri katika kutekeleza majukumu yangu. Naendelea kuwaahidi kuwa nitaendelea kutoa utumishi uliotukuka kwao na kamwe sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunivumilia hasa pale ninapokuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu yangu ya Kibunge. Upendo wao kwangu umekuwa ni chachu na kichocheo kwangu katika kufanya kazi yangu kwa bidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salam hizo, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni kuhusu Mkataba ulio mbele yetu ambao unahitaji uridhiwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi mdogo wa Watanzania katika kutekeleza mkataba na itifaki za Kimataifa. Serikali yetu imekuwa na utashi mdogo wa kutekeleza mkataba na itifaki za Kimataifa. Hii ni kwa sababu imekuwa ikichukua muda mrefu mno kuleta Bungeni mikataba au itifaki za Kimataifa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge na hata pale mikataba au itifaki hizo zinapowasilishwa, zinaporidhiwa na Bunge bado Serikali imekuwa na ugumu wa kuleta Miswada ya Sheria kwa minajili ya kutunga Sheria za Mikataba au itifaki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri wa ucheleweshaji usio na tija wa kuleta mikataba au itifaki kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge, ni mkataba huu Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani. Mkataba huu uliandaliwa tangu mwaka 2006, nchi yetu ilitia sahihi makubaliano hayo, lakini umecheleweshwa kwa zaidi ya miaka kumi kuletwa mkataba huu hapa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itambue kuwa nchi yetu sio kisiwa, nchi yetu ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa na kwa sababu hiyo inatakiwa kushiriki katika mikataba na itifaki za Kimataifa ili kwenda sambamba na mageuzi makubwa katika nyanja mbalimbali yanayoendelea kutokea duniani. Bila kuwa sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa kwa maana ya kushiriki na kuridhia Itifaki za Kimataifa, nchi yetu itaendelea kubaki nyuma na hatimae kutengwa na jamii ya Kimataifa na jambo hili sio zuri kwa nchi changa za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Mkataba wa Kimataifa wa Kazi wa Mabaharia wa Shirika la Kazi Duniani wa Mwaka 2006. Maudhui ya Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani la mwaka 2006, ni kuweka mazingira mazuri na salama kwa mabaharia pamoja na wamilikiwa vyombo vyaa usafiri majini. Mkataba huu

unalenga kuweka utaratibu wa kuwatambua mabaharia kwa kuzitaka Nchi Wanachama kutoa nyaraka za utambulisho kwa kila raia wa nchi husika ambaye nchi yake imeridhia mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu unaweka bayana kwamba kutokana na kuongezeka kwa vitendo nya kiharamia dhidi ya tasnia ya usafirishaji majini usalama wa wasafirishaji, mabaharia na vyombo kwenye usafiri wa majini uko hatarini hivyo kutokana na hali hiyo imebidi watu/wafanyakazi za ubaharia wapatiwe ulinzi maalum wa Kimataifa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa usalama kama ambavyo wafanyakazi wengine wamekuwa wakilindwa na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu umetambua haki za Mabaharia, wamiliki wa vyombo nya usafiri majini na haki za nchi husika ambazo kazi za ubaharia zinakuwa zinafanyika katika ngazi za Kimataifa. Aidha, mkataba huu unaweka misingi ya kutambuliwa kwa kutendewa haki kwa Mabaharia wakiwa nchi zao zingekuwa zimeridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkataba huu umelenga kuweka mazingira mazuri ya kazi za ubaharia Kimataifa; na kwa kuwa Mkataba huu unalenga pia kuhakikisha usalama wa mabaharia, wasafiri wanaotumia vyombo nya majini na wamiliki wa vyombo nya usafiri majini ili kukabiliana na vitendo nya kihalifu dhidi ya maharamia wa vyombo nya usafiri majini; na kwa kuwa nchi yetu ina mahusiano ya kibashara na Mataifa mengine mbalimbali ambazo meli zao za mizigo zinaingia katika bandari yetu na kutoka na Mataifa mengine ambayo meli zetu zinaingia na kutoka; na kwa kuwa Shirika la Kazi Duniani ni chombo cha Umoja wa Mataifa ambacho Tanzania ni Nchi Mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na inapendekeza kwamba Bunge hili liridhie mkataba huu kwa kuwa una manufaa kwa nchi yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka

Serikali kulieleza Bunge hili ni lini italeta Muswada wa Sheria ya Kusimamia utekelezaji wa Mkataba huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI YA MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA,
AJIRA NA WENYE ULEMAVU, MHESHIMIWA ESTHER AMOS
BULAYA (MB), KUHUSU MKATABA WA KIMATAIFA WA KAZI
ZA UBAHARIA WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (MARITIME
LABOUR CONVENTION, 2006) - KAMA ILIVYOWASILISHWA
MEZANI**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge nikiwa na afya njema. Pili, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge (Mb), kwa uongozi wake mahiri na busara zake ambazo zimeifanya Kambi kuendelea kuwa imara. Aidha, nawapongeza wabunge wote wa upinzani kwa ujumla wao kwa kutimiza wajibu wao kikamilifu wa kuisimamia Serikali kwa mustakabali mwema wa tafifa letu, lakini pia kwa ushirikiano wanaonipa, ambao umeniwezesha kutekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii pia kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kuendelea kuniamini, na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge. Ninaendelea kuwaahidi utumishi uliotukuka na kamwe sitawaangusha. Mwisho, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunivumilia, hasa pale ninapokuwa mbali nao wakati nikitekeleza majukumu yangu ya kibunge. Upendo wao kwangu umekuwa chachu kubwa na kichocheo kwango kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mkataba uliopo mbele yetu ambao unahitaji kuridhiwa na Bunge.

2. UTASHI MDOGO WA TANZANIA KATIKA KUTEKELEZA MIKATABA NA ITIFAKI ZA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imekuwa na utashi mdogo wa kutekeleza mikataba na itifaki za kimataifa. Hii ni kwa sababu, imekuwa ikichukua muda mrefu mno kuleta bungeni mikataba au itifaki za kimataifa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge. Na hata pale mikataba au itifaki hizo zinaporidhiwa na Bunge, bado Serikali imekuwa na ugumu wa kuleta miswada ya sheria kwa minajili ya kutunga sheria za utekelezaji wa mikataba au itifaki hizo. Mfano mzuri wa ucheleweshaji usio na tija wa kuleta mikataba ya kimataifa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge ni Mkataba huu wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani. Mkataba huu uliandaliwa tangu mwaka 2006 na nchi yetu ilitia saini makubaliano, lakini imechukua zaidi ya miaka kumi (10) kuuleta mkataba huu kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itambue kuwa nchi yetu sio kisiwa. Nchi yetu ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa na kwa sababu hiyo, inatakiwa kushiriki katika mikataba na itifaki za kimataifa ili kwenda sambamba na mageuzi makubwa katika nyanja mbalimbali yanayoendelea kutokea kila siku duniani. Bila kuwa sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, – kwa maana ya kushiriki na kuridhia itifaki za kimataifa, nchi yetu itaendelea kubaki nyuma, na hatimaye kutengwa na Jamii ya kimataifa jambo ambalo ni hatari kwa taifa changa kiuchumi.

3. MAUDHUI YA MKATABA WA KIMATAIFA WA KAZI ZA UBAHARIA WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI 2006

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani 2006 ni kuweka mazingira mazuri na salama kwa Mahabaria pamoja na wamiliki wa vyombo vya usafiri majini. Mkataba huu unalenga kuweka utaratibu wa kuwatambua mabaharia kwa kuzitaka

nchi wanachama kutoa nyaraka za utambulisho (Seafarers Identity Documents) kwa kila raia wa nchi husika ambaye atakuwa anafanya kazi za ubaharia.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu unaeleza bayana kwamba; kutokana na kuongezeka kwa vitendo nya kiharamia dhidi ya tasnia ya usafirishaji majini (shipping industry), usalama wa wasafiri, Mabaharia na vyombo vyenyewe nya usafiri majini uko hatarini. Hivyo, kutokana na hali hiyo, imebidi watu wanofanya kazi za ubaharia wapatiwe ulinzi maalum wa kimataifa ili waweze kufurahia kazi yao, kama watu wengine wanavyofurahia kazi zao kutokana na kulindwa na sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu umetambua haki za Mabaharia, wamiliki wa vyombo nya usafiri majini na haki za nchi husika ambapo kazi za ubaharia zitakuwa zinafanyika katika ngazi za kimataifa. Aidha, mkataba huu unaweka unaweka misingi ya kutambuliwa na kutendewa haki kwa Mabaharia ikiwa nchi zao zitakuwa zimeridhia mkataba huu na kutoa nyaraka za utambulisho kwa baharia husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mkataba huu ulenga kuweka mazingira mazuri ya kazi za uhaharia kimataifa,

Na kwa kuwa mkataba huu unalenga pia kuhakikisha usalama wa mabaharia, wasafiri wanaotumia vyombo nya majini na wamiliki wa vyombo nya usafiri majini ili kukabiliana na vitendo nya kiharamia dhidi ya mabaharia na vyombo nya usafiri majini,

Na kwa kuwa wapo watanzania wanaofanya kazi za ubaharia katika mwambao wa nchi yetu na katika bahari kuu, wanaomiliki vyombo nya usafiri majini vinavyofanya kazi katika mwambao wan chi yetu na katika bahari kuu na wanaosafiri na vyombo nya usafiri majini,

Na kwa kuwa nchi yetu ina mahusiano ya kibashara na mataifa mengine ambapo zipo meli za mizigo zinazoingia

katika bandari yetu kutoka mataifa mengine na nyingine kutoka katika nchi yetu kwenda mataifa mengine;

Na kwa kuwa Shirika la Kazi Duniani ni chombo cha Umoja wa Mataifa ambapo Tanzania ni nchi mwanachama,

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, Bunge hili liridhie Mkataba huu kwa kuwa una manufaa kwa nchi yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni lini italeta muswada wa sheria ya kusimamia utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

Masoud Abdallah Salim (Mb)

**KNY: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA,
AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

28 Juni, 2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hujaendelea na hiyo ya pili kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) naongeza nusu saa lakini Fasili hii inaitaka nilihoji Bunge kwa hivyo nitawahojii.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Hoja ya kuongeza nusu saa kwa ajili ya kumalizia shughuli za Bunge ilikubaliwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y MHE. ESTER A. BULAYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba

ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia namba 185 wa mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) (*Seafarers' Identity Documents Convention (Revised), 2003*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na mamlaka ya Bunge katika kuridhia Mikataba ya Kimataifa. Kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili lina mamlaka ya "kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hata hivyo, Bunge hili limekuwa likishindwa kutekeleza mamlaka hayo, kutohana na Serikali kushindwa kuleta Bungeni mikataba na itifaki mbalimbali kwa wakati kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge haliwezi kuanza kujadili na kuridhia mkataba ambao haujaletwa mbele yake. Kwa hiyo, kitendo cha Serikali kuchelewa kupita kiasi kuleta mikataba na itifaki mbalimbali Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na kutumia madaraka yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mkataba huu wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia ulitiwa saini na nchi yetu tangu mwaka 2003, lakini umeletwa leo baada ya miaka 14 kupita ili uridhiwe na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kwa miaka yote hiyo 14, Mabaharia wetu walioko katika Mataifa mbalimbali duniani walikuwa wanatambuliwaje na haki zao zilikuwa zinalindwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukomesha tabia hii ya Serikali kuchelewesha kwa makusudi au kwa uzembe mikataba na itifaki za Kimataifa zinazohitaji kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Bunge liazimie kwamba; ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu mkataba au itifaki ulipotiwa saini; Serikali ihakikishe inauleta Bungeni kwa ajili ya kujadili na kuuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia na. 185 wa 2003. Kwa ujumla mkataba huu unalenga kuwatambua mabaharia kwa kuwaandalia vitambulisho vitakavyowasaidia kutambulika na kupatiwa ulinzi na huduma nyingine mbalimbali zitakazohitajika katika nchi tofauti watakazokuwa wamekwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia ya leo ambayo vitendo vya uharamia na ugaidi vimeshamiri kuanzia mfumo wa utambuzi, utambulisho wa Mabaharia, ni jambo la msingi sana. Kwa muda mrefu Mabaharia wetu wamekuwa wakifanya kazi za ubaharia katika Mataifa mengi bila ya kuwa na vitambulisho na kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya Mabaharia hao wametekwa au wamekufa kwa kukosa kuwa na utambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo kubwa la mkataba huu ni kuwalinda mabaharia wetu dhidi ya vitendo vya kiharamia, ugaidi wa baharini; na kwa kuwa mkataba huu pia unalenga kuwapa ulinzi na msaada wa kibinadamu Mabaharia wetu; Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na inapendekeza kwamba Bunge hili liridhie Mkataba huu ili Mabaharia wetu waweze kutambuliwa na kupata ulinzi katika shughuli zao. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MAONI YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, KATIKA OFSI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA,
AJIRA NA WENYE ULEMAVU, MHESHIMIWA ESTHER AMOS
BULAYA (MB), KUHUSU MKATABA WA KIMATAIFA WA
VITAMBULISHO VYA MABAHLARIA NA. 185 WA MWAKA 2003
WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (ILO) (SEAFARERS' IDENTITY
DOCUMENTS CONVENTION (REVISED), 2003) KAMA
YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa bidii kuisimamia Serikali kwa kuikosoa na kuishauri mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mkataba wa Kimataifa ulioletwa na Seriakali kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

2. MAMLAKA YA BUNGE KATIKA KURIDHIA MIKATABA YA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili lina mamlaka ya *"kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa"* Hata hivyo, Bunge hili limekuwa likishindwa kutekeleza mamlaka hayo, kutohana na Serikali kushindwa kuleta bungeni mikataba na itifaki mbalimbali kwa wakati kwa ajili ya kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Bunge haliwezi kuanza kujadili na kuridhia mkataba ambao haujaletwa mbele yake na Serikali kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, kitendo cha Serikali kuchelewa kupita kiasi kuleta mikataba na itifaki mbalimbali bungeni kunalizua Bunge kutumia madaraka yake kwa mujibu wa ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mkataba huu wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia ulitiwa saini na nchi yetu tangu mwaka 2003, lakini umeletwala leo baada ya miaka 14 kupita ili uridhiwe na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kulieleza Bunge hili, kwa miaka yote hiyo 14, mabaharia wetu walioko katika mataifa mbalimbali duniani walikuwa wanatambuliwaje na haki zao zilikuwa zinalindwa vipi?

Mheshimiwa Spika, ili kukomesha tabia hii ya Serikali kuchelewesa kwa makusudi au kwa uzembe mikataba na itifaki zinazohitaji kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Bungeni inashauri Bunge liazimie kwamba; ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu mkataba husika ulipotiwa saini; Serikali ilete mkataba huo bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kuna mikataba mingapi ya kimataifa ambayo nchi yetu imetia saini ambayo hajajaletwa bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge.

3. MANTIKI YA MKATABA WA KIMATAIFA WA VITAMBULISHO VYA MABAHARIA NA. 185 WA 2003

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Mkataba huu unalenga kuwatambua mabaharia kwa kuwaandalia vitambulisho vitakavyowasaidia kutambulika na kupatiwa ulinzi na huduma nyingine zitakazohitajika katika nchi zilizoridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, katika dunia ya leo, ambapo vitendo vya uharamia na ugaidi vimeshamiri, kuanzisha mfumo wa utambuzi au utambulisho wa mabaharia ni jambo la msingi. Kwa muda mrefu mabaharia wetu wamekuwa wakifanya

kazi ya ubaharia katika mataifa mengine, bila kuwa na vitambulisho , na kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya mahabaria hao wametekwa au pengine kuuwawa na kwa kuwa hawana vitambulisho hatuna taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo kubwa la mkataba huu ni kuwalinda mabaharia wetu dhidi ya vitendo vyta kiharamia na ugaidi baharini, na kwa kuwa mkataba huu pia unalenga kuwapa ulinzi na msaada wa kibinadamu mabaharia wote wa nchi zilizoridhia mkataba huu, na kwa kuwa mkataba huu unalenga pia kuwapa mabaharia uhuru wa kusafiri katika Bahari Kuu na hata pwani ya nchi zilizoridhia mkataba huu; na kwa kuwa kuwa mkataba huu utafungua fursa za kibiashara kwa nchi yetu na nchi nyingine zilizoridhia mkataba huu; Hivyo, basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliishi Bunge hili kuridhia mkataba huu ili nchi yetu iwe sehemu ya dunia katika mapambano dhini ya uharamia na ugaidi dhidi ya mabaharia wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuridhia mkataba ni jambo moja lakini utekelezaji wake ni jambo la jingine; Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pia kuleta muswada wa sheria katika bunge hili, ili Bunge litumie madaraka yake chini ya ibara ya 63(3) (d) kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mkata huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

Masoud Abdallah Salim (Mb)

**KNY: MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, KATIKA OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA,
AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

28 Juni, 2017

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumeshamaliza mawasilisho. Nimepata majina machache hapa kwa ajili ya uchangiaji, sasa kwa kuwa tumepata majina machache basi watachangia hawa halafu nitamwita mtoa hoja.

Wachangiaji hawa kila mmoja ameomba dakika tatu kwa hiyo Katibu, uzingatieve.

Mheshimiwa Salum Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Machano Othmani Said na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata muda huu wa kuchangia kwenye mawasilisho haya. Kwanza nipongeze kuletwa huu Mkataba ambao utaweza kusaidia kurekebisha kasoro nyngi zinazotokea kwenye sekta hii ya *marine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza hasa kwenye mambo machache kwa sababu ya muda, hasa suala zima la Mabaharia ambao wanasafiri na vyombo ambavyo vya kuchukulia hasa mizigo kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara na vile vingine vinaenda Mafia na vingine vinaenda mpaka Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaharia hawa hawana mikataba rasmi, lakini vyombo vile vinakaguliwa na *SUMATRA*, vinapewa leseni ya kusafirisha mizigo, lakini uhalali wa ufanyakikazi wao katika zile meli haupo. Mtu unaweza kuingia leo kazini kesho ukasimamishwa, ukakoseshwa mshahara na mambo mengine ambayo hayastahiki kufanyiwa wafanyakazi hasa wa meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile suala zima la vyombo ambavyo vinasafirisha abiria hasa katika bandari zile ndogo ndogo mfano Mkokotoni kuja Tanga, Kipumbwi nao vilevile wale Mabaharia wanaofanya kazi ndani ya vyombo vile zile *fiber*, boti ndogo ndogo hakuna mikataba ya ufanyakiji kazi katika meli zile au boti zile ambazo zinakwenda katika maeneo yale. Linapotokezea lolote Baharia yule anakuwa hatambuliki, anayetambulika pale ni mwenye chombo au Nahodha kwa kiasi kidogo sana. Naomba vilevile hili Waziri aje atupe maelezo hatua gani *SUMATRA* itazichukua kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye hili ni suala zima la wanafunzi ambao wanasoma katika Chuo cha Marine kile kilichopo Dar es Salaam, wanafunzi wale wanapata nafasi ya kwenda kufanya kazi katika meli za nje, lakini ikifika muda kutaka kuja *ku-renew* zile leseni zao, pale kwenye kile chuo wanatakiwa wasome tena...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machano Othman Said atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo tutamallizia na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niishukuru Serikali kwa kuleta Azimio hili la kuridhia Mkataba wa kazi wa Mabaharia, Mheshimiwa muda ni mchache sana, kwa hivyo nitazungumza kwa haya mambo mafupi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, imekuwa ni kawaida kwa Tanzania kutohudhuria vikao vingi vya IMO na pia Shirika la Kazi Duniani kuhusu Mabaharia. Bahati nzuri nchi yetu ina bahari kubwa na ina fursa nydingi sana katika eneo hili, kwa hiyo naomba Serikali isidharau. Mimi mwenyewe nilishawahi kuhudhuria vikao kama vinne vya IMO lakini upande wa Bara hawakushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tukiridhia Azimio hili la mkataba huu tutanufaika sana, kwa sababu tuchukulie mfano Zanzibar kwa kupitia mamlaka ya usafiri baharini wamesajili meli karibu 400 duniani na kila meli sasa hivi wanatozwa dola 500 kwa sababu bado Tanzania hatujaridhia mkataba huu na kiasi kama dola 200,000 kila mwaka zinalipwa na ZMA kwa ajili ya suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nafurahi kwamba Serikali inaridhia itatuwezesha Tanzania kwa ujumla kuongeza idadi ya Mabaharia lakini pia kutoa fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la ubaharia ni eneo pana sana na linaweza kutusaidia. Bahati nzuri Tanzania tuna vyuo viwili vinavyotambulika duniani, tuna Chuo cha DANAUSE kiko Zanzibar na tuna chuo cha DM/Dar es Salaam. Vyuo hivi wanatoa *certificate* na zinatambulika na vinatoa ajira kwa vijana wetu. Kwa hivyo niiombe Serikali kwamba ni wakati muafaka sasa tuseme kwamba tumechelewa kidogo, lakini maadam leo limeletwa hakuna tatizo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote tutaridhia na sisi ili kuwezesha nchi yetu isonge mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba nimalizie hapo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Mbogo, tutamalizia na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nichangie Azimio la Kuridhia Mkataba wa Mabaharia nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kuleta hili Azimio kwa sababu limekuja wakati muafaka, tumekuwa tukiona vijana wa Kitanzania wamekuwa wakipata shida huko nchi za nje wanapokwenda kufanya kazi za ubaharia. Pia wamekuwa wakipoteza mali zao kwa sababu Tanzania ilikuwa haijaridhia hii mikataba ambayo ni mikataba takribani 37 ambayo Tanzania ilishindwa kuridhia kwa muda wa miaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuunganisha Mikataba hii 37 kuleta mkataba huu itawawezesha vijana wetu wa Kitanzania kupata ajira kirahisi kwenye meli za nje, itawawezesha pia Tanzania nchi yetu kusaidia kwenye ajira za kazi kwa

sababu tuna ukosefu wa ajira vijana wetu wataweza kuajiriwa nje na Serikali itaweza kupata manufaa zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo angalizo dogo kuhusu sheria ambazo zitatumika kwa sasa hivi tunazo sheria za *SUMATRA*, pia tunazo sheria za Zanzibar kwa sababu tunakwenda kuingia Mkataba wa Kimataifa itabidi Serikali ilete hizi sheria izirekebishe maana yake *flag country* itakuwa ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar wanasa jili meli wanaye *Agentanayesajili* hizi meli kule Dubai, lakini *SUMATRA* hawana. Ningombaa Serikali ijaribu kuliangalia hili suala kwa sababu mkataba huu hautaonesha kwamba hii meli imesajiliwa na Zanzibar na hii imesajiliwa Tanzania Bara, inabidi sheria hizi ziunganishwe kwa pamoja za ZMA na *SUMATRA* kwa sababu mkataba ni wa Kimataifa, kitakachokuwa kinaleweka hapa ni *sovereignty of the state* ambayo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haitakuwa busara kwamba sasa hivi hii meli imesajiliwa na Zanzibar, kwa hiyo ikipata pale matatizo tutasema kwamba hii meli ilisajiliwa na ZMA au hii ilisajiliwa Tanzania Bara, ningombaa uoanisho wa hizi sheria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho....

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imegonga Mheshimiwa.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio hili. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi atamalizia Mheshimiwa Mtolea.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nipongeze Serikali kwa kuleta mkataba huu,

niseme tu kwamba mkataba huu umechelewa sana. Sisi kule Tanga tumepteza vijana wengi sana kwa sababu ya kuchelewa kusaini mikataba kama hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi walikuwa wanajihuisha na shughuli za madawa ya kulevyia wanapozamia kwenye meli kwa ajili ya shughuli za ubaharia. Kwa mkataba huu naamini sasa kwamba kwa kuwa kazi za ubaharia zinaenda kutambuliwa rasmi ndio utakapoona tofauti kwa kazi ambazo ni rasmi na zile kazi za kishoka utaweza kuona kwamba tukiwa na mikataba rasmi kama hii basi shughuli nyingi zitakazofanyika zinalinda pia maslahi mapana ya usalama wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri Serikali kwamba kwa kuwa mkataba huu ni wa Kimataifa na pia tunayo maziwa katika mipaka yetu na milpaka hii tunapakana na nchi mbalimbali. Kwa upande wa Ziwa Victoria tuna Kenya na Uganda; Ziwa nyasa kuna Malawi na Zambia; na Tanganyika kuna Burundi na Congo na hapa nimeona Congo wameridhia mkataba huu mwaka 2015. Nitoe rai kwamba kwa kuwa nao kwenye maziwa haya pia kuna vyombo hivi vyaya usafirishaji basi tujaribu *ku-harmonies* na hizi sheria pia zitumike kwenye vyombo ambavyo vinasafiri katika maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumejifunza kwenye Kamati kwamba wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wana chombo maalum cha kusajili vyombo vyaya majini, sasa huku kwetu tuna *SUMATRA* ambao wanasa jili vyombo vyaya majini na vyombo vyaya nchi kavu. Ningependa sasa kuishauri Serikali kwamba ifikie mahali tutenganishe hivi vitu kwa sababu tunaona mara nyingi sana kwenye maziwa huku kunatokea maafa makubwa labda ni kutokana kwamba *SUMATRA* wako *busy* zaidi na vyombo vyaya nchi kavu kuliko vyombo vyaya majini. Kwa hiyo, nitoe rai kwamba kwa kutumia mkataba huu sasa tuweze kupanua wigo wa kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo niseme kwamba hii ni fursa nzuri sana kwa vijana wetu kupata ajira,

lakini ni fursa nzuri pia kwa utambuzi wa Kitaifa kama alivyomalizia msemaji wa mwisho hapa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa inatumia wakala kusajili meli na ndio maana unakuta wakati mwingine hata hizi meli zinahusishwa na uharamia, lakini pia zinahusishwa na mambo mabaya ambayo yanachafua taswira ya Taifa. Sasa ni imani yetu kwa mkataba huu kila kitu kitawekwa katika utaratibu ambao ni mzuri kwa ajili ya kulitangaza Taifa letu katika Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono azimio hili. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Nami niungane na waliotangulia kusema Wizara imefanya vizuri kuleta mikataba hii ili iweze kuridhia sasa kwa kuwa imechelewa kufanya hivyo kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji sasa kuwa na uangalifu wa hali ya juu kwamba lengo la kuridhiwa kwa mikataba hii ni kupunguza wimbi la uharamia huko baharini hasa bahari kuu. Sasa tunapokwenda kutoa vitambulisho kwa ajili ya kuwatambua wavuvi wetu tunahitaji kuwa na umakini wa hali ya juu sana kwa sababu vinginevyo wahalifu kutoka Mataifa mengine watajipenyeza na wao wapate vitambulisho hivi kutoka nchini kwetu ili waende kuvitumia vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hatupaswi kuweka urasimu mkubwa ambao utawafanya sasa wavuvi wetu kwa maana ya Watanzania ambao wanastahili kupata vitambulisho hivi waanze kupata usumbufu mkubwa wa kuvipata, ni lazima tutengeneze utaratibu mzuri ambao hautakuwa na usumbufu ili wavuvi wetu waweze kuvipata vitambulisho ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia ni jambo moja, tunahitaji pia sasa iletwe sheria ambayo tuje tuijishe hapa kwa ajili ya utekelezaji wa mikataba hii. Kwa sababu kama tutairidhia leo, lakini sheria ya kusimamia utekelezaji wake na wenyewe utachukua miaka 10 bado tutakuwa hatujaenda kumaliza tatizo, Kwa hiyo, niishauri Serikali ifanye hivi kwa wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtoha hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwashukuru sana Wabunge wote waliochangia, wote wameunga mkono hoja hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuunga mkono hoja yetu ya leo humu ndani Bunge tunaendana pia na kilio cha Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (*TUCTA*), lakini na Vyama vya Wafanyakazi ambavyo vimekuwa vikisimamia sekta ya mabaharia nchini, wamekuwa wakililia sana jambo hili Bunge letu Tukufu liweze kuridhia na hivyo leo wanavyotusikia kwa pamoja, ninaposema kwa pamoja , ukisikiliza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni leo wameunga mkono Maazimio yote haya mawili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nichukue nafasi hii kumpongeza sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa sababu si kwamba kila jambo jema linalofanywa na Serikali ni lazima kupinga, mambo yanayofanywa na Serikali kama ni jambo jema lina faida kwa Watanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inapounga mkono huu ndio uungwana na huu ndio mwenendo mzuri wa uwakilishi wetu ndani ya Bunge kwa kuhakikisha kwamba tunawawakilisha Watanzania wote. Namshukuru sana Mheshimiwa Mtolea kwa kuliona jambo hili ni la msingi kwa manufaa ya Watanzania wote na kuunga mkono hoja yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati nzima. Wamefanya kazi kubwa sana, Kamati hii na kwa namna ya ajabu kamati ilianza kukutana na wadau mbalimbali, iliamua kuchukua hatua ya kujielimisha kwa kina namna nzuri ya kuendana na hoja ambayo Serikali ilikuwa imeipeleka kwenye Kamati, kwa kweli naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niishukuru sana Kamati na maoni yao yote tunayachukua na tutayazingatia katika kutekeleza mkataba wenyewe baada ya kuridhiwa na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nizungumze kidogo kuhusu maoni ya Kambi ya Upinzani; Kambi ya Upinzani wao wamesema kwamba ni kwa nini tunachelewa kuleta mikataba ndani ya Bunge ili iweze kuridhiwa. Kama Serikali ni lazima baada ya kusainiwa kwa mikataba ni lazima Serikali tufanye kwanza tafiti za kina tujiridhishe kabla ya kuridhia kweli mikataba hiyo inaendana na hali halisi ya mazingira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tujiridhishe, tufanye tafiti za kutosha, tuangalie sera tulizonazo katika nchi yetu, tuangalie uzoefu wa Mataifa ambayo wamekwisha kuridhia, tuone changamoto ambazo wenzetu wanazipata, kusudi sisi tunapokuja kufanya kazi ya uridhiaji angalau tuone tuko kwenye *position* ya kujihakikishia kwamba hatutakuwa na shida ya utekelezaji wa mkataba wenyewe ndani ya nchi ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mtolea kwamba, tunafanya hiyo kwa nia njema na sio kwamba tunachelewesa kwa makusudi hapana. Tumekuwa tuna uzoefu baadhi ya mikataba ukiangalia unakuta inakinzana kwa namna moja ama nyingine na mazingira halisi ya utendaji wa kazi na usimamizi wa shughuli mbalimbali za kisheria na za kisera ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutakuwa

tunajitahidi kufanya tafiti za kutosha na tunapokwenda kuridhia mikataba tunaridhia tukiwa na uhakika Watanzania watanufaika na kila kila kitu tutakachokiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Salum Rehani, Mheshimiwa Mbunge amezungumza sana masuala ya leseni kwenye vyombo vyetu vya majini na namna gani pia mabaharia wetu wanaofanya kazi kwenye vyombo vya majini wanavyokosa mikataba ya ajira na mambo mengine ambayo yangeweza kuwapa haki stahiki kama wafanyakazi katika vyombo vya majini. Naomba nimhakikishie kwamba kwa kuridhia mkataba huu kwanza tutakwenda kuweka mfumo mzuri ambaao utawasaidia sana Mabaharia kutambulika ndani na nje ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaharia wetu wengi ambaao walikuwa wanapata ajira kwenye vyombo vya usafiri na hasa vyombo vya nje walikuwa wanadharauriwa sana, hawakuwa wakipata haki, walikuwa hawatambuliki Kimataifa, kwa hiyo, walikuwa wanapata shida sana. Hata hivyo, mkataba huu sasa unatupa sisi nafasi ya kuzitazama sheria tulizonazo ili kuwafanya Mabaharia wetu wanapopata vile vitambulisho sasa waweze kutambulika hata kwenye medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wale Mabaharia wanaofanya kazi ndani ya nchi yetu ya Tanzania kwa kutumia vyombo tulivyonavyo ndani ya nchi yetu ya Tanzania na sheria tulizonazo, tutaendelea kusimamia. Namhakikishia Mheshimiwa Salum Rehani kwamba, sasa tumepata nguvu mpya ya kuhakikisha kuwa tasnia hii ya kazi ya Mabaharia inakuwa ni kazi yenye staha, yenye heshima na inayotoa fursa kwa vijana wa Tanzania kujiajiri na kuajiriwa na kupata haki na stahiki sawa ndani na nje ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana umeunga mkono na wewe na umeona jambo lenyewe lina msingi kwa hiyo naomba nimshukuru kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka Mheshimiwa Machano ametukumbusha *IMO* ni muhimu na hasa sisi upande wa Bara, tuwe tunashiriki, namhakikishia kwamba tutaendelea kufuatilia vikao hivyo na kushiriki kwa manufaa ya nchi yetu. Hata hivyo, ametukumbusha pia kwamba kumekuwa na shida ya usajili wa meli na tozo ambazo zimekuwa zikitolewa wakati wa usajili wa meli na amefurahi sana mkataba huu sasa utakwenda kutatua matatizo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwamba baada ya kuridhia tutakwenda kukaa ndani ya Serikali, chombo kimoja na kingine kinachohusika na mkataba huu ni lazima huko mbele tutakwenda kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuhakikisha kwamba mkataba unaendana na sheria tulizonazo ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, tutatoa fursa nydingi kwa vijana wa Tanzania na kupata ajira za ubaharia katika vyombo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Pia nakubaliana na yeye, kwamba tunavyo vyuo vinavyofundisha tasnia ya ubaharia bara na visiwani katika nchi yetu na ni vyuo vizuri, vinatoa Mabaharia wazuri na wamekuwa wakitambulika ndani na nje ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu unatuimarishe kwa sababu unatoa fursa ya kupata utaalami kutoka nje ukaletwa tena na kwenye vyuo vyetu vya ndani na kuwafanya mabaharia wetu waweze kubobe katika medani za ndani na nje ya Tanzania. Kwa hiyo, mkataba huu kwa kweli ni mzuri sana na utatoa fursa nzuri sana kwa Mabaharia wetu na vijana wetu wa Tanzania wanaotaka kufanya kazi kwenye tasnia hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa dada Taska amepongeza vijana wengi sasa angalau ajira zao zitakuwa za staha na zitaweza kutambulika vizuri, nakubaliana na yeye. Ametoa hapa rai kwamba ni lazima tuangalie sheria za usajili wa meli na vitu vya namna hiyo. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Taska kwamba, Serikali inalichukua kwa sababu ni suala ambalo litabidi lifanyiwe mazungumzo ya pande zote mbili za Muungano. Tutaendelea kujadiliana na kuona

namna nzuri ya kurekebisha utaratibu na mifumo yetu ili pande zote mbili za Muungano ziweze kufaidika na mkataba huu, lakini na sheria zote ambazo zinasimamia masuala yote ya usajili wa meli lakini na masuala ya ajira kwa vijana wetu kwenye tasnia hii ya ubaharia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shangazi amezungumza hapa kwa urefu na amesema tumechelewa. Ni kweli tumechelewa lakini tumechelewa kwa makusudi maalum nimesema hapo mwanzo na lengo letu lilikuwa ni kujiridhisha kile tunachoenda kufanya kama kweli kitaendana na hali halisi ya mazingira katika nchi yetu ya Tanzania lakini kitakuwa na tija kwa Watanzania ambao wameingia kwenye tasnia hiyo ya ubaharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ametukumbusha hapa kwamba ni lazima tuangalie tunalinda mipaka yetu kwa sababu kuna vyombo ambavyo vingine vimesajiliwa na vitatakiwa kuendeshwa na mabaharia lakini viko katika maji ya maziwa kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, ametukumbusha ni lazima tuhakikishe vinasajiliwa kwa sheria tulizonazo kuepusha ajali na usalama wa abiria, vilevile mabaharia wanaoendesha vyombo hivyo waweze kuwa na viwango vinavyotambulika. Naomba nimwambie Mheshimiwa Shangazi kwamba, tunalichukua hilo na tutalizingatia kwa sababu hata mkataba wenyewe ndio unatutaka tufanye hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Shangazi ametuambia kwamba ni lazima tuangalie fursa nzuri za kuwatambua Mabaharia tulionao katika nchi yetu Kitaifa na Kimataifa na tuwe na *data* maalum ya kufanya hivyo, mkataba unatuagiza kuandaa *database* ya kuwatambua Mabaharia wetu. Kwa hiyo, tutafanya hivyo na tutaweka mfumo na mkataba umetuelekeza Nchi Mwanachama atakayeridhia ni lazima afunque *database* ya kuwatambua Mabaharia wote. Hiyo pia itatusaidia kuondoa nafasi za kuwepo na Mabaharia ambao watajiingiza katika masuala mengine kama ya uharamia na vitu vingine vya ugaidi na kahdalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namwambia Mheshimiwa Shangazi tutayazingatia hayo maoni aliyojasema. Nakumbuka aliyazungumza sana wakati wa Kamati nikiwa pale na naomba tu kumhakikishia kwamba tunayachukua na tutayafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mtolea amezungumza kwamba tuangalie ni namna gani tunawasaidia wavuvi katika kupata hivi vitambulisho. Naomba tu niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, vitambulisho hivi kwanza ni kwa ajili ya Mabaharia lakini wavuvi nao hawakatazwi kusomea ubaharia katika vyuo vyetu na wao wakapata vitambulisho hivi na wakaweza kufaidika na mkataba huu lakini tasnia ya ubaharia katika nchi yetu. Vile vile ametuagiza na ametuomba tuharakishe sana kuona sheria zetu tulizonazo zinaweza kuendana sambamba vipi na mikataba hili tuliyoridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, kama nilivyosema mwanzo wakati nawasilisha, tayari tunazo sheria kwa pande zote mbili Bara na Visiwani. Vilevile tunayo nafasi nyingine nzuri baada ya uridhiaji na kuwasilisha hati *ILO* tukaangalia pia je, sheria hizi sasa zinaendelea kuwa rafiki kwenye mikataba hii? Kama hazzioneysi kuwa rafiki basi Bunge hili tutakuja kwenu tutashirikiana na nyie. Lengo letu siku ya mwisho ni kuwafanya Watanzania waweze kunufalika na kufaidi fursa hii muhimu ya kazi za staha kwenye tasnia hii ya ubaharia ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kusema hivyo, naomba sasa kutoa hoja Maazimio haya ya Bunge yote mawili kwa pamoja yaweze kuridhiwa na Bunge lako Tukufu ili yaweze kuendelea na hatua nyingine zinazostahiki kwa manufaa ya nchi yetu na kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono asanteni sana. Waheshimiwa sasa nitawahoji Azimio moja baada ya lingine. Kwanza nitawahoji kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organization (ILO) - Maritime Labour Convention, 2006*).

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Waliosema ndio wameshinda, kwa hiyo Bunge limeazimia na kuridhia mkataba husika.

Sasa nitawahoji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Vitambulisho vya Mabaharia Na. 185 wa Mwaka 2003 wa Shirika la Kazi Duniani (*International Labour Organization (ILO) – Seafarers Identity Documents Convention (Revised, 2003)*).

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Azimio hili pia limepita. (*Makofii*)

Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu na timu yake kwa haya Maazimio ambayo Bunge limeridhia na tuwatakie kila la heri katika utekelezaji. Tunaamini kwamba vifungu vile vitakavyohitaji mabadiliko ya sheria, basi mtafanya hivyo na vile ambavyo vitahitaji sheria mahususi basi mtazileta Bungeni ili Bunge liweze kufanya kazi yake.

Waheshimiwa Wabunge tulikuwa na jambo ambalo nilikuwa nimesema kwamba ningeliamua baadaye baada ya kusikia meza ya Makatibu. Sasa tutaanza jambo moja baada ya lingine kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za Bunge vizuri.

Tutaanza na jambo linalomhusu Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza la kusema uwongo Bungeni, Kamati kama tulivyosikia taarifa ilioleta, Kamati imependekeza kumsimamisha Mheshimiwa Rwamlaza vikao vitatu vya Bunge hili la Bajeti.

Ukisoma Kanuni ya 63(8) Kamati ilichofanya imemshauri Spika kwa sababu kwa kutumia Kanuni ya tano (5) na 72 Spika aliona umuhimu wa Kamati hii kumsaidia kujiridhisha kama Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alichosema Bungeni ulikuwa ni uwongo ama aliweza kuthibitisha.

Sasa baada ya kupeleka jambo hili kwenye Kamati, Kamati imeridhika kwamba Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza hakuweza kuthibitisha na kwa hivyo kiti pia kinaridhika na mapendekezo ya Kamati kwa maana ya kwamba Bunge halijaridhishwa kwa sababu kiti ndio kinachotakiwa kuridhishwa kwa mujibu wa kanuni ya 63.

Sasa kiti kinapokea maoni ya Kamati kwamba hakuweza kutoa ushahidi wa kuonesha namna gani Mheshimiwa Tibaijuka alikuwa amejipa hekta hizo kama yeye alivyokuwa amesema. Fasili nane(8) nitasoma sehemu tu kwa sababu ya muda inasema

"basi Spika atamwadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi vitano"

Kwa hivyo Kamati imemshauri Spika kwamba, Mheshimiwa huyu aadhibiwe kwa kusimamishwa vikao vitatu, kwa maana hiyo havizidi vitano.

Fasili ya tisa (9) inasema inatoa fursa kwa Mbunge mwingine kutoa adhabu kubwa zaidi kama ikionekana adhabu hii haitoshi na ukisoma fasili ya tisa (9) inaeleza kama ni kosa lake la kwanza, basi Mbunge anaweza akasema asihudhurie vikao vya Bunge visivyozidi kumi na hili ni kosa la kuhusu kusema uwongo sio kosa la kudharau Kiti cha Spika. Kosa la pili na lenyewe ni vikao visivyozidi 20 ama achukuliwe

hatua nyingine za kinidhamu zitakazotajwa katika hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma fasili ya tisa (9) na ya 10 kwa pamoja utagundua kwamba Mbunge ambaye anaadhibiwa na Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(8) ikitolewa hoja chini ya fasili ya tisa (9) Mheshimiwa Mbunge anapaswa apewe fursa ya kujitetea.

Kwa kuwa tulishawahi kufanya maamuzi huko nyuma ya Wabunge kadhaa na hapa naweza kuwataja wachache ambao waliwahi kusema uwongo na adhabu zao zilikuwa zinafananaje kwa mujibu huo huo wa kanuni ya 63(8) tuliweza kuwaadhibu Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa James Milly ambao walikuwa pia wamefanya kosa la kuzungumza uwongo Bungeni na tulipowapeleka kwenye Kamati wakashindwa kuthibitisha wakaadhibiwa kwa mujibu wa fasili ya nane (8).

Sasa matumizi ya fasili ya tisa (9) yangeweza kutoa fursa kwa kile alichokifanya Mheshimiwa Musukuma cha kuonesha kwamba yeye adhabu ambayo imependekezwa hakubaliani nayo, lakini kwa kuwa fasili ya 10 inatutaka Bunge kabla hatujafanya maamuzi tumsikilize yule ambaye anapewa adhabu ili aweze kujitetea, kwa mamlaka hayo niliyonayo chini ya kanuni ya 63(8) naridhika na adhabu ambayo Kamati imependekeza. Kwa hivyo Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza amesimamishwa Bunge kwa vikao vitatu.

Waheshimiwa Wabunge, hili ni la kuhusu kusema uwongo Bungeni ambayo kanuni inayohusika ni 63 na 64 kwa hivyo hilo tunalimaliza hivyo na kwa mujibu wa kanuni zetu wala sihitaji kulihoji Bunge kwa sababu mimi ndiye ninayetua adhabu kwa kanuni zetu zinavyosema. Kwa hivyo, nimekubaliana na mapendekezo ya Kamati kuhusu Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Kuhusu Mheshimiwa Nassari kosa lake yeye haliko chini ya kanuni ya 63 kosa lake liko chini ya kanuni ya 74 kosa ambalo ni la kudharau Mamlaka ya Spika. Kwenye kosa hili kamati imependekeza kwa kutumia taratibu ambazo tumeshazifanya huko nyuma ambalo baadaye nitawahoji kwa sababu hili linataka niwahoji maamuzi ambayo tutafikia pamoja.

Kanuni ya 74 inazungumza nini cha kufanya Mbunge anapodharau Kiti cha Spika na akapelekwa kwenye Kamati. Kamati katika hekima zake na kwa kutumia hayo maamuzi ambayo yameshawahi kutolewa huko nyuma kuhusu kosa kama hili Kamati imependekeza kwamba Mheshimiwa Nassari asamehewe.

Kwenye hili Mheshimiwa Musukuma pia alikuwa na hoja kwamba Mheshimiwa Nassari asisamehewe lakini wakati akitoa hii hoja yake ambayo ningeweza sasa kuihoji Bunge kama linakubaliana na hoja ya marekebisho ya Mheshimiwa Musukuma kulitokea shida kidogo katika haya mapendekezo yake, kwa sababu yeye amesema ni kosa la pili kwa Mheshimiwa Nassari kwamba amedharau Mamlaka ya Spika.

Hata hivyo, ukizisoma kanuni makosa hata haya ukichukua kusema uongo na ukichukua kudharau mamlaka ya Spika namna kanuni zetu zilivyo zinahesabu kosa la pili kama kanuni iliyotumika kukuadhibu ni hiyo. Ndio maana kanuni ya 63 inaeleza utaratibu na kanuni ya 74 pia imeweka utaratibu wake peke yake.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye hoja aliyoitoa Mheshimiwa Musukuma ilikuwa inasema ni kosa la pili kwa hivyo ikatoa mapendekezo ya kutumia kanuni ya 74(3)(b). Nimepata taarifa kwamba kosa la kudharau mamlaka ya Spika kwa Mheshimiwa Nassari kwa Bunge hili ni la kwanza kama Kamati ilivyozungumza. Kwahiy, pendekezo la Mheshimiwa Musukuma linakuwa limeenda kinyume kidogo na kanuni kwa sababu imetaja kwamba hili ni kosa la pili wakati ni kosa la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kanuni yetu ya 74 inatoa huo utaratibu kwa Kamati kuleta kwa Bunge na kulishauri Bunge nini cha kufanya, Kamati imeshaleta maazimio yake. Kwa kufuata utaratibu mzuri wa uendeshaji Bunge tunayo mambo mawili hoja iliyoko mbele yetu ni ya Kamati na mapendekezo yake.

Mapendekezo aliyotoa Mheshimiwa Musukuma ya kubadilisha adhabu hii kwa mujibu wa kanuni zetu tulizonazo yaani 57 na 58 ili yeye aweze kuleta hayo marekebisho, kama nilivyosema marekebisho haya yanaleta tabu kidogo kwa sababu yanataja kosa hili kuwa ni la pili wakati ni la kwanza. Sasa nitarejea kwenye kiti ili niweze kulimaliza jambo hili kwa kuwahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu adhabu ya Mheshimiwa Nassari halafu mwishoni nitamalizia na maelezo ya jumla.

Waheshimiwa Wabunge, nitawahoji kwa sababu marekebisho haya hayajatimiza matakwa yetu ya kikanuni nitahoji wanaokubaliana na hoja ya Kamati ya kumsamehe Mheshimiwa Nassari.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Walioafiki hoja ya Kamati wameshinda, kwa hivyo Mheshimiwa Joshua Nassari anasemehewa kama Kamati ilivyopendekeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu sasa ya jumla na haya ni ya Wabunge wote kwa sababu Bunge ndio linaloamua pia Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, utaratibu ambao pengine ulianza hapo nyuma wa kusamehe watu wanaofanya makosa chini ya kanuni ya 74 na kuwafanya wanaofanya makosa chini ya kanuni ya 63 wao hata kosa la kwanza hawapati msamaha, ni kana kwamba makosa yanayofanyika humu Bungeni yamepewa uzito tofauti, wakati yote ni makosa.

Sasa niombe Kamati iangalie namna bora ya kushughulika na hili kwa sababu kanuni ya 74 inazungumzia Mbunge kudharau Mamlaka ya Spika. Sasa haiwezekani Mbunge kudharau mamlaka ya Spika likaonekana ni kosa dogo akifanya la kwanza anasemehewa, halafu kosa la kusema uwongo Bungeni kuhusu Mbunge mwingine linaonekana kwamba hilo ni kosa kubwa sana yeche la lazima aadhibiwe hata kwa kosa la kwanza.

Kama ambavyo Kamati imesema na mimi nimetaja hapa baadhi ya majina utaratibu umekuwa hivyo. Wabunge wanaofanya makosa chini ya kanuni ya 74 likiwa kosa la kwanza wengi wao wanasamehewa lakini chini ya kanuni ya 63 hata la kwanza hawasamehewi. Niombe muyapime haya makosa kwa uzito huo kwa sababu Mbunge anapodharau mamlaka ya Spika pengine ni zito zaidi kuliko hata la kudanganya kuhusu Mbunge mwingine. Kwa hivyo, hilo ningeomba militazame. (*Makofi*)

Lingine ambalo pia ni la jumla ni kuhusu hiyo hiyo kanuni ya 74, kwa sababu kanuni ya 74 imetaja adhabu kama ambavyo kanuni ya 63 imetaja adhabu. Ningeomba kwa kuzingatia yale ambayo tumeyapata kutokana na mjadala wa baada ya mawasilisho ya Kamati tuangalie namna bora ya matumizi ya kanuni ya 74 kwa sababu na yenyewe imetaja adhabu kwa kuangalia kwamba Mbunge anapofanya kosa anapaswa kuadhibiwa kwa sababu ukiisoma pamoja na kwamba huu ndio umekuwa utaratibu, imetaja kosa la kwanza adhabu ni ipi kama ambavyo kuhusu uwongo imetaja kwamba kosa la kwanza adhabu ni ipi.

Kwa hiyo, naomba tuangalie haya yote kwa pamoja ili tusijikute kwamba tunayafanya makosa mengine ni madogo kuliko mengine. Pamoja na kwanza Bunge limeshawahi kuamua maamuzi huko nyuma na ukisoma kanuni ya tano (5) inaweza ikatoa mwongozo kidogo. Kamati ina uwezo wa kuondokana na hayo maamuzi ya nyuma hasa pale ambapo sheria na kanuni iko wazi kuhusu kosa husika na adhabu inayotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tumefika mwisho shughuli zetu za leo, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi, tarehe 29 Juni.

*(Saa 7.40 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 29 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*